Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Tatu - Tarehe 15 Aprili, 2004

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka 2003.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2003.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):**

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa Mwaka 2003.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje kwa Mwaka 2003.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA (k.n.y. MHE. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2003.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kwa Mwaka 2003.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

**Mafanikio ya Mfuko wa *TASAF***

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mfuko wa *TASAF* umefanikisha vizuri miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya zilizofadhiliwa na mfuko huo katika awamu ya kwanza; na kwa kuwa Wilaya zilizobaki, ikiwemo Wilaya ya Liwale zilitarajiwa kufadhiliwa na mfuko huo katika awamu ya pili kwa mwaka 2003; na kwa kuwa hayo hayajafikiwa hadi sasa:-

(a) Je, ni sababu gani zilizocheleweshа utekelezaji wa awamu ya pili ya mfuko huo?

(b) Je, ni lini sasa mfuko huo utaanza awamu ya pili ya kufadhili miradi ya maendeleo ya Wilaya zilizosalia ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Liwale?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, ningependa kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mfuko wa Huduma za Jamii *(TASAF),* kama mkakati mmojawapo wa kuondoa umaskini ulianza kufanya kazi hapa nchini mwaka 1999 kwa majaribio katika Wilaya nane za Tanzania Bara. Dhana kuu ya ufadhili wa *TASAF* ni ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo. Hivyo, awamu ya majaribio pia ilihusu mafunzo katika fani ya mbinu shirikishi. Ufadhili wa Miradi ya *TASAF* ulipanuliwa hadi kufikia Wilaya 40 za Tanzania Bara na visiwa viwili vya Zanzibar (Unguja na Pemba) mwaka 2000. Awamu hii ilipangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka minne, yaani Novemba, 2000 hadi Desemba, 2004. Utekelezaji wa miradi inayogharamiwa na *TASAF* umeonyesha mafanikio ya kuridhisha, kwa maana ya kupunguza kero za wananchi na pia kwa maana ya dhana yenyewe ya ushirikishwaji.

Mafanikio haya yameonyesha kuwa kuna haja ya kuendelea kutekeleza Miradi ya *TASAF* ili dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika hatua zote za mipango ya maendeleo ieleweke na kutumika katika sekta zote za maendeleo. Ushirikishwaji unalenga zaidi kujenga uwezo wa jamii katika hatua zote hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo ya ujumla, ufadhili wa Mfuko wa *TASAF* ulianza katika sehemu chache kwa majaribio. Lengo la majaribio lilikuwa kupata uzoefu wa utekelezaji wa dhana ya *TASAF* yaani ushirikishaji wa wananchi katika hatua zote za mradi. Hatua hizi ni pamoja na uibuaji wa miradi (kero) kwa mbinu shirikishi, dhana ambayo inahitaji muda wa kutosha na utaalam katika kutoa mafunzo. Aidha, kama nilivyoonyesha katika maelezo ya ujumla, awamu hii ilipangwa iishie Desemba, 2004. Hivyo, kwa mujibu wa makubaliano ya awali hukuna ucheleweshaji uliotokea.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na *TASAF* katika Wilaya 40 za Tanzania Bara na Visiwa vya Zanzibar na Pemba kuonyesha mafanikio, Serikali imeamua shughuli za mfuko huu zisambae nchi nzima. Tayari Serikali inawasiliana na Benki ya Dunia, kwa nia ya kuanza utekelezaji wa awamu ya pili mwanzoni mwa mwaka ujao wa 2005. Aidha, Serikali imeanza maandalizi ya awamu ya pili ya *TASAF*.

(c) Mheshimiwa Spika, matarajio ya awamu ya pili ni kuwa na mradi utakaotekelezwa kwa muda usiopungua miaka minne kuanzia mwaka 2005. Aidha, lengo kubwa katika kipindi hiki ni kuhakikisha kuwa pamoja na kutatua kero za wananchi, sekta zingine zinaiga mfano wa utekelezaji wa Miradi ya *TASAF* kwa kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika kubuni, kutekeleza na kusimamia maendeleo yao.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Nashukuru kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu hayo mazuri ningetaka kujua ni kigezo gani kilitumika kwa wale waliokuwa katika awamu ya kwanza ya mradi huo?

Pili, ningetaka kujua awamu hiyo nyingine ya Wilaya zote zitaingia lini hasa tupate *time frame* kuliko kusema tu mwaka 2005, lini mwezi Januari, Februari au Desemba? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema, *TASAF* ni mkakati mmojawapo ambao umebuniwa na Mheshimiwa Rais katika mkakati mzima wa kuondoa umaskini. Ni mfuko mmojawapo ambao unashirikisha wananchi kwa madhumuni hayo. Kwa hiyo, kigezo kilichotumika kwanza lazima tukubaliane kila mmoja anapenda mradi kama huu, kila mmoja wetu hapa angependa kwenye Jimbo lake mradi kama huu utekelezwe.

Lakini vigezo ambavyo vinatumika pamoja na hata na mfuko ule wa *SELF* ni kuchukua zile Wilaya ambazo ziko chini sana katika maendeleo kwa maana unapima umaskini wao kwa vigezo mbalimbali na Wilaya zilizochukuliwa zilikuwa na vigezo hivyo. Lakini katika kufanya hivyo, bado Wilaya zinazofanana na zile zilizochukuliwa kwa umaskini ziliachwa na ndiyo maana nikasema tunaenda hatua kwa hatua. Hakuna ubaguzi uliotumika isipokuwa ni kule kuwa chini katika umaskini.

Awamu ya pili nimesema mwanzoni mwa 2005. Sasa kwa sababu haya ni makubaliano kati yetu na Benki ya Dunia, siwezi nikasema tarehe kwanza Januari, lakini mwanzoni kila mtu tunajua kwamba kitu tukikisema mwanzoni mwa mwaka ujao tunaelewa haiwezi kuwa Julai, haiwezi ikawa Mei, itakuwa mwanzoni. *(Kicheko)*

Na. 31

**Sherehe za Muungano**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 12 Januari kila mwaka tunaadhimisha Sikukuu ya Mapinduzi Zanzibar na sherehe hufanyika Zanzibar; na kwa kuwa kila ifikapo tarehe 9 Desemba kila mwaka tunaadhimisha Sherehe ya Uhuru wa Tanzania ambazo hufanyika Tanzania Bara; na kwa kuwa tarehe 26 Aprili kila mwaka tunaadhimisha Sikukuu ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na sherehe huwa zinafanyikia Tanzania Bara siku zote wakati ni Sikukuu ya Kimuungano; na kwa lengo la kuwakumbusha wananchi wa pande zote umuhimu wa Muungano wetu:-

(a) Je, ni mara ngapi Sherehe za Maadhamisho ya Sikuukuu ya Muungano zimewahi kufanyika Kitaifa Zanzibar tangu mwaka 1964 Hadi sasa?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa Sherehe za Muungano pamoja na hizo nyingine zikawa zinafanyika Kitaifa Zanzibar kwa utaratibu utakaoonekana unafaa ili vizazi vya pande zote mbili viweze kujifunza na kuwa na upeo mzuri wa kuujua, kuutetea na kuulinda Muungano wetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa ufafanuzi mdogo kwamba, Sherehe za Muungano kama alivyorekebisha, husherehekewa kila mwaka tarehe 26 Aprili na mwaka huu tutafanya Sherehe hizo huko Zanzibar. Ninashukuru kwa kurekebisha maana alikuwa amesema mwaka 1962 na 1962 tulikuwa hatuna Muungano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, napenda kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sherehe za Muungano ambazo zinafanyika tarehe 26 Aprili kila mwaka zimekuwa zikifanyika mara nyingi zaidi Dar es Salaam ambapo shughuli zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hufanyika. Kumbukumbu zetu zinaonyesha kwamba, sherehe hizi ziliwahi kufanyika Zanzibar katika eneo la Mwanakwerekwe tarehe 26 Aprili, 1984 na zilikuwa ni sherehe za kutimiza miaka 20 ya Mungano, ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Awamu ya Kwanza, Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kuna umuhimu wa Sherehe za Muungano na nyinginezo ziwe zinafanyika Kitaifa Zanzibar kwa utaratibu utakaoonekana unafaa ili vizazi vya pande mbili viweze kujifunza na kuwa na upeo mzuri wa kuujua, kuutetea, kuulinda na kudumisha Muungano wetu. Serikali itaangalia uwezekano wa kuadhimisha sherehe hizi upande wa pili wa Muungano.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wengine huwa hawapati nafasi ya kushiriki kikamilifu katika sherehe hizi Kitaifa na hasa wale wanaoishi vijiji vya ndani huko na ambako hakuna mawasiliano; na kwa kuwa wanapenda na wao kujua nini kinaendelea kuhusiana na Muungano wetu huu; je, ni njia gani muafaka zitatumika juu ya kuelimisha jamii juu ya maendeleo ya Muungano wetu huu?

Pili, je Serikali itakubaliana nami kuwa sasa ni wakati muafaka wa kusherehekea Sherehe hizi za Muungano katika mikoa tofauti ya Tanzania ili wananchi waweze kuhamasika na kujua historia ya Muungano wetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, la kwanza nina hakika Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba, tunapofanya sherehe mahali pale ambapo zinafanyika sherehe za Kitaifa si rahisi kila mwananchi mmoja mmoja kufika sehemu ile. Lakini anachokisema kwamba elimu kwa umma kuhusu nini tunasherehekea, hii tunafanya kupitia vyombo vya habari, kupitia maswali kama hivi ninavyofanya. Kwa hiyo, elimu kwa umma nadhani ni ya msingi na inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwa nini pengine tusifikirie sherehe hizi kufanyika mikoa tofauti ili kuendeleza dhana hii ya elimu kwa umma. Ningependa niseme kwa kuzingatia gharama za sherehe kama hizi, utaangaliwa uwezekano, lakini nina hakika tunajua kwamba sherehe yoyote ile iwe sherehe ya Harusi, iwe Sherehe ya Muungano, kuna gharama zake.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri kabisa. Napenda tu niongezee kidogo kwamba, kwa swali la kwamba watu walio katika maeneo mengine pia waelewe juu ya Muungano, napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba, sherehe hizi zinapofanyika Kitaifa sehemu moja katika mikoa mbalimbali, nao siku hiyo na katika Wilaya wanafanya sherehe za mfano na viongozi mbalimbali wa Serikali katika ngazi mbalimbali wanatoa hotuba kuwaeleza wananchi na kuwakumbusha juu ya mambo muhimu ya Muungano. *(Makofi)*

Juu ya kubadili sehemu ya kufanyia sherehe hizi, pamoja na gharama alizozitaja Mheshimiwa Waziri, pia tunalo tatizo la viwanja. Ni viwanja vichache sana ambavyo vinaweza vikamudu sherehe za aina hiyo. Kwa hiyo, haiwezekani kabisa kwamba tunaweza tukaamua sherehe hizi kwenda katika kila Mkoa. *(Makofi)*

Na. 32

**Fedha Zilizobaki kwenye Mradi wa Songo Songo**

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kwamba fedha zilizobaki kwenye mradi wa kujenga mabomba ya gesi ya Songosongo ni shilingi bilioni 79; na kwa kuwa matumizi ya fedha hizo yametokana na makubaliano kati ya Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania; na kwa kuwa gharama ya kuweka umeme kutoka Songosongo hadi Mikoa ya Lindi na Mtwara ni shilingi bilioni 35 lakini jambo la kusikitisha ni kwamba fedha hizo zitatumika kuziba nyaya Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora:-

(a) Je, kwa mpango huo watu wa Kusini wanawekwa wapi kimaendeleo kwani gesi hiyo inatoka huko Kusini na kitendo hicho kinaleta mshikamano gani baina ya watu wa Kusini na Mikoa ya Kaskazini?

(b) Je, watu wa Mikoa ya Kusini wanakosa gani na hali hiyo itaendelea mpaka lini?

(c) Je, Serikali inaposema Daraja la Mto Rufiji ni ukombozi, tatizo la Kusini ni daraja au miundombinu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Saidi Chubi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa mfumo na mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya Songo Songo itagharimu Sh.208.8 bilioni badala ya Sh. 276.3 bilioni zilizokisiwa awali na hivyo kuweza kunusuru Sh.67.5 bilioni. Bakaa hii inatarajiwa kutumika kwa mpango wa kuimarisha gridi kutokana na uchakavu wa muda mrefu, kuongeza ugavi wa umeme kutokana na vyanzo visivyotegemea maji na kujenga bomba kutoka Salasala kwenda kwenye Kituo cha *IPTL*, Tegeta ili kituo hicho kiweze kutumia gesi mara itakapopatikana Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi na Taifa moja. Serikali haijawahi na wala haina sera ya kuwabagua wananchi wake kwa makundi. Suala la kuchelewa kwa miundombinu katika Mikoa ya Kusini ni la kihistoria na uwezo wa kiuchumi. Wakati Tanganyika inapata uhuru na baadaye kuungana na Zanzibar kuwa Tanzania, waasisi wa Taifa hili waliweka mkakati wa kupambana na ukoloni mkongwe wa Wareno na ubaguzi wa rangi wa Makaburu kama njia pekee ya kumkomboa Mwafrika na hivyo kuihakikishia Tanzania uhuru wake na usalama wake.

Kutokana na sababu za kimkakati na za kiuchumi, isingekuwa rahisi kwa Serikali kushughulikia kwa pamoja suala la ukombozi na la miundombinu, hasa ikizingatiwa

kwamba, mapato yetu hayakuwa makubwa. Ndio maana baada ya kutoweka kwa ukoloni na kuimarika kwa uhuru na uchumi wetu, kumewezesha Serikali kushughulikia kikamilifu maendeleo ya Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kwa kujenga barabara imara, kufikisha umeme na kuufungua ukanda mzima kama ukanda wa maendeleo wa *Mtwara Development Corridor.*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Serikali imesema mara nyingi, wananchi wa Mikoa ya Kusini wametoa mchango mkubwa na wa kipekee katika ukombozi wa Bara la Afrika na kulinda uhuru wetu. *(Makofi)*

Kuomba kutumia fedha zilizobaki kwenye Mradi wa Songo Songo kufikisha umeme Lindi na Mtwara kutahitaji makubaliano mapya na Benki ya Dunia na kutokana na urasimu na masharti magumu ya Benki hiyo, siyo tu kwamba mpango mzima ungechukua muda mrefu. Lakini kwa hakika Wizara ilishawahi kufikisha jambo hili katika Benki ya Dunia na haikuwezekana. Ndio maana Serikali imekaribishauwekezaji wa kampuni ya Artumas katika mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay,* kama njia ya haraka ya kutimiza azma ya kufikisha umeme Mikoa ya Lindi na Mtwara ifikapo mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Artumas tayari imefikia makubaliano ya awali na Serikali Septemba, 2003 na tarehe 24 Machi, 2004 Wawakilishi wa Artumas na Makampuni ya Fedha ya *IDC* ya Afrika Kusini na *FMO* ya Uholanzi, walikutana na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kuieleza Wizara kuwa wamefurahishwa na Mradi wa *Mnazi Bay* na kwamba hatua zote za kuipatia fedha Kampuni ya Artumas zitakamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Daraja la Mkapa lililoko kwenye Mto Rufiji ni ukombozi na ni hatua muhimu katika azma ya Serikali ya kuimarisha miundombinu katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Umeme ni miundombinu nyingine ambayo itakapopatikana kutokana na mipango madhubuti ya Serikali, itakuwa ni hatua nyingine muhimu katika mchakato wa maendeleo na utafungua ukurasa mpya katika maendeleo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kumbe imeshafahamika kwamba kitendo chetu cha kuwasaidia ndugu zetu wa Msumbiji wapate ndicho kilichosababisha tusipate umeme mpaka leo. Sasa je, hivi fadhila hiyo tunaweza tukafadhiliwa hivyo na Serikai hii kwa kufanya mema yaani tunafadhili mambo halafu matokeo yake tunapata adhabu kama hiyo? *(Makofi)*

La pili, siyo jambo la utani ni kwamba kwa mfano kwenye jimbo langu vijana 157 wamepofuka macho kwa ajili ya kusomea kwenye vibatari. Je, ni kweli kulingana na kauli ya Mheshimiwa Waziri, tuendelee kupofuka kama asili yetu vibatali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza si kweli kabisa kwamba, kitendo cha kijasiri kabisa ambacho kimefanywa na wananchi wa

Mikoa ya Kusini wakiungana na wananchi wenzao wa nchi nzima katika kutetea maslahi ya Mwafrika na kulinda uhuru wa nchi hii imekuwa ni kitendo cha adhabu. Ningeomba Waheshimiwa Wabunge tusipotoshe historia ya nchi hii. Kama nilivyosema awali, suala la kupigania uhuru halikuwa ni suala la kuchagua, nchi yetu ilijikuta katika mapambano na Wareno na nchi hizi ambazo zilikuwa na ubaguzi wa rangi na kwa kweli hapakuwa na njia nyingine isipokuwa ni kufuata njia ya kupambana na ukoloni mkongwe ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema awali, Serikali ina mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba tufikapo 2005 na kwa mujibu wa taratibu hizi ambazo ziko hivi sasa nimezielezea, tunatarajia kwamba, Mikoa hii ya Lindi na Mtwara itakuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, si sahihi kwa kweli kusema kwamba, Serikali inawataka wananchi wake waendelee kuwa wanatumia vibatari ili wapofuke macho. Mipango ya Serikali iko imara na mimi nataka nimwombe Mheshimiwa Omari Chubi, kama ambavyo amekuwa akishirikiana na sisi muda wote, aendelee kushirikiana na sisi ili tuhakikishe kwamba, Mikoa hii inapata nishati ya uhakika. *(Makofi)*

Na. 33

**Wachimbaji wa Madini wa Kitanzania**

**MHE. BAHATI ALI ABEID** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ya Tanzania inaonyesha kuwa na madini mengi ikiwemo dhahabu; na kwa kuwa migodi mikubwa imeanzishwa na itaendelea kuanzishwa hapa nchini na wachimbaji au wafanyakazi katika machimbo hayo ni Watanzania; na kwa kuwa wachimbapo madini hayo hupata matatizo mengi ikiwa ni pamoja na vifo:-

(a) Je, wananchi wetu wanaochimba migodini kwa mashine kubwa, wanapata wapi mafunzo na je, wana vyeti maalum vya kutambuliwa Kitaifa na Kimataifa?

(b) Je, wataalam wa afya wanawatembelea ili kujua afya zao na wamepata matokeo gani kama kweli wamewatembelea ikiwa ni pamoja na kinga wanazopewa?

(c) Kwa kutambua kazi ngumu na ya hatari kwa afya na maisha yao, je, mishahara wanayopata inalingana na kazi yao na ni kiasi gani na ni ya Kimataifa/Kitaifa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baadhi ya wafanyakazi wanaoajiriwa migodini, wanakuwa na mafunzo ya msingi kutoka vyuo mbalimbali vya ufundi nchini pamoja na

Vyuo vya *VETA*. Ni dhahiri kwamba, vyeti hivi vinatambuliwa Kitaifa. Mara wanapoajiriwa hupewa mafunzo maalum kulingana na aina ya mashine watakazozifanyia kazi. Baada ya mafunzo hayo, wafanyakazi hao hupimwa *(assessed)* na baada ya kuthibitika kwamba wanaweza kuzifanyia kazi mashine hizo, basi hupatiwa vyeti malum *(Certificate of Competence)* vinavyoonyesha uwezo wao na aina ya mashine wanazoweza kuzifanyia kazi.

Waendeshaji mafunzo hayo *(Trainers),* wana viwango vinavyotambuliwa Kimataifa na watengenezaji mbalimbali wa mashine zitumikazo migodini kama vile *Ceterpiller, Komatsu, Atlas Capco, Sandvik* na *Tamrock.* Muhimu zaidi ni kiwango cha utendaji wao *(Performance)* na tija *(Productivity)* katika mashine hizo ambazo unashindana sawia na wafanyakazi katika migodi mikubwa na ya muda mrefu katika nchi nyingine.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kwamba, wataalam wa afya kutoka katika Wilaya na kutoka katika Taasisi husika, *Institute of Radiation*, Arusha, huwatembelea wafanyakazi wa migodini. Aidha, migodi yenyewe ina vitengo vinavyoshughulikia afya za wafanyakazi *(Occupational Health and Safety),* ambavyo siku hadi siku hufuatilia hali ya mazingira ya kazi na afya za wafanyakazi. Hakuna kinga yoyote wanayopewa mbali ya hatua za lazima migodini dhidi ya ajali na vumbi na masharti mengine kwa mujibu wa sheria.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uzito na mazingira ya kazi mishahara wanayopata ni ya ushindani kwa kulinganisha na migodi na makampuni makubwa mengine nchini, mishahara hiyo sio ya Kimataifa. Kwa hapa nchini ni wastani wa Sh.400,000/= kwa mwezi ukichanganya na malipo ya saa za ziada na marupurupu mengine.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunitambua. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika migodi ambayo imejitokeza, kumetokea ajali mbalimbali ambazo zinatokana na bahati mbaya na zingine zimetokana na makusudi. Je, Serikali kama mhimili mkuu wa shughuli zote zinazofanyika katika migodi hiyo, inahakikisha vipi kuwepo kwa usalama wa mashine na raia kwa kuwapa angalau mafunzo na ulazima wa kuweka Bima ili inapotokea ajali waweze kulipwa fidia wao waliopata ajali pamoja na familia zao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika migodi mbalimbali kuna taratibu za kisheria na za kiutawala ambazo wenye migodi wanatakiwa kufuata katika ufanyaji wao kazi. Wizara inao watu ambao hupenda kupita katika migodi hii na kukagua wakati hadi wakati kama ambavyo Taasisi nyingine hapa nchini zinazohusika na wafanyakazi pia huwa na taratibu za kukagua na endapo ajali inatokea basi taratibu husika hufuatwa na kuhakikisha kwamba, makosa kama hayo ambayo yamesababisha ajali, hayarejewi tena na inategemewa kwa kweli na aina za ajali nyingine uchunguzi huhusisha mpaka vyombo vya dola kama Polisi.

Na. 34

**Mpango wa Kuchangia Huduma za Afya**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA (k.n.y. MHE. DR. LUCY S. NKYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilianza mpango wa kuchangia huduma za afya na kwa kuwa nia na madhumuni ya mpango huo ilikuwa ni kuiwezesha Serikali kuboresha huduma za afya kwa wananchi wote. Je, kama kumekuwepo na mafanikio ni kwa nini kumekuwepo na manung'uniko kutoka kwa wananchi kwamba dawa hazipatikani au hazitoshi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Nkya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali ilianzisha mpango wa kuchangia huduma za afya kwa madhumuni ya kuongeza kipato cha vituo vya kutolea huduma za afya ili kuongeza ubora wa huduma zao kwa manufaa ya wananchi wote.

Aidha, kumekuwepo na mafanikio yaliyoletwa na uchangiaji wa huduma za afya ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Spika, manung'uniko ya wananchi kuwa baadhi ya dawa hazitoshi au hazipatikani ni sahihi kwa sababu zifuatazo:-

(i) Bado kuna pengo kati ya mahitaji halisi ya dawa na dawa zinazotolewa na Serikali hivi sasa. Hii inatokana na hali halisi ya uchumi wetu. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya dawa kila mwaka ili kukabiliana na tatizo hili. Ukilinganisha tatizo la upungufu wa dawa miaka mitano iliyopita na hivi sasa, ni dhahiri kuwa hali ya leo ni nzuri zaidi ya ile ya miaka iliyopita;

(ii) Dawa nyingi zimekuwa zikitolewa kwa makundi yaliyopewa msamaha wa kuchangia hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa fedha zinazopatikana; na

(iii) Udhibiti wa dawa au fedha walizochangia wananchi ili wapate huduma unasimamiwa na Halmashauri husika. Hivyo, Halmashauri ina jukumu la kusimamia na kufuatilia uendeshaji wa mpango wa uchangiaji, kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi, hususan inapothibitika kwamba udhibiti wa mapato ya uchangiaji ni hafifu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mpango huu unatekelezwa ipasavyo, Wizara yangu ilitoa mwongozo wa utekelezaji ambao upo kwenye Halmashauri zote. Kwa kuwa mwongozo huo uko wazi, basi yanapotokea mapungufu na

udhaifu wa kiutendaji, ushirikiano na wadau mbalimbali zikiwemo Bodi za Afya za Halmashauri na Mamlaka nyingine zina wajibu wa kufikia maamuzi sahihi ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa fedha zinazokusanywa kwa kuchangia gharama katika huduma za afya zimekuwa zikitumika katika matumizi mbalimbali wengine hukarabati majengo, wengine kununua dawa na wengine hukaa nazo bila kuzitumia, je, Wizara ina uhakika mwongozo ilioutoa unatumika kama ilivyoutoa?

(b) Kwa kuwa Serikali wakati fulani ilifuta ada ya kuingia katika Hospitali kama kuondoa kero na kwa kuwa hivi karibuni Hospitali moja ya Rufaa imerejesha ada inayofanana na hiyo, je, ada hiyo inatofautiana vipi na ada iliyofutwa na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya fedha za uchangiaji, ni kweli Wizara imetoa mwongozo na mwongozo huo upo katika Wilaya zote na ni wajibu wa Halmashauri husika na Bodi za Afya za Halmashauri kuhakikisha kwamba, matumizi ya fedha hizo yanatumika kama mwongozo unavyosema. Aidha, uchangiaji una maeneo zaidi ya moja, kuna ule uchangiaji wa madawa peke yake ambao tunaita *Drug Revolving Fund,* kwa maana kwamba, fedha zinazokusanywa kutokana na mauzo ya dawa zinatakiwa zirudi kuongezea dawa ili kupunguza upungufu na zile zinazokusanywa kwa *Cost Sharing* za upande mwingine zinatakiwa kushughulikia upungufu wa vifaa na ukarabati mdogo mdogo na kadhalika. Kwa hiyo, wajibu wa kuangalia matumizi ya mwongozo bado ni jukumu la Halmashauri ya Wilaya na Bodi za Afya za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ada ya kuingilia katika Hospitali anayoizungumzia Mheshimiwa Diodorus Kamala, napenda niseme kwamba, wakati ada zile zikifutwa na Hazina katika Bunge hili, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, endapo kuna taasisi yoyote itahitaji kutoza ada hizo basi inatakiwa ipate kibali kutoka Hazina, hakusema kwamba hawaruhusiwi mia kwa mia. Kwa hiyo, ninachotaka kumfahamisha Mheshimiwa Diodorus Kamala ni kwamba, Hospitali ya Taifa Muhimbili imeomba kibali hicho ili iweze kuruhusiwa kuendelea kutoza ada hiyo.

Na. 35

**Mtaalam wa Matibabu ya Viungo Wizarani**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini hakuna Mtaalam wa Matibabu ya Viungo *(Physiotherapist)* Mwakilishi katika Wizara ya Afya na Serikali ina mpango gani wa kupeleka Mtaalam wa aina hiyo kwenye ngazi ya Wizara?

(b) Je, kuna Wataalam wangapi wa fani hiyo wanaofanya kazi Serikalini hadi sasa na ni wangapi kati ya hao wameacha kazi Serikalini kwa kipindi cha miaka kumi hadi sasa na ni sababu zipi ziliwafanya waache kazi?

(c) Kwa kuwa Wataalam wa fani hiyo ni wachache na hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu sana, je, Serikali inao mpango gani wa kuwapandisha vyeo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa hakuna Mtaalam wa Mazoezi ya Viungo *(Physiotherapist)* katika ngazi ya Wizara kama mratibu wa taaluma hiyo. Kazi za *Physiotherapist* ni aina ya tiba hivyo uratibu wake unasimamiwa na Mkurugenzi wa Huduma za Hospitali Wizarani. Kuna Kada nyingine kadhaa ambazo hazina uwakilishi Wizarani na hali hii haiondoi umuhimu wake.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2003 kulikuwa na wataalam wapatao 32 katika vituo na hospitali za umma. Wizara yangu haina takwimu za uhakika ni watumishi wangapi wa kada hii wameacha kazi Serikalini kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita na hivyo kuwa vigumu kujua sababu zilizofanya waache kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, wataalam hawa wazoeza viungo ni wachache. Wizara yangu imekuwa ikifanya zoezi la kupandisha vyeo watumishi wa Sekta ya Afya wakiwemo wazoeza viungo *(Physiotherapist)*.

Hivi sasa zoezi la kukamilisha kupandishwa vyeo wazoeza viungo 12 linaendelea na baada ya muda si mrefu watumishi hawa watakuwa wamepandishwa vyeo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Kitengo hiki cha Tiba ya Viungo hakina Mwakilishi Wizarani na kwa kuwa Kitengo hiki sasa kina wateja wengi, je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba sasa kuna haja Kitengo hiki cha Tiba ya Viungo kuwa na Mwakilishi Wizarani ili aweze kusimamia zoezi zima kwa nchi nzima?

(b) Kwa kuwa wagonjwa wenye matatizo ya viungo sasa ni wengi nchini, je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuwa na wataalam hawa kwenye Hospitali zote za Wilaya nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema si taaluma zote zenye Wawakilishi Wizarani lakini wazo analolitoa Mheshimiwa Mbunge

ni zuri na nataka nimhakikishie kwamba, tutalifanyia kazi ili tuone uwezekano wa kupata Mwakilishi huyo ndani ya Wizara ili kuratibu shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwa na wataalam hawa Wazoeza Viungo Wilayani, ni jambo zuri lakini tatizo tulilokuwa nalo kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, idadi yao bado ni ndogo kukidhi mahitaji ya Wilaya zote tulizokuwa nazo. Kwa hiyo, tunachoweza kusema ni kwamba, tutaendelea kutoa mafunzo kwa taaluma hii ili idadi yao itakapokuwa kubwa zaidi tuweze kuwafikisha katika ngazi ya Wilaya.

Na. 36

**Benki Kuwekeza katika Dhamana za Serikali**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Benki hapa nchini hupendelea zaidi kuwekeza katika amana za Serikali badala ya kuwekeza katika sekta za kilimo, uvuvi, viwanda, madini na biashara, ili kuongeza uzalishaji na kuboresha huduma wanazotoa:-

(a) Je, Serikali inalifahamu hilo na kama inalifahamu, inachukua hatua gani?

(b) Kama kweli hali hiyo itazidi kuendelea, kama ilivyo sasa, je, wananchi watapata wapi mitaji ya kuwekeza katika sekta mbalimbali hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, katika kipindi kilichopita kiasi cha uwekezaji katika dhamana za Serikali kilikuwa kikubwa kuliko kiasi cha mikopo kwa sekta binafsi. Kwa mfano, mwishoni mwa mwaka 1995, Mabenki yalikuwa yameweka shilingi 181.1 bilioni katika dhamana za Serikali ikilinganishwa ana shilingi 163.5 bilioni zilizokuwa zimetolewa kama mikopo kwa sekta binafsi. Hali hii ilitokana na kuwepo kwa matatizo yaliyokuwa yakikwamisha utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi *(Structural and Institutional Impediments).* Kutokana na hali hiyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kurekebisha uchumi pamoja na kuboresha mazingira ya utoaji mikopo ambazo ni pamoja na:-

Kuendelea kurekebisha asasi za fedha, kuanzisha Mahakama ya Biashara ili kupunguza mlundikano na urasimu wa uendeshaji kesi za biashara, kurekebisha sheria mbalimbali ili kuwezesha uanzishaji wa asasi za fedha kwa ajili ya mikopo midogo midogo ambazo zimeongeza ushindani katika kutoa mikopo kwa wananchi, kupunguza kukopa kwa ajili ya Bajeti ya Serikali na kwa hivi sasa Serikali haikopi mikopo mipya isipokuwa inakopa kulipia dhamana za Serikali zinazoiva na kuanzisha Mfuko wa

kudhamini mikopo kwa wakopaji wanaozalisha bidhaa zinazouzwa nje ya nchi *(Export Credit Guarantee Scheme).*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa, mikopo kwa sekta binafsi imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Kwa mfano, takwimu zinaonyesha kwamba, mikopo kwa sekta binafsi imeongezeka zaidi ya maradufu (asilimia 153.4) kutoka shilingi 333.3 bilioni Desemba, 2000 hadi kufikia shilingi 884.6 bilioni  Februari, 2004, wakati uwekezaji katika dhamana za Serikali ulishuka kutoka shilingi 403.8 bilioni hadi shilingi 365.5 bilioni katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matokeo mazuri ya juhudi za Serikali, utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi bado haujafikia kiwango cha kuridhisha. Kutokana na hali hii, hivi sasa Serikali inachukua hatua mbalimbali ili kuongeza utoaji mikopo kwa sekta binafsi, hatua hizo ni pamoja na kupitishwa kwa marekebisho ya Sheria ya Ardhi ili kuwezesha matumizi ya ardhi kama dhamana kwa mikopo, kuwezesha kuanzishwa kwa asasi za kutoa taarifa za ubora wa wakopaji *(Credit Reference Bureaus),* kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuanzisha asasi za kutoa mikopo midogo midogo kama vile Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa na Benki za Wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi ambazo Serikali inaendelea kuzifanya, mikopo kwa sekta binafsi  itaendelea kuongezeka katika miaka ijayo na hivyo kuwezesha wananchi wengi zaidi kupata mikopo ya kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mazingira ya shughuli za Kibenki hivi sasa ni ya kibiashara na kwa vile Serikali imetoa unafuu kwenye masharti ya uanzishaji na uendeshaji wa Benki za Wananchi, Serikali inawaomba Waheshimiwa Wabunge, kusaidia kuhamasisha wananchi kutumia fursa hiyo kuanzisha vyombo vyao vya fedha badala ya kutegemea Mabenki ya kawaida ya Biashara, ambayo yana masharti mengi na magumu. Kwa kuzingatia haya, wananchi wanaweza kuanzisha vyombo vyao wenyewe vya kuweka na kukopa kwa urahisi zaidi. Aidha, Serikali inawaomba Waheshimiwa Wabunge, kuendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kutumia vyema mikopo na kujenga tabia ya kulipa kwa wakati ili kuwezesha upatikanaji zaidi wa mikopo na kuimarisha sekta ya fedha nchini.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema mikopo imeongezeka lakini hii ni katika sehemu za miji mikubwa na kwa hiyo kuleta tofauti kati ya watu wanaoishi vijijini kama kule Kyerwa au Kisiwa cha Ukara.  Je, sasa Serikali ina utaratibu gani wa ama kuleta sheria hapa kama walivyofanya kwa Vyama vya Ushirika kuhakikisha kwamba Benki za Wananchi zinaanzishwa vijijini na kuzisimamia na kuhakikisha kwamba utaratibu mzima unakwenda kwa haraka, Serikali inalionaje hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeboresha sana masharti ya uanzishwaji wa Benki sehemu zote nchini mijini na vijijini. Napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kuanzisha Benki katika miji midogo ikiwemo Kata na Vijiji, kiwango cha chini kabisa ni shilingi milioni 50 hata Mheshimiwa Mutungirehi anaweza akakopa Benki na akaanzisha Benki kwenye Kata yake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika miji ya kati kiwango cha chini ni shilingi milioni 100, katika Manispaa ikiwa ni pamoja na Jiji na Miji mikubwa ni shilingi milioni 200 unaanzisha *Community Bank, Non Bank Financial Institutions* ambazo hazishughuliki na mambo ya *Cheque* kiwango cha chini ni shilingi milioni 500 na mtaji kwa Benki mpya kwa maana inafanya shughuli zote za Kibenki kiwango cha chini ni shilingi bilioni 5.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kutumia fursa hii kuwahamasisha na kuwaomba wananchi popote pale walipo, wafanyabiashara, *NGOs,* pamoja na madhehebu ya dini watumie fursa hii ya masharti yaliyoboreshwa ili huduma hizi za kifedha ziweze kuenea kote nchini.

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Katika Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema kwamba zilitengwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kwa kuwapa mitaji katika biashara ndogo ndogo katika sekta ya kilimo, uvuvi, viwanda, madini na biashara, je, hadi leo ni kiasi gani kati ya fedha hizo kimetolewa kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, katika Bajeti iliyopita shilingi milioni 500 zilitengwa kwa ajili ya ku-*guarantee* mikopo kwa ajili ya wafanyabiashara na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika sekta mbalimbali. Kwa sababu kilikuwa ni kitu kipya tunaanzisha, ilibidi kwanza kuweka utaratibu mzuri na muafaka kwa ajili ya shughuli hiyo. Waliopewa jukumu hili ni Benki Kuu pamoja na *SIDO*. Kwa hiyo, utaratibu kwa ajili ya kuanza kutoa mikopo hiyo unafikia hatua za mwisho na itatangazwa hivi karibuni kwamba, mikopo itaanza kutolewa kwa utaratibu gani. Lakini tumepata mafanikio makubwa sana katika *Export Guarantee Scheme* ambapo wote waliokopa chini ya utaratibu huu ambapo zilikuwa zimetolewa shilingi bilioni 6.5, wote walirudisha na walirudisha kwa wakati na ndio maana kiwango kikaongezwa mara dufu

Na. 37

**Madai ya Wafanyakazi waliokuwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyakazi wengi waliokuwa wakifanya kazi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, kabla ya kuvunjwa hawajalipwa haki zao, hasa ikilinganishwa na wenzao wa Kenya na Uganda; na kwa kuwa tatizo hilo limekuwa sugu na kero kubwa katika Majimbo yetu mengi:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya madai hayo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kulimaliza kabisa tatizo hilo kwa kutoa taarifa nchi nzima ili walengwa waelewe hatma yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Juni, 1999 Serikali ilitangaza kukubali kuwalipa mafao yao yote wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokana na kuitumikia Jumuiya hiyo. Hivyo, ili kuweza kufahamu madai halisi ya wastaafu hao, Serikali iliunda Tume ambayo ilipewa jukumu la kuchambua na kuyaweka mafao hayo kama ambavyo yangelipwa kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya hiyo. Kwa msingi huo, Tume hiyo ilifanya kazi ya kutafsiri viwango cha malipo kwa kuangalia vigezo vya makubaliano ya Mkataba wa Upatanishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kutokana na mapendekezo na ushauri wa Tume, tarehe 30 Novemba, 1999, Serikali ilianza kuwalipa wastaafu hao kwa kuzingatia kumbukumbu za utumishi za kila mstaafu kwa lengo la kila mhusika kupata stahili yake kulingana na kumbukumbu hizo.

Mheshimiwa Spika, wakati malipo hayo yalipokuwa yakiendelea, mwezi April, 2000, Serikali ilipokea barua ya wastaafu hao kupitia kwa Wakili wao ikionyesha kusudio la kuishtaki Serikali katika shauri hili. Baada ya hapo kesi zifuatazo zilifunguliwa: Kesi Na.13 ya mwaka 2000 iliyofunguliwa katika Mahakama Kuu ya Arusha dhidi ya Afisa Mapato wa Mkoa na wengine na kesi ya Madai Na.95 ya mwaka 2003 iliyofunguliwa Mahakama Kuu Dar es Salaam dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kesi hizo bado hazijatolewa hukumu, naliomba Bunge lako Tukufu livute subira hadi uamuzi wa Mahakama utakapotolewa. Baada ya hapo, Serikali itaweza kulisemea tena suala hili.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wafanyakazi wa Jumuiya hii walioko upande wa Uganda na Kenya walilipwa mafao yao mapema kabisa, ningependa kujua ni sababu zipi zilizosababisha Serikali yetu ya Tanzania isiwalipe wafanyakazi hawa mpaka tarehe 2 Juni, 1999?

(b) Kwa kuwa madeni, mali na stahili zote za wafanyakazi zimefafanuliwa vizuri sana katika ripoti ya Dr. Umbritch, je, Serikali itakuwa tayari kuiweka ripoti hiyo wazi ili sisi sote tuweze kujua ni kitu gani wafanyakazi hao walistahili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, walishaanza kulipwa na kutokana na sababu walizokuwa nazo ndio maana wakafungua kesi Mahakamani. Uganda na Kenya hawakuwa na matatizo walilipwa na sisi pia hatukuwa na matatizo kwa sababu taratibu zote zilikamilika na wakaanza kulipwa. Kwa hiyo, madai yao yako Mahakamani na kama kuna haki zao zitazungumzwa Mahakamani na zitatolewa na Serikali itatekeleza mara hukumu itakapotolewa.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Dr. Umbritch kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ipo na wala sio siri, kama ataihitaji ataweza kupatiwa.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu suala hili la mafao ya wastaafu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali haiwezi kukubaliana nasi kwamba kutolipa mafao hayo kwa muda mrefu kumewakosesha haki wafanyakazi hao kwa sababu malipo yaliyofanywa kwa kipindi cha mwaka 1999 mpaka 2000 yalikuwa hayatilii maanani juu ya muda uliopita, fedha ilivyopoteza thamani wakalipwa kwa kiwango cha mwaka 1977?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, iliundwa Tume kufuatilia suala hili na Tume hii haikuwa ni Idara moja ya Serikali wala mtu mmoja, ilikuwa ni Tume kwa hiyo iliangalia masuala yote yaliyohusika pamoja na hayo anayosema Mheshimiwa Mbunge. Tume ilitumia taarifa mbalimbali na kumbukumbu na Mikataba mbalimbali iliyokuwepo ya wafanyakazi wa ngazi mbalimbali. Kwa hiyo, kwa sababu suala hili bado liko Mahakamani, napenda kusisitiza kwamba, tuachie Mahakama imalize kazi yake na itakapomaliza kazi yake Serikali itachukua hatua zinazostahili.

Na. 38

**Mapato Yatokanayo na Michezo ya Kubahatisha**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa ndani ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Act, 2002)* kuna maelezo kuwa asilimia fulani ya mapato kutokana na michezo hiyo itatumika kuendeleza michezo ya aina mbalimbali nchini ikiwemo ile ya watu wenye ulemavu:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa kwa ajili ya michezo tangu mwaka 2002 mpaka siku ya swali hili kujibiwa?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kila mchezo kimepewa kutokana na mapato hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ni ya mwaka 2003 na ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2003. Kwa mujibu wa Kifungu 34(1) cha Sheria hiyo, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha itatenga nusu ya fedha kutoka katika tozo la kodi ya asilimia 10 ya bei ya kila tiketi ya Bahati Nasibu itakayokusanywa kutoka katika uendeshaji wa michezo ya Bahati Nasibu ya Kitaifa ili fedha hiyo isaidie kuendeleza na kudhamini michezo Tanzania Bara. Aidha, fedha hizo zitatolewa kwa Baraza la Michezo la Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna fedha zilizokusanywa kutokana na chanzo hiki kwa kuwa Bodi ilikuwa haijateua wala kutoa leseni kwa kampuni yoyote ya michezo ya kubahatisha. Hii ni kwa sababu uteuzi na utoaji wa leseni ya Bahati Nasibu (Kitaifa) inategemea maelekezo yaliyomo katika Kanuni za Michezo ya Kubahatisha ya mwaka 2003 *(Gaming Regulations, 2003),* hivyo, ililazimu kuzichapisha kwanza na kuziingiza kabla ya kuanza kutoa leseni. Kanuni hizo zilichapishwa Novemba, 2003 na kutolewa Desemba, 2003 na hivyo Bodi ikaanza kupokea maombi kutoka kwa Wazabuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua maombi hayo, kwa mujibu wa Kifungu 41(1) cha *Gaming Act, 2003* na Kanuni ya 86(2) ya *Gaming Regulations, 2003*, tarehe 8 Aprili, 2004, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha iliiteua Kampuni ya *Gaming Management Tanzania Limited (GAMAT)* ya Dar es Salaam kupewa leseni ya kuendesha biashara ya Michezo ya Bahati Nasibu Kitaifa nchini. Kampuni imepewa muda wa miezi mitano kujiandaa kwa kuweka mitambo, kuajiri na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kuteua mawakala wa Mikoa. Hivyo, inatarajiwa kuwa michezo hiyo itazinduliwa rasmi ifikapo Septemba, 2004 na hapo ndipo mapato yatokanayo na michezo hiyo yataanza kukusanywa.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika michezo hii ya kubahatisha mara nyingi imeonekana kwamba, wale wanaoichezesha wanafanya ujanja mkubwa ili kupata zaidi kuliko wale wanaocheza na mara nyingine vile vile imeonekana jambo hili linahusu jamii hasa inapotokea kwamba baadhi ya wale wanaokwenda kucheza wakiliwa sana wanaweka dhamana nyumba hata mara nyingine kuweka wake zao dhamana, je, Serikali inaweza ikaingilia jambo hili ili michezo hii iwe halali? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, mchezo huu au michezo ya kubahatisha imetungiwa sheria na sheria hii ilitungwa na Bunge lako Tukufu na pia kuna *Gaming Regulations* ambayo imetungwa mwaka 2003 na hizi ndio zinalinda taratibu na mchezo mzima wa kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, mchezaji halazimishwi kwenda kucheza Bahati Nasibu, inakuwa juu yake. Lakini pia kuna aina nyingi za Bahati Nasibu unaweza kuchagua ipi ambayo unaona kwamba haikupi *risk* kubwa kwa mfano, kuna *scratch* za papo kwa papo ambazo huyu amepewa, huyu wa kwanza amepewa aina mbili tu na kuna aina nyingine zaidi kama tatu ambazo wafanyabiashara wengine ambao wanapenda kuchukua leseni, bado wanakaribishwa kufanya hivyo. Kwa hiyo, mchezaji anapocheza anacheza *at his own risk.*

Na. 39

**Ujenzi wa Shule Binafsi Nchini**

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa Taifa letu limezinduka na kutambua umuhimu wa elimu kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa kutambua hivyo wananchi kwa maana ya watu binafsi na jamii mbalimbali hapa nchini wamefikia kiwango cha uhamasishaji kinachowaongoza kushiriki katika jitihada hizo kwa kujenga shule binafsi. Je, ni vigezo na masharti gani yanayotumika kwa shule binafsi au ya umma kukubalika na kupitishwa na Serikali kuwa Shule ya Sekondari?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Taifa letu sasa limezinduka na kuona umuhimu wa elimu kwa maendeleo ya nchi yetu na hivyo hata watu binafsi na jamii mbalimbali kuanzisha Shule za Sekondari katika Mikoa na Wilaya mbalimbali. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, inaruhusiwa kuanzisha Shule za Serikali na zisizo za Serikali. Katika kuanzisha shule hizo, Serikali inasisitiza kwamba, hakuna shule itakayoruhusiwa kuanzishwa bila kibali cha maandishi kinachotolewa na Afisa Elimu Kiongozi, kwa mujibu wa Kifungu Na.14 cha Sheria ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, ili shule ya Sekondari iweze kupata kibali cha kuanza au kusajiliwa, pamoja na kuwa na Walimu wa kutosha wenye sifa kitaaluma na kitaalam, wenye shule hawana budi kutimiza Masharti ya Msingi yafuatayo: Wawe na majengo ya kutosha yakiwemo jengo la utawala, vyumba vya madarasa kulingana na ukubwa wa shule, maabara mbili, nyumba za Walimu zisizopungua nane, maktaba moja, vyoo matundu mawili kwa wafanyakazi na vyoo vya wanafunzi kwa uwiano wa wasichana 25 tundu moja na wavulana 30 tundu moja, jengo la jiko, bwalo na ukumbi.

Vile vile wawe na samani za kutosha yakiwemo madawati na viti kulingana na idadi ya wanafunzi, meza za darasani na viti vyake, makabati ya vitabu na vifaa vingine, meza na viti vya Ofisi za Walimu na kasiki (Kasha la kuhifadhia fedha) moja. Pia vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vitabu vya kiada na ziada, muhtasari wa kila somo na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia vya kutosha. Aidha, ziwepo Huduma muhimu za maji, tiba, sanduku la barua na barabara ya kufika shuleni.

Mheshimiwa Spika, shule zikikamilisha masharti hayo na kukaguliwa, Afisa Elimu Kiongozi, hutoa kibali cha kuanza au kusajili shule hiyo. Aidha, napenda kutumia nafasi hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Wilaya na Mikoa mbalimbali na wananchi kwa ujumla, waendelee kuhamasisha ujenzi wa shule hizi zisizo za Serikali ili ziendelee kuchangia katika maendeleo ya elimu hapa nchini.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu haya yaliyo fasaha sana ya Mheshimiwa Waziri, nashawishika kuuliza ifuatavyo:-

Nimepata kuona mahali katika eneo la karibu kilomita kumi kutoka Morogoro pana shule ambayo ilikuwa inaitwa *Pangawe Academic* na watoto walikuwa wameanza kuruhusiwa kwenda kwa wakati ule nilipokwenda. Vigezo hivi vyote sioni kama ile shule ilikuwa navyo kwa sababu hapakuwa na majengo ya kutosha, vyoo havikuwepo, lakini nasema ni shule mbovu, kama ni shule kweli mazingira yake ni mabovu sana. Sasa

iliwezaje kupata nafasi hii ya kuweza kutoa *admission* kwa wanafunzi kwa kupitishwa kwa vigezo hivi, hivi kweli? Hilo moja.

Kama kweli shule hiyo nilivyoiona mimi ndivyo ilivyokuwa na imeendelea kuwa hivyo, nataka kujua hivi baada ya pale nilipoiona mimi shule hii bado ipo mpaka leo na kama ipo inamilikiwa na nani?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naona sasa swali limebadilika kidogo limelenga shule moja maalum. Jibu langu lilikuwa kwa ujumla, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, tupeane vizuri jina la shule hiyo, Wizara inao mtandao mzuri sana wa Wakaguzi, tuna Wakaguzi wa Kanda na Kanda hii ya Kati Makao Makuu ni hapa hapa Dodoma na tuna Wakaguzi wa ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, akinipa jina la shule hiyo vizuri, naweza haraka sana nikaagiza Wakaguzi waende kuiangalia na nitaweza kumpa majibu yaliyo sahihi. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru na Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi katika ujumla wao wamehamasika na ni shule nyingi za jamii ndiyo zinazojengwa sasa hivi na kwa kuwa walimu wanatolewa na Serikali na kwa bahati mbaya idadi ya walimu ni ndogo na shule zilizojengwa hazina walimu. Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti na wa makusudi kuhakikisha kwamba shule hizo zilizojengwa zinapata walimu wa kutosha ili wananchi waliozijenga wasikatishwe tamaa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba, spidi ya wananchi kujenga na kuanzisha sekondari hizi zisizo za Serikali hasa zile ambazo zinajengwa na wananchi ili ziendeshwe na Serikali, imekuwa ni kubwa kupita spidi tuliyokuwa nayo ya kuandaa walimu na sasa hivi ni jambo la kawaida. Nasikitika kusema kwamba, ni jambo la kawaida, kufika kwenye sekondari karibu kila sekondari katika Wilaya na Mikoa mbalimbali na kukuta kuna upungufu wa walimu. Lakini napenda kusema kwamba, Serikali inalifahamu jambo hili na kikao kilichopita cha Bunge hili, tuliomba *supplementary* na kulikuwa na maombi maalum yaliyoombwa na Bunge hili na Bunge hili likaidhinisha ili tuweze kufanya mkakati maalum wa kuwapata walimu.

Nilitoa maelezo hapa kwamba, tutajaribu kuwapata walimu wenye *degree* hata kama siyo za ualimu na vijana waliofaulu vizuri ambao wamemaliza kidato cha sita kwa kufaulu vizuri mitihani ya kidato cha nne na cha sita, hawa tutawachukua kwa kutumia fedha zile tulizopewa na Bunge, tutawapa *crash programme* kujifunza pedagojia ya elimu yaani namna ya kufundisha na tumeandaa mafunzo hayo ya muda wa mwezi mmoja. Tangu kikao kile cha Bunge tulivyopata fedha, walioangalia katika magazeti tumekwishatangaza wanaohitaji nafasi hizo na maombi tumeanza kuyapokea na ni matumaini yangu kwamba, baada ya muda mchache tukimaliza hayo mafunzo, tutafuta kabisa suala la mapengo ya walimu katika sekondari zetu.

Na. 40

**Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Kujenga Sekondari**

**MHE. PHILLIP S. MARMO (k.n.y. MHE. PARSEKO V. KONE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu alipotembelea Wilaya ya Simanjiro aliahidi kwamba Serikali itajenga sekondari moja ya bweni katika Wilaya zenye wafugaji yaani Wilaya ya Simanjiro, Monduli, Kiteto na Ngorongoro. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa katika Wilaya ya Simanjiro?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parseko Vincent Kone, Mbunge wa Simanjiro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, alitembelea Wilaya za Simanjiro, Ngorongoro, Karatu, Monduli na Kiteto kuanzia tarehe 10 hadi 17 Julai, 1998 na akaahidi kuwa, Serikali katika kuimarisha mfumo mzima wa elimu, itazingatia shule za bweni zijengwe katika Wilaya za Wafugaji ili wanafunzi wasiwe wanaathirika kutokana na kuhamahama kwa wazazi wao. Serikali kupitia Wizara yangu, imezingatia ahadi hiyo katika kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004 - 2009, ambao uandaaji wake umekamilika mwaka huu. Moja ya miradi katika mpango huo ni kujenga shule mpya za sekondari 1,200 katika maeneo yaliyo nyuma katika kupatiwa elimu ya sekondari *(Underserved Areas)* ikilinganishwa na maeneo mengine nchini. Wilaya ya Simanjiro ni moja ya maeneo hayo kutakakojengwa shule za sekondari mpya kwa utaratibu maalum wa ruzuku ya maendeleo itakayotolewa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya shule pamoja na majengo maalum ya kulala wanafunzi (hosteli) yatakayoendeshwa na wananchi wenyewe. Lengo maalum la mpango huo ni kuongeza nafasi za elimu ya sekondari kutosheleza asilimia hamsini ya wanafunzi wanaohitimu darasa la VII ifikapo 2010. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kutoa wito kwa Wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Simanjiro, kuandaa mipango yao ya Kiwilaya ya kufikia lengo hilo.

**MHE. PHILLIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza.

(i) Nampongeza Waziri kwa mpango huo alioutaja lakini wasiwasi wetu ni kwamba utafanikiwa, hizo shule za bweni watakaosoma ni wanafunzi wa Wilaya kama hizo za Simanjiro kwa vile mpaka sasa tunapoongea mpango wa elimu ya msingi kwa Wilaya kama Simanjiro umeshindikana kwa sababu fedha zinazotolewa ni kwa ajili ya asilimia sitini na mbili tu ya watoto wote ambao wanastahili kuingia shuleni, watoto zaidi ya asilimia 38 wapo majumbani?

(ii) Bila shaka Waziri na wahusika Wizarani wanafahamu kwamba toka dunia hii iundwe watu wanaoitwa Wahadzabe hawana mtu hata mmoja ambaye amepata *degree* hadi leo na waliofanikiwa kupata elimu ya kidato cha sita hadi leo hawafiki hata watano. Sasa kwa ajili ya uungwana wetu na ustaarabu wetu sisi Watanzania, Waziri na Wizara yake, atawaambia nini Watanzania ili tuachane na fedheha hii katika mpango huu wa elimu ya msingi na sekondari kwa watu kama hawa ambao wamesahauliwa kwa miaka hii yote? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, napenda nikubaliane naye kwamba, kama ipo kweli kasoro hiyo ya kibajeti, shule zile za msingi bajeti inayotolewa ni asilimia sitini na mbili aliyoitaja. Nitapenda tuliangalie suala hilo kwa sababu lengo la shule hizo ni kwamba, zipewe fedha za kutosha ili watoto wa ndugu zetu wafugaji wanaosoma katika shule hizo waweze kusoma kwa ukamilifu unaohitajika. Lakini napenda nichukue nafasi hii pia niombe viongozi wa maeneo hayo tusaidiane.

Nilipotembelea baadhi ya shule hizo zilikuwa zinapokea wanafunzi wengi zaidi kutoka maeneo na makundi yasiyolengwa kuliko kutoka makundi lengwa. Jambo hili linaweza kusimamiwa vizuri zaidi ngazi ya Wilaya na Mkoa kuliko sisi tulioko Dar es Salaam, naomba hilo nalo tulisahihishe.

Mheshimiwa Spika, la pili, ametueleza hapa kwamba, ndugu zetu Wahadzabe, hakuna hata mtu mmoja mwenye *degree* ya Chuo Kikuu. Mimi ninachoweza kusema nafurahi sana kwamba leo sauti ya Wahadzabe imesemwa humu Bungeni, kwa sababu Mheshimiwa Marmo ndiyo Mbunge wao na ametamka jambo hili hapa Bungeni, mimi nadhani ni mfano mzuri kwamba Mheshimiwa Mbunge yeyote aliye na makundi maalum, ambayo sera zetu za elimu kwa wote bado hazijawafikia, ni vizuri sauti zikasikika humu Bungeni ili Serikali tushirikiane na Wabunge hao husika tuhakikishe suala hili la elimu kwa wote kweli tunalitekeleza ipasavyo. Kwa hiyo, naomba tushirikiane, tulifuatilie jambo hili na tutafute namna ya kufanya angalau Wahadzabe wachache nao waweze kupata nafasi ya kwenda shuleni. Lakini nimalizie kwa kusema kwamba, suala hilo lipo katika maeneo mengi, siku moja Mheshimiwa Makwetta aliniambia kwamba Kijijini kwao kule Muhaji wa kwanza kupata *degree* ni yeye Mheshimiwa Makwetta na wa pili ni mtoto wake Mheshimiwa Makwetta. Sasa *gaps* za namna hizo hazifai, ni afadhali tupanue kwa ujumla. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 41

**Utunzaji wa Mazao ya Biashara**

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa mashamba yote ya Zao la Katani hapa nchini yana magugu mengi na makubwa kuliko hata katani yenyewe ambayo yanaifanya katani kudumaa na kukosa ubora wake na kwa kuwa vile vile kwa upande wa zao la kahawa na michungwa pia imedumaa na kufanya kahawa kutoa matunda yaliyodhoofu kama shanga na machungwa

kutoa machungwa madogo kama ndulele kutokana na kukosekana kwa Maafisa Ugani *(Extension Officers)* ambao wangewatembelea wakulima wa mazao hayo na kutoa elimu kinadharia na kivitendo na maelekezo ya kitaalam ya kuyahudumia mazao hayo, jambo linaloikosesha Serikali yetu fedha nyingi za kigeni:-

(a) Je, kuna Daftari kwa Afisa Kilimo wa Mkoa, Wilaya, Tarafa na Kata linaloonyesha siku, tarehe, jina la mkulima aliyefundishwa utunzaji wa shamba lake kwa mwezi na kwa mwaka?

(b) Je, Serikali iko tayari kuwasimamisha kazi au kama imeshawasimamisha kazi Maafisa Kilimo wa ngazi yoyote ambao madaftari yao hayaonyeshi idadi ya wakulima (angalau 100) waliopatiwa mafunzo juu ya kutunza mashamba yao na kama haijafanya hivyo inangoja nini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Meja Mstaafu, Mheshimiwa Jesse J. Makundi, Mbunge wa Vunjo, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kuota kwa magugu kwenye mashamba ya katani na kudumaa kwa kahawa na michungwa hakukutokana na Maafisa Kilimo kutokuwatembelea wakulima na kuwapa mafunzo bali kunatokana na sababu maalum zinazohusu kila zao. Kwa mfano, mashamba mengi ya mkonge yametelekezwa kwa miaka mingi bila matunzo, jambo ambalo limesababisha baadhi ya mashamba hayo kuwa machakavu.

Kwa upande wa kahawa, baadhi ya wakulima wameacha kutunza mashamba yao kwa visingizio mbalimbali. Kwa upande wa machungwa, sina hakika Mheshimiwa Meja Makundi anazungumzia michungwa ya wapi. Michungwa ninayoijua mimi inazaa machungwa yenye sifa nzuri za ukubwa na ladha.

Mheshimwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse J. Makundi, lenye sehemu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wataalam wa kilimo hawana madaftari maalum ya kuonyesha orodha ya majina ya wakulima wanaowahudumia siku kwa siku katika ngazi za Mkoa, Wilaya, Tarafa na Kata. Hata hivyo, wataalam wote wa ugani wanatakiwa wawe na ratiba za kazi zinazosimamiwa na Halmashauri za Wilaya na Miji husika na wataalam wote wanatakiwa kutoa taarifa za kila mwezi kwa Viongozi wa Halmsahuri zao. Taarifa hizo zikiandaliwa vizuri zitaonyesha kazi zilizofanywa na Afisa anayehusika na mafanikio na matatizo waliyopata katika utendaji wake wa kazi kwa mwezi unaohusika. Viongozi wanaopelekewa taarifa hizo wanapaswa kuzichambua na kutoa misaada na maelekezo kwa maafisa ugani ili kuinua ubora wa kazi zao.

(b) Kama nilivyoeleza wakati nikijibu swali namba 96 la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi katika Mkutano wa 14 wa Bunge lako Tukufu, Wataalam waliopo katika ngazi za Wilaya hadi Vijijini walihamishiwa kwenye Serikali za Mitaa tangu mwaka

1998. Lengo la uamuzi huo ni kuwaweka wataalam karibu na Mamlaka zinazowaajiri na karibu na wakulima. Lengo lilikuwa watumishi wasimamie uzalishaji wa kilimo na mifugo kwa karibu zaidi kuliko ambavyo ingekuwa kama wangeendelea kuwa moja kwa moja chini ya Wizara. Viongozi wa Halmashauri za Wilaya na Miji wana jukumu la kuwapangia kazi, kuwasimamia na kudhibiti nidhamu ya kazi. Kazi ya Wizara ni kuandaa miongozo ya kitaalam na kuisambaza Wilayani, kuwapatia Maafisa Ugani mafunzo na matokeo ya tafiti mbalimbali na kushaurina na TAMISEMI na Tume ya Utumishi katika Serikali za Mitaa, juu ya maendeleo na matumizi bora ya Maafisa hao. Hivyo, kama wapo wataalam wavivu, wazembe, watoro na walevi, ni jukumu la Viongozi wa Halmashauri kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Wataalam hao.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, imejitokeza kumbe hawa Mabwana Shamba hasa Wagavi wanafanya kazi chini ya Mabwana wawili, Bwana TAMISEMI na Bwana Wizara ya Kilimo. Matokeo yake bajeti tunayopitisha hapa Bungeni unakuta kwamba wao hata zile zana za kufanyia kazi na usimamizi vinakuwa na utata na hivyo kufanya hawa Maafisa Ugani washindwe kutekeleza wajibu wao chini ya utaratibu wa Wizara moja stahili.

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Je, Waziri yuko tayari kushika hatamu ya Wizara yake bila kuhusisha Wizara nyingine ili kuleta ubora wa kazi hii?

Pili, kwa kuwa kilimo sasa hivi kimeonekana kwamba hakiendelei kutokana na mgongano huu na kwamba kumekuwa na picha kwamba kuna kigezo kingine cha kupata uchumi bora zaidi huenda kikawa cha madini na kusahau kwamba kilimo hiki lazima kizingatiwe kikamilifu.

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Je, Wizara ipo tayari kusimamia uchumi huu wa kilimo ili ilete uchumi sambamba na uchumi wa madini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nirudie jibu la nililotoa katika jibu langu la msingi ni kuwa bajeti inayotumika kuwalipia na kuwahudumia watumishi wa kilimo inatokana na Bunge hili hili. Ipo bajeti inakwenda Wizara ya Kilimo na ipo inayokwenda TAMISEMI na baadaye inafika huko katika Wilaya husika. Lakini mamlaka inayowasimamia wale kazi ni Halmashauri ya Wilaya, nafikiri Moshi Vijijini na siyo moja kwa moja kwa Waziri wa Kilimo. Wizara ya Kilimo inatoa sera na miongozo kama nilivyokwishaeleza lakini haihusiki kumsimamia mtumishi siku hadi siku. Bado ningependa kurudia kuwa Halmashauri ya Moshi Vijijini, ambayo Mtendaji wake Mkuu ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Wilaya, yeye anawajibika moja kwa moja kuwasimamia hawa wasiende huko kwenye machimbo au kwenye shughuli nyingine au kuwa walevi na kadhalika. Huyu Mkurugenzi

anasimamiwa na sisi Madiwani ikijumuisha na Wabunge katika maeneo haya. Bado narudia kusema, tafadhali tuwasiliane katika Wilaya ile na Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya ya Moshi Vijijini na Mheshimiwa Diwani, kuangalia jinsi gani ya kusimamia hawa watumishi kusudi kilimo kineemeke na nikialikwa nitasaidia kutoa ushauri. *(Makofi)*

Na. 42

**Zao Moja la Chakula na la Biashara kwa Kila Wilaya**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliagiza kuwa kila Wilaya iteue zao moja la chakula na la biashara ili mazao hayo yaweze kupewa kipaumbele wakati wa kugawa misaada ya kuinua hali ya kilimo nchini:-

(a) Je, mpango wa Serikali wa kutoa kipaumbele cha misaada *(support)* utaanza lini?

(b) Je, Serikali imejiandaa vipi kuhusu upatikanaji wa mbegu ya ngano inayoweza kustawi katika Jimbo la Bumbuli na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla?

(c) Je, ni Maafisa Kilimo wangapi wameandaliwa ili kutoa mafunzo ya kilimo cha ngano?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwa na zao moja la chakula na moja la biashara kwa kila Wilaya ulitangazwa na Serikali katika Mkutano wa 12 wa Bunge la Bajeti la Mwaka 2003/2004. Utekelezaji wake unafanywa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs),* ambapo Halmashauri huainisha maeneo ya kipaumbele na kutengewa fedha. Serikali katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, kwa kuanzia ilitenga shilingi bilioni nne kwa ajili ya kufanikisha programu hizo. Kati ya fedha hizo, Wilaya ya Lushoto ilitengewa shilingi 46,460,000.

(b) Mbegu bora za ngano zinazalishwa katika mashamba ya Serikali ya mbegu yaliyoko Arusha na Dabaga, Iringa, kwa kiwango cha tani 100 kwa mwaka. Hadi sasa kuna aina nane za mbegu za ngano zinazofaa kwa maeneo ya mwinuko kama ya Wilaya ya Lushoto. Aina hizo ni Mbayuwayu, Azimio, Kware, Juhudi 87, Tausi, Njombe 7, Selian 87 na Viri. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inashauriwa kununua mahitaji ya mbegu kutoka kwenye Shamba la Arusha au Dabaga kwa ajili ya Jimbo la Bumbuli na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla.

(c) Wataalam wote wa kilimo wanaohitimu mafunzo katika Vyuo vyetu kwa Mafunzo ya Kilimo wana ujuzi wa kutoa utaalam wa zao la ngano kwa wakulima. Aidha, kama Wilaya ina mpango wa kulima ngano kwa wingi, Wizara iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kutoa mafunzo rejea kwa baadhi ya Wataalam wa Wilaya ya Lushoto ili kupata Wataalam waliobobea katika kilimo cha ngano ili nao waweze kutoa mafunzo zaidi kwa Wataalam Vijijni na wakulima.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Waziri ametamka kwamba Wilaya ya Lushoto imetengewa shilingi milioni arobaini na mbili, je, ana uhakika kwamba fedha hizo zimekwishapelekwa huko? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa zao la ngano ni zao ambalo linahitaji uangalizi na kwa kweli ni muhimu liende na wakati na uzoefu unaonyesha kwamba mbegu zinapelekwa katika maeneo wakati msimu upo katikati au umekwisha. Je, wakulima wanahakikishiwaje kwamba mbegu zitafikishwa katika maeneo kwa wakati unaofaa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, nimetamka kuwa fedha zimepelekwa katika Wilaya, ninachoomba Mheshimiwa mwuliza swali na mimi tushirikiane kufuatilia maana tukishazitoa kule tunategemea wenzetu waliopokea watujibu. Sasa kama zimepotea hapa katikati inanifadhaisha. Naomba tushirikiane kufuatilia fedha hizi mara baada ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, mbegu kutofika kwa wakati ni jukumu letu sote wawili, anayeagiza akitoa fedha kulipa, kwa hiyo fedha ifike kwa wakati, lakini kama tutachelewa kulipia mbegu hizo na kule hakuna ambaye yuko tayari kuhakikisha zimefika kwa wakati, jambo hili litatupa utata siku zote. Ninachoomba tushirikiane kama tunataka kulima mwezi wa Desemba basi maandalizi yafanyike Septemba na safari hii mimi nitakuwa tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha mbegu zimefika kwa wakati. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 43

**Uuzwaji wa *Share* za *TTCL***

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na mwuliza swali)*

Na. 44

**Mtambo wa Simu za Kisasa Itigi**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaupatia Mji Mdogo wa Itigi mtambo wa simu za kisasa ambao unajiendesha wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Manyoni ni Mji Mkuu wa Wilaya ya Manyoni na una mtambo wa simu za *TTCL* wa aina ya *Neax,* wenye uwezo wa njia 400. Mtambo huu ulipowekwa ulibadili mtambo wa aina ya *C.Dot* uliokuwa na uwezo wa njia 100.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Simu Tanzania, iliahidi kuwa ingepeleka Itigi mtambo wa simu ambao ulikuwa unatumika Manyoni baada ya Manyoni kupata mtambo mpya. Baadaye ilionekana kuwa mtambo huo hauingiliani na *system* ambayo tayari ipo Itigi. Hata hivyo, tunategemea kuupatia Mji Mdogo wa Itigi huduma ya simu za kisasa katika kipindi cha mwaka 2004/2005 iwapo mipango ya Serikali ya kutafuta fedha kwa ajili ya huduma hiyo itafanikiwa.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kupeleka huduma ya simu Vijijini, Serikali inafanya mpango wa kuanzisha Mfuko Maalum ujulikanao kama *Universal Access Fund* ili kusaidia kufanikisha azma hiyo. Wadau mbalimbali watahusishwa katika mpango huo. Kutokana na juhudi hizo za Serikali, ni mategemeo yetu kuwa mara mfuko huo utakapotuna, tatizo la ukosekanaji wa simu Vijijini litapungua kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, hivi sasa tuna Makao Makuu ya Wilaya 18 ambazo bado hazijapata simu za kisasa.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa ahadi hii imekuwa ni ya muda mrefu na mwaka 2003 wakati wa Bajeti nilipata nafasi ya kuongea na Mkurugenzi wa Idara ya Mipango wa Kampuni ya Simu na alikuwa ametoa ahadi nzuri tu. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, atakuwa tayari kuwasiliana na Mkurugenzi wa Idara ya Mipango kuona ile ahadi aliyokuwa ameitoa ya kuhamisha mtambo kutoka sehemu fulani ya Dar es Salaam inatekelezwa kama alivyokuwa ameniahidi mwaka 2003?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kuwasiliana na Mkurugenzi si suala zito ni suala ambalo tunalifanya kila leo, si wa *TCCL* tu, lakini pia wa Kampuni za *Mobitel* tukipata maombi kutoka kwenu na kwa juhudi za Wizara. Hilo Mheshimiwa Mbunge, napenda nikuhakikishie tutalifanya. Lakini bado tunarudi pale pale katika jibu la msingi kwamba, fedha zikipatikana shughuli hii Mheshimiwa Ismail Iwvatta, itafanywa 2004/2005.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali pia yamekwisha, sina matangazo niliyoletewa, kwa hiyo, tunaendelea na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Taasisi za Kazi wa Mwaka 2003
### *(The Labour Institutions Bill, 2003)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Taasisi za Kusimamia Masuala ya Kazi wa mwaka 2003 *(The Labour Institutions Bill, 2003)* na kwa mujibu wa mabadiliko yaliyoambatanishwa, sasa usomwe mara ya pili.

Muswada huu unakwenda pamoja na ule uliopita wa Ajira na Mahusiano katika Kazi, ambao Waheshimiwa Wabunge mmeupitisha hapa Bungeni kwa kuwa unahusu Sheria za Taasisi zitakazosimamia na kuzitekeleza sheria mpya za kazi. Umuhimu wa kuzibadilisha sheria za Kazi na Mahusiano Viwandani, umelazimu pia kuangalia upya mifumo ya Taasisi hizo ambazo zimeonekana kuwa na mapungufu makubwa kama sheria zenyewe zilivyokuwa. Aidha, Taasisi hizo zimeonyesha udhaifu mkubwa wa kutomudu majukumu yanayoendana na mabadiliko ya uchumi na hali ya uajiri ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto ya kuwa na mifumo bora ya uendeshaji wa shughuli za kazi inayoendana pia na mabadiliko ya utendaji Serikalini *(Public Service Reform),* Kamati Maalum *(Task Force),* kwa kuwahusisha wadau wale wale, ilitoa mapendekezo na Serikali iliyatafakari. Serikali kwa upande wake ilitoa maamuzi yenye lengo la kuweka Taasisi zenye kuzingatia miundo na mifumo ya uendeshaji shughuli za kazi ambayo madhumuni yake ni haya yafuatayo: Kuleta ufanisi wa utendaji wa kazi, kupanua mianya yenye kuimarisha Utatu, kujenga mtandao wa ushauriano na majadiliano na kuruhusu shughuli kufanyika kwa uwazi na haki.

Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika sheria inayopendekezwa kutungwa ni pamoja na kuunda upya Chombo cha Utatu cha Ushauri wa Masuala ya Kazi *(Labour Advisory Board),* kwa kupanua wigo wa uwakilshi na kukiongezea demokrasia na wigo wa masuala ya kishauri. Chombo hiki kitajulikana kama *Labour, Economic and Social Council (LESCO).*

Pili, kubadili shughuli na majukumu ya Idara ya Kazi kwa kuondoa shughuli za usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya kikazi na kuziweka kwenye chombo kipya chini ya Wizara kitakachojulikana kama Kamisheni ya Usuluhishi na Maamuzi *(Mediation and Arbitration Commission).*

Tatu, kuweka bayana madaraka, utaratibu na mifumo ya Utatu ya kuweka kima cha chini cha mishahara na vima vya chini vya mishahara Kisekta na vima hivyo kuwekwa bayana kwa wafanyakazi na waajiri wao. Madaraka haya yameondolewa kwa

Rais na kuwekwa chini ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Waziri anayeshughulikia masuala ya Watumishi wa Sekta ya Umma.

Nne, kupandisha daraja kwa Mahakama ya Kazi iliyopo na kuifanya Kitengo cha Mahakama Kuu *(The Division of the High Court)* na kuiondoa chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Tano, Kamishna wa Kazi amepewa madaraka ya kupeleka suala lolote la kisheria katika Mahakama ya Kazi na kupeleka Mahakama ya Rufaa suala lolote linalohusu maamuzi ya Mahakama ya Kazi yanayotofautiana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu una sehemu kuu nane ambazo ni hizi zifuatazo:-

Sehemu ya kwanza, ina vifungu cha kwanza hadi cha pili, ambayo inahusu mambo ya awali kama jina la Muswada, kuanza kutumika kwa sheria na ufafanuzi wa maneno.

Sehemu ya Pili, kifungu cha tatu hadi cha 11 ya Muswada inaelezea kuhusu Uanzishwaji wa Baraza la Kazi *(LESCO),* ambalo ni chombo cha Utatu kwa ajili ya kumshauri Waziri.

Ibara ya nne na ya tano, zinaimarisha kazi, wajibu, mamlaka ya hilo Baraza, muundo wake, masharti na kipindi cha Wajumbe kuwa katika Baraza hilo.

Sehemu ya tatu, kifungu cha 12 hadi 28 ya Muswada inaweka utaratibu wa namna ya kuanzishwa Tume ya Usuluhishi wa maamuzi ya migogoro *(Mediation and Arbitration Commission).*

Kifungu cha 13 kinaelezea Mamlaka ya Tume hiyo na hadhi yake kwamba, Tume itakuwa ni Idara ya Serikali ambayo itakuwa huru.

Kifungu cha 14 mpaka 17 vinaelezea kuhusu kazi za Tume, mamlaka yake, muundo na masharti ya kazi na kipindi cha Makamishna wa Tume kutumikia. Vilevile katika sehemu hii Muswada unazungumzia uteuzi wa Mkurugenzi wa Tume hiyo na Wasuluhishi wa Migogoro *(Mediators and Arbitrators),* wanavyochaguliwa kwa mujibu wa vifungu vya 18 na 19. Katika sehemu hii utaratibu umewekwa jinsi ambavyo wasuluhishi wa migogoro watakavyotekeleza shughuli zao za kusuluhisha migogoro.

Sehemu ya nne, ni kifungu cha 29 mpaka 33, ina kifungu kuhusu Kamati ya Huduma muhimu. Katika sehemu hii ya Muswada vipo vifungu kuhusu kuanzishwa kwa hiyo Kamati, kazi zake, uteuzi wa Wajumbe wa Kamati hiyo, mamlaka yake na utawala.

Mheshimiwa Spika, hii Kamati inayozungumziwa hapa ni ile *Essential Services Committee.* Kazi ya Kamati hii ni kutambua ni aina gani ya kazi ndiyo muhimu kwa mujibu wa kifungu cha 76 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano katika Kazi, ambazo

sehemu hizo wafanyakazi watazuiliwa kufanya mgomo au kufungia nje. Kamati hii itasikiliza mashauri kuhusu mfanyakazi fulani au aina fulani ya kazi au huduma kuwa siyo huduma au kazi muhimu.

Sehemu ya tano, vifungu 34 mpaka 42 ya Muswada huu ina vifungu kuhusu uanzishwaji wa Bodi ya kupanga kima cha chini cha mishahara ambayo kazi yake itakuwa ni kumshauri Waziri wa Kazi kuhusu masuala ya upangaji wa kima cha chini cha mishahara na masharti ya ajira kisekta. Bodi zitakazoanzishwa katika sehemu hii hazitakuwa za kudumu badala yake zitakuwa zinaanzishwa kila inapohitajika kufanya hivyo, kwa kusudi la kupunguza gharama na kuleta ufanisi wa kazi. Sehemu hii ina vifungu 6 vinavyoelezea masuala ya Bodi hizo kuhusu kazi yake, mamlaka yake na taratibu za kufanya ukaguzi na namna ya kuandaa na kuwasilisha taarifa.

Sehemu ya sita, ina vifungu 43 mpaka 49 ya Muswada ambayo inahusu mfumo wa uendeshaji kazi na kaguzi za kazi *(Labour Administration and Labour Inspection).* Kifingu cha 43 kinaweka masharti ya jinsi ya kufanya uteuzi wa Kamishna wa Kazi na Maafisa wengine wakati vifungu 44 hadi 49 vinaelezea mambo ya kukasimu madaraka ya Kamishna kwa Naibu Kamishna, Mamlaka ya Maafisa wa Kazi, amri ya kutekeleza agizo, rufaa na mambo ambayo ukifanya Afisa wa Kazi yatakuwa ni kosa.

Sehemu ya saba, inahusu vifungu 50 mpaka 58 ya Muswada ambayo inaelezea kuanzishwa kwa Kitengo cha Mahakama ya Kazi kuwa mojawapo ya Idara za Mahakama Kuu zilizo katika Muundo wa Mahakama Kuu kwa ajili ya kutoa maamuzi ya migogoro ya kikazi. Hivyo, kifungu 50 hadi 55 vinaelezea mamlaka na masuala yatakayoshughulikiwa na Mahakama hiyo, uteuzi wa wasajili, sheria ndogo za Mahakama hiyo, namna ya kuwakilishwa katika Mahakama hiyo, rufaa na mambo ya kisheria, ambayo yanaweza kukatiwa rufaa kupelekwa katika Mahakama hiyo.

Sehemu ya nane ina vifungu 59 hadi 66 ya Muswada ambavyo vinaweka mambo ya jumla kuhusu utunzaji siri, wajibu wa kuthibitisha katika shauri lolote kuhusu ukiukwaji wa sheria za kazi, kuthibitisha kwamba yeye ni mwajiriwa, maelekezo ya kanuni za namna ya kutekeleza sheria hii na ambayo yatatangazwa na Waziri, makosa na adhabu pamoja na kifungu kuhusu mambo ya mpito. Vilevile katika sehemu hii ya Muswada kuna jedwali ambalo linaelezea viapo vinavyotakiwa kufanywa na Kamishna, Wakurugenzi na watatua migogoro.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza kutoa hoja yangu, naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa michango yao iliyoboresha Muswada huu mpaka ukafikia katika hatua hii.

Aidha, shukrani za pekee ziende kwa wadau wa Utatu, wafanyabiashara na watu binafsi, waliotoa mawazo yao ya namna ya kuboresha Muswada huu. Niwashukuru pia Wataalam mbalimbali wa Sheria, Kamishna wa Kazi na Wataalam wake, kwa kazi kubwa ya kuchambua masuala mbalimbali ya kazi mpaka kufikia hatua hii. *(Makofi)*

Ninawashukuru kwa nafasi ya pekee, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na Katibu Mkuu, Bwana Abubakar Rajab, kwa kunipa ushirikiano wa hali ya juu ili kufanikisha Muswada huu.

Pia napenda nimalizie kwa kuwashukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, liujadili Muswada huu na kuupitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Hii ni heshima kubwa kwa Bunge letu na kwa Tanzania kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati yangu juu ya Muswada wa Sheria ya Taasisi za Kusimamia Masuala ya Kazi *(The Labour Institutions Bill, 2003),* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Namba 70(2), Toleo la 2004, kama Mwenyekiti wangu alivyoeleza katika Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Kamati ilipitia hatua zifuatazo kabla ya kufikiria Muswada huu:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria Semina iliyoandaliwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO).* Semina hiyo ilifanyika Morogoro tarehe 30 - 31 Oktoba, 2003. Semina hiyo ilihudhuriwa pia na wadau mbalimbali ambao waliweza kutoa maoni yao ambayo mengi yamezingatiwa na Serikali. Napenda kuipongeza Serikali kwa utaratibu huu wa kushirikisha Kamati pamoja na wadau mapema.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu wa *Public Hearing,* unaowawezesha watu mbalimbali kuhudhuria Vikao vya Kamati za Bunge na kutoa maoni yao, tarehe 6 - 7 Aprili, 2004, Kamati yangu ilikutana na kupokea maoni ya wadau mbalimbali wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, wadau walioshiriki ni wale wale ambao walitajwa hapa jana na Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Kamati yangu inawapongeza wadau hao kwa umakini waliouonyesha katika kuchambua Muswada huu kwani maoni yao kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati katika kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, Kamati yangu kwa kiasi ilikubaliana na Serikali na kwa jumla inaunga mkono na imeridhika na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha Taasisi itakayosimamia masuala ya kazi. Hata hivyo, Kamati inashauri katika maeneo kadhaa ili kuboresha zaidi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 31, kimsingi Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, katika kifungu cha 31(1)(a), ni ushauri wa Kamati yangu kuwa itajwe idadi ya Wajumbe wa Kamati *(Essential Services Committee),* watakaoteuliwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 43(2), Kamati inashauri kifanyiwe marekebisho ili kiwekwe katika muundo mzuri ambapo Ofisi ya *"Registrar"* itakuwa ni Idara inayojitegemea chini ya Katibu Mkuu wa Wizara, badala ya kuwa chini ya Kamishna wa Kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 50(1), Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, sheria itamke kuwa mfanyakazi hatatakiwa kulipa ada yoyote kwa shauri lolote atakalopeleka Mahakamani linalohusu ajira yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 52(2), Kamati inashauri maneno yaliyotumika yafanyiwe marekebisho ili bila ya kubadili maana yaweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotamka awali, ushauri wetu kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na Serikali. Ni matumaini yangu kuwa yale ambayo sikuyagusia, Wajumbe wa Kamati hii na Waheshimiwa Wabunge wengine, watachangia watakapopata fursa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Alhaj Mtarajiwa, Katibu Mkuu wa Wizara, Bwana Abubakar Rajab, Kamishna wa Kazi, Bibi Regina Rweyemamu, Wawakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wataalam wote walioshirikiana nao, kwa maelezo ya kina na ufafanuzi waliotoa mbele ya Kamati. Aidha, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao mbele ya Kamati, ambayo yamesaidia sana kuboresha Muswada huu.

Kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu, kwa kushiriki kikamilifu katika vikao na kutoa michango ya kina ambayo imewezesha Muswada huu kuwa katika sura ionekanayo sasa, tofauti na ilivyokuwa awali. Naomba kuwatambua kwa kuwataja Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo: Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yussuf Kombo

Juma, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Omar Mohammed Mwenda, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde, Mheshimiwa Janeth Edward Mashele, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri na Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

Aidha, napenda kumpongeza Katibu wa Kamati hii, Bibi Angelina Sanga, kwa kuihudumia vyema Kamati na kutayarisha maoni kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu 43(5)(c), Toleo la mwaka 2003, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi za Kusimamia Masuala ya Kazi ya mwaka 2003.

Vilevile napenda kutoa shukrani na pongezi zangu binafsi na za Kambi nzima ya Upinzani, kwa Mheshimiwa Getrude Mongella na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kuongoza kwenye Medani ya Kimataifa.

Vilevile namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, pamoja na wadau wote waliofanikisha na kuhakikisha kuwa kasoro ambazo zilikuwa ni za waziwazi na za kiufundi ndani ya Muswada huu, zinatolewa na kuwekwa wazi kwa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kambi ya Upinzani, namshauri Mheshimiwa Waziri kwenye kifungu 31(5) cha Muswada huu, kuweza kupata maoni na ushauri wa kila Idara kati ya hizo Idara ya tatu kabla ya kufikia hatua ya kutoa maamuzi yanayohusu Wajumbe wa Baraza la Kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, Kambi ya Upinzani haina matatizo na Muswada huu na inaunga mkono kupitishwa kwa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kabisa katika kuchangia Muswada huu. Awali ya yote, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama, naomba nimpongeze Mheshimiwa Balozi GetrudeMongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzake, kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika kutoka ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niseme jambo tu la jumla kuhusu Muswada huu, ambalo nadhani ni muhimu tukaliweka wazi na litusaidie katika kutazama mwelekeo wetu. Wakati sina tatizo la msingi na Muswada huu na hata ule wa

jana. Nina tatizo na dhana kwamba utandawazi unatuongoza na kwamba kutokana na mabadiliko ya kiuchumi katika dunia, sasa lazima tusukumwe na sheria za utandawazi ambazo sisi hatuna mamlaka nazo, hii ndiyo inanipa tatizo.

Mimi nadhani ni vyema kabisa tukajua kwamba, utandawazi sisi siyo pekee duniani na walimu wakubwa wa utandawazi ndiyo wenzetu wakubwa hao, Marekani ndiyo wenyewe, Uingereza ndiyo wenyewe, Ujerumani wenyewe na Japan ndiyo wenyewe. Lakini kwao sheria zao ukizitazama cha kwanza zinalinda wananchi wa nchi yao na mimi inanipa tatizo tunapokuta kwamba tunajifunua, lakini sisi hatuweki vigezo vya msingi katika kulinda watu wetu. Hili nalisema kwa dhati kabisa kwamba, tusipoangalia, tulifungua milango ikawa huria katika soko huria na kwa kweli matokeo yake tumeyaona imeleta uholela na sasa tukifanya tukaachia na hapo tutaingia kwenye tatizo hilo hilo. Tunakumbuka yaliyotokea wenzetu wa Ulaya ndiyo wenyewe waliokuwa wanafanya maandamano kupinga utandawazi, Seattle tuliona hilo, Uswiss walipokutana watu wa *WTO* waliandamana na mwisho Cancun pia walifanya hivyo.

Kwa hiyo, ningependa sheria zetu kwa makusudi kabisa zilinde Watanzania na hivyo Taasisi zote tunazoziunda ni lazima ziwe na sheria za makusudi za kulinda pia watu wetu. Haiwezekani sisi tukawa Taifa ambalo tunafungua milango, tunaziachia nchi nyingine, tunaachia *principles* au misingi ya utandawazi ndiyo inaendesha nchi yetu. Hilo ningependa kutoa kama tahadhari ya awali.

La pili, ni hali ambayo inajitokeza katika nchi yetu na kwenye Muswada huu, inajitokeza zaidi kwamba sasa Waziri ataunda anachokiita *Wage Board. Wage Board* ndiyo itakayokuwa inamshauri Waziri kuhusu vima mbalimbali vya mishahara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza hata leo kabla ya sheria hii ni kwamba, tumeanza kuwa na vima mbalimbali vya mishahara na tofauti imeanza kuwa ni kubwa kati ya Watanzania na wanaachana japo wanakuwa na kisomo cha aina moja, wana sifa za aina moja, wamemaliza Vyuo Vikuu labda mwaka mmoja na tarehe moja, lakini kwa kuwa wameajiriwa katika sehemu mbalimbali, tofauti inaanza kuwa kubwa.

Sisi si peke yetu tunaoendeshwa pia na taratibu hizi za utandawazi pamoja na sifa za ajira. Wenzetu wa Denmark, kwa mfano au *Scandinavian Countries* zote, kwa pamoja na wao pia wanaendesha na sifa hizo hizo, lakini wana kitu kinachoitwa *spill over effect* kwamba wale wenye kuwa nazo kwa mfano, Makampuni makubwa ya Madini, utakaporuhusu wakapata mishahara mikubwa na wengine wakawa na midogo na hakuna *spill over* kutoka kwenye Makampuni hayo ambayo yana *substitute* wale wa chini, hali itaendelea kuwa mbaya katika nchi yetu. Tutazusha na kuzalisha majambazi, tutazalisha mifarakano katika jamii, tutazalisha watu kujiona kwamba ni wa tabaka la chini na kadhalika.

Mimi ningependa hili Serikali iliangalie vizuri na Bodi hii kwa sababu inaundwa pamoja na zile Taasisi nyingine, ziwe na kazi kubwa ya kushauri Waziri namna gani misingi ya Taifa hili ambayo imeundwa kwa miaka 40, kwa mshikamano na umoja

mkubwa, kwa kuwa karibu wote tunafanana, misingi hii isije ikabomolewa leo kwa sababu eti tumeingia kwenye utandawazi. Ningependa nitoe hiyo kama tahadhari.

Sasa baada ya hayo, naomba niingie kwenye maeneo mbalimbali kwa lengo la kusaidia Muswada wetu. Kwanza, niseme kwamba, kwa bahati nzuri mimi ni mmoja niliyeshirikishwa katika semina zilizotajwa na nashukuru kwamba, maeneo mbalimbali ambayo tulichangia yamechukuliwa, namshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa hilo.

Katika sehemu ya pili, ukurasa wa 6, kifungu cha 4(1), linapozungumziwa suala la kuchagua Mwenyekiti wa hiki kinachoitwa *Labour Economic and Social Council,* ningependa sifa za huyo Mwenyekiti, zingeainishwa wazi kabisa. Hiki ni chombo muhimu, kazi zake zimeainishwa kule kwenye ukurasa nafikiri ni wa 7 mpaka 8 na kazi hizi ni nzito na ndizo zitakazojenga misingi ya kazi katika nchi yetu. Tusipokuwa na Mwenyekiti, ambaye tumemuainisha, mimi nadhani tutakuwa na tatizo huko mbele. Nafikiri hili ni jambo muhimu, ni kweli wamemtenganisha kwamba, asiwe ni mwajiriwa, asitoke kwenye *Trade Unions* na asiwe ni mfanyakazi wa Serikali. Lakini sifa zake hazikuainishwa. Ningependa hizo sifa zingelijulikana ili apatikane mtu ambaye hawezi kunyooshewa kidole kwa jambo lolote lile.

Katika sehemu ya pili ya Ibara hiyo hiyo ya 4 pale Waziri anapowateua *(to invite nominations),* anaalika mialiko. Ningelipenda katika kifungu cha (c) na (e) kuhakikisha kwamba, kwa kweli *Trade Unions* zinashirikishwa na zenyewe zishiriki kikamilifu na kusiwe na namna yoyote ya ubaguzi au namna yoyote ya upendeleo wanapotolewa au kusaidiwa kupendekeza watu hawa. Hiki ni muhimu ili tuweze kupata vigezo vya watu ambao kwa kweli wataenda kuwa muhimu. Hawa ndiyo wanaopendekeza baadaye *Labour Market Policy*, sera nzima inayohusu *Labour.* Sasa tusipopata watu waaminifu kwa kweli tutapata tatizo.

Lakini napata tatizo kwenye kifungu cha 3 cha kazi yake: *"the prevention and reduction of unemployment"* kwamba, wanashauri hilo. Ni kweli lakini sina hakika kama hutawachagua vizuri na kwa uwiano mzuri wakaweza kufanya kazi nzito kama hiyo. Lakini kikubwa zaidi ni kwamba, wanatakiwa wafanye *research into Labour Economic and Social Policy,* sijaona mahali popote wanapopewa bajeti. Kwa hiyo, nafikiri kwamba ni muhimu bajeti ya watu hawa iainishwe ili waweze kufanya kazi hii. *Stability* ya nchi yoyote inategemea *Labour Market* yake na kama huna fedha za kutosha na kukiwezesha chombo hicho kufanya kazi yake kwa umakini na bila upendeleo na bila ubaguzi, kwa kweli huwezi kupata matokeo mazuri. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, bajeti ya kifungu hicho pia nayo ingeliwekwa mahali ambapo panaweza pakakubalika vizuri.

Ninadhani vilevile katika sehemu ya 10 ambapo wanaweka *Permanent Secretary* ndiyo ana-*provide Secretariat*, lakini hii inaondoa ule uhuru wa chombo hiki kufanya kazi yake vizuri. Nadhani bajeti yake iwe kasma inayojitegemea ili wawe huru kutoka kwa huyo *Parmanent Secretary,* asimamie kama kawaida anavyosimamia Bajeti ya Serikali, lakini *at least* tuwe na kasma ambayo inajitegemea wasiende kuomba fedha kutoka kwenye Kasma ya Katibu Mkuu kila wakati wanapotaka kufanya kazi yao. Hasa

hivi vipengele vya *consultation* vya kila mahali na kwenye kifungu cha 10(2)(b), wanatakiwa wapate *express approval* wanapotaka kuweka watu wao ambao wanawafanyia kazi. Hizi *approval* ndizo zinazofanya baadaye kazi zingine ziweze kushindikana. Nadhani tuna *experience* ya kutosha sasa hivi tunapoweka vipengele vya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipengele cha 16, nilifikiri vile vile kuna tatizo kidogo. Kwa upande wa kuchagua huyu Mwenyekiti wa *Commission* tuliyemwita *Commission* ya *Mediation Arbitration,* ambayo mimi naiona ni *Commission* muhimu sana, migogoro ni lazima itatokea, kama katika familia inapotokea. Kwa hiyo, kutakuwa kuna migogoro ya hapa na pale na migogoro lazima isuluhishwe. Sasa nilifikiri kwa ajili ya kupata *independence* kamili ya watu hawa, *Trade Unions* zilitakiwa ziweze kupendekeza Wajumbe.

Kwa sababu hapa inasema: *"Two Commissions proposed by Members of the Council representing the interest of the employees". Proposed by the Council,* huko nyuma tumesema anayetakiwa katika *quorum* ni mmoja tu. Sasa huyu mmoja upande wetu ukizidiwa huwezi kupata ile *balance* unayotaka. Kwa hiyo, tutapendekeza mtu ambaye si wa eneo lile.

Lakini kwa upande wa Serikali kwenye kifungu cha (d) tumesema *to represent the government,* hapendekezwi na *Council.* Lakini kwa *employers* na *employees* anapendekezwa na *Council*. Mimi nilidhani kuna umuhimu wa kuachia kitu hiki wenyewe wapendekeze kwa sababu ni *arbitration* inahusu maisha yao, inahusu maslahi yao. Lakini unatoa kwenye *Council* ambayo ni jumla ina-*represent* watu wengi na kura ikipigwa wa Serikali na wa *employees* wakiwazidi wale wafanyakazi wenyewe, haki yao inaweza ikamezwa. Mimi nilidhani hapo kuna hoja ambayo ni lazima tuangalie na hapa ndio tunataka kulinda watu wetu. Hapa ndio ninaposema kwamba, lazima na sisi taasisi zetu zilinde maslahi ya nchi, maslahi ya wafanyakazi na ndio hapa ninaposema kwamba, ni lazima vyombo vya namna hiyo tuviangalie na tuwape watu wetu nguvu ya kutosha hata kama hatutaki kuwabagua, kama hatutaki kuwapendelea. Nadhani hicho ni kipengele muhimu na kinahitaji kuangaliwa katika sura hiyo.

Katika kipengele cha 23 nilidhani vile vile kuna suala zito kabisa. Tunazungumzia fedha zitakazopatikana kwa ajili ya taasisi ambayo itashughulikia masuala ambayo tumeyasema kwa wale Makamishna watakaopatikana kushughulikia mambo ya *mediation.* Uzoefu kwa mfano sasa hivi tunapata Tume ya Haki za Binadamu lakini bajeti yake sehemu kubwa inatoka kwa mfano, kwa wafadhili kutoka nje. Sasa *arbitration* hapa inahusu migogoro ya kazi. Wawekezaji wengi wanatoka nchi za nje. Ukiachia fedha zinatoka kwenye *donation* na zinatoka kwenye nchi hizo hizo ambao ndiyo nchi zao zime-*invest* hapa, mimi nadhani tunaweza *eventually* tuka-*compromise.* Kuna suala la ubinadamu na ni vyema bajeti kubwa ya chombo hiki cha *arbitration* zitoke kwenye vyombo vyetu.

Kuna bajeti ya Serikali imetajwa lakini baadaye tunakwenda tunasema kwamba, zitokane na *donations grants, requests may from time to time receive without*

*compromising their independence.* Ki-*principle* ni rahisi kuisema kwamba sheria imetaja iwe *independent* lakini katika hali halisi, mtu anayekupa fedha kimsingi ndiyo atakayetawala mwelekeo wako. Kwa hiyo, mimi nilifikiri kwamba, kuna umuhimu mkubwa kabisa, *independence* ya chombo hiki ilindwe na wananchi wetu tutawalinda pale ambapo Serikali yetu na sisi wenyewe kwa njia zetu ndio tunatoa fedha za kuwezesha waweze kufanya kazi hii. Si tena tutegemee vyombo vingine hata kama ni muhimu. Hata kama hela hizo zitaingia isiende *directly* kwao. Hata kama hela hii itakuja iende Serikalini, iende Hazina na Hazina ndiyo itoe hizo hela. Lakini sio iende *directly* kutoka kwa mfadhili ziingie kwenye *account* ya *Commission* hiyo ndiyo zitumike na unapata *influence* na hao ndio wanapata nafasi ya kwenda kuwashughulikia.

Katika kifungu cha 30, nakwenda haraka kidogo, ni suala la *Essential Service Committee.* Naona hapo bado kuna *arbitrariness,* tuliisema hata kule Morogoro. Mimi nisingependa kuiachia hii nafasi ya *Essential Service Committee* pale kwenye (a) tunaposema: *"to designate essential services in terms of section 76".* Nadhani kuna umuhimu wa kuzitaja hizo *essential services.* Haiwezekani kila wakati mgogoro unapotokea ndio Kamati hii ikae iseme kwamba hizi ndizo *essential services. Essential services* lazima zitajwe kwenye sheria ili mfanyakazi anapogoma anajua kwamba, mimi katika *category* hii utaratibu wangu ni huu na huu. Lakini unakuta siku wamegoma ndio Kamati imekaa inasema nyie mlikuwa hamruhusiwi kugoma kwa sababu mko kwenye eneo la *essential service*. Mimi nadhani hapo tuna-*compromise* ile *quality* yenyewe ya kazi inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nisigongewe kengele nyingine, ninafikiri ningependa kuzungumzia vile vile katika kifungu cha *Commissioners* cha *Wage Board* ambapo kinasema: *"The Minister may remove a member from office at any time".* Hawa *members* ni wale *members* wanaolinda. Tusitoe madaraka kwa Waziri kumtoa wakati wowote bila sababu. Inawezekana huyu ndiye mtetezi mkubwa wa wafanyakazi. Inawezekana kabisa huyu ndiye mwenye kupiga kelele kuliko wengine wote. Waziri atashawishiwa tu kwenda kumwondoa kwa sababu ni mtetezi. Tuna uzoefu kila wakati sasa hivi inatokea kwamba, yule anayetetea wafanyakazi, kiongozi wa wafanyakazi, amekwisha ondolewa kwenye nafasi yake kwa sababu tajiri hamtaki.

Sasa tusitumbukie kwenye mtego huu kwa kusema tu: *"The Minister may remove a member from office at any time"* , bila kutaja sababu. Ile ya kifungu kinachofuata (b) angalau kinaweka vipengele vingine. Lakini vile viko *clear* na sielewi ni kwa nini kifungu hiki cha (a) kimewekwa pale, kimetumbukizwa ili kumpa mamlaka Waziri amwondoe huyu ambaye labda ndiyo mtetezi mkuu wa nchi. Ni vyema kuondokana na *arbitrariness* yaani kuepukana na hali hii ya mtu kuweza kuondolewa tu kwa sababu hawezi inaweza kuwa ni ya tuhuma au inawezekana tu ikajengewa sababu akaondolewa Waziri akashawishika, Waziri hajapata nafasi ya kuchunguza vizuri akamwondoa na mimi nadhani hilo itakuwa vizuri tuondoe kipengele hicho tuweze kusaidia kifanye kazi yake vizuri kadri inavyowezekana.

Katika kipengele hiki cha *wage limit* vile vile ninaona kuna mlolongo mrefu umepangwa wa kuweka vima vya chini vya mishahara. Mimi nadhani hivi vipengele

vyote kuanzia kifungu cha 30 mpaka kwenye kifungu kidogo cha (i) mpaka (v), vinatoa mlolongo mzima na havitoi *time limit,* lini *minimum wage* iweze kutangazwa. *Process* yote inakwenda kwenye *consultation.* Sasa inaweza kukaa hata miaka mitano watu haki yao bado haijawekwa. Wafanyakazi wanangojea mishahara, wanangojea kima chao cha chini lakini hakitangazwi kwa sababu Kamati ile haijakutana kwa sababu *consultation* ile haijafanyika. Mimi naomba huu mlolongo uwekewe muda. *Consultation* labda ni lazima lakini isiachwe tu huria na mtu asipate nafasi ya kufanya *consultation* inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu. Kabla sijaanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa nyadhifa ambazo wamepata Kimataifa ambazo zinaonyesha kwamba nchi yetu inaheshimika kiasi gani nje huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na timu yake yote, kwa kufikiria kuleta hii miswada miwili hapa Bungeni. Kwa kweli sheria za kazi zilitungwa siku nyingi sana na zilikuwa zimeshakuwa *outdated* kiasi kwamba, kwa wale ambao walikuwa wanazitumia walikuwa wanapata matatizo makubwa sana. Ninachowaomba wasichoke. Ziko nyingine zilizobaki waendelee kuzifanyia marekebisho hasa *Workmen's Compensation Ordinance* ni sheria ambayo kwa sasa hivi haifai kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye Muswada huu. Nasema kwamba, naunga mkono Muswada huu moja kwa moja na jitihada iliyofanywa ya kuleta sheria zote zinazohusu masuala ya ajira na masuala ya utatuzi wa migogoro ya ajira katika sheria moja ni jambo ambalo lazima liungwe mkono kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninayo mawazo machache ambayo nataka kuyatoa katika juhudi za kuboresha huu Muswada. Naomba niende kwenye kifungu cha 20, kifungu kidogo cha 4. Katika kifungu kile msuluhishi *(Mediator or Arbitrator),* amepewa uwezo wa kumwona mtu amedharau kikao chake *(Contempt of the Commission).* Kile kifungu kinasema kwamba, baada ya kuona hivyo atapeleka uamuzi wake Mahakama ya Wilaya upate baraka zao na baada ya hapo ile Mahakama ya Wilaya baada ya kufanya *summary hearing* inaweza ikatoa adhabu.

Mheshimiwa Spika, mashaka yangu ni kwamba, hapa mshtaki amekuwa Hakimu. Yeye anayetuhumu kwamba amedharauliwa anapewa uwezo wa kuamua kwamba tayari mtu ameshamdharau. Suala la kama mtu amedharau *tribunal* au hakudharau ni suala la Kimahakama. Ningeomba iwe kwamba huyu *mediator or arbitrator* akiona vitendo vya dharau aripoti kwa vyombo vinavyofaa ili mtu ashtakiwe kikawaida kwa sheria ya *contempt.* Kifungu kidogo cha 5 hakiokoi hii hoja kwa kusema kwamba, kutakuwa na *summary hearing. Summary hearing* haileti ushahidi wote. Mahakama haitaweza kupata

maelezo kamili kwa nini kwa mfano mtu amekataa kutoa ushahidi. Lakini angepewa nafasi ya kujieleza kwa nini ameshindwa kutoa ushahidi, basi angeweza kui-*satisfy* Mahakama kwamba, hakufanya dharau. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, kifungu kidogo cha 4 kiwe tu kwa ajili ya mashtaka kupelekwa kwa vyombo vinavyohusika.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye kifungu cha 39, *wage order,* ni matumaini yangu kwamba, mishahara itakuwa inakuwa *reviewed* mara kwa mara kwa kadri inavyowezekana. Tumekuwa na *minimum wage board* lakini *minimum wage board* haikuwa inafanya kazi yake kikamilifu. Wafanyakazi wamekuwa wanalalamika sana juu ya mshahara kutokuwa unatosha, majibu yamekuwa hali ya uchumi. Lakini kwa ninavyojua, *minimum wage order* ambayo imetolewa kwa upande wa sekta binafsi, imetolewa siku nyingi sana. Hii kwa kweli inaumiza wafanyakazi wetu. Ni matumaini yangu sasa maadam kuna sheria mpya itakayotumika, Waziri ataitumia hii Bodi kikamilifu na aweze kuwapunguzia wafanyakazi wetu matatizo ya kipato chao kuwa kidogo zaidi kuliko gharama za maisha. Ni jambo ambalo liko wazi kwamba, zamani Serikali ikitangaza mabadiliko ya mishahara ya Serikali, *Private Sector* au waajiri binafsi hawakuwa wanafuatilia hilo tangazo la Serikali kwa upande wa wafanyakazi wake na utetezi ulikuwa kwamba, Serikali kama mwajiri, imeamua kuongeza mishahara kwa wafanyakazi wake. Tumekuta hali ambayo aidha kwa Mikataba Binafsi au kwa mwajiri tu kukataa mishahara ya Serikali. Wakati mwingine imekuwa kima kile kidogo kimekuwa juu kidogo kuliko vima vingine vya chini katika *Private Sector.* Hii inaonyesha wazi kwamba, ile *Minimum Wage Board* haikuwa inafanya kazi sawa sawa. Ninaomba kwa sasa hiyo *Minimum Wage Board* itakayoundwa, iweze kufanya kazi zake sawa sawa. Niko *conscious* na jambo hili kwamba chini ya kifungu cha 41(1) imeelezwa wazi kwamba, kukitokea *minimum wage order* basi *employers* wote watatakiwa waifuate. Ninaomba watu wa *Labour* waweze kushughulikia hilo jambo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye *Labour Administration,* kuna kifungu cha 45 ambacho kinaeleza juu ya madaraka ya *Labour Officers* kufanya *inspections.* Hizi *inspections* zimekuwepo lakini mara nyingi watu wamekuwa wanakufa katika viwanda vyetu hasa viwanda vya chuma. Kuna *accidents* ambazo kungekuwa na *inspectorate* ambayo inafanya kazi yake sawa sawa, hizi ajali hazingetokea. Kuna *accidents* kwenye migodi, ninaomba hii *inspectorate* iwe *strengthened* na baada ya kuwa *strengthened* wawe wanafanya *inspection* zao *more frequently.*

Naomba sasa suala ambalo naona kwangu ni *serious* zaidi ni suala la *Labour Court*, kifungu cha 50. Nahofia sasa tuna Idara ya Mahakama Kuu nyingi mno ambazo zimeitwa Mahakama. Tuna *Land Court,* ambayo ni Idara ya Mahakama Kuu, tuna *Commercial Court,* ambayo ni Idara ya Mahakama Kuu, sasa tunaleta tena *Labour Court.* Hizi sheria zetu tulivyozitunga zinaonyesha kwamba, zile Mahakama ni Mahakama ambazo ziko tofauti. Sasa nilikuwa nafikiria badala ya kutumia *Labour Court, Land Court* na *Commercial Court,* tungetumia *Labour Division.* Ieleweke wazi ni *Labour Division* ya *High Court.* Hiyo italeta *impression* nzuri zaidi katika sheria zetu kwamba, hatuundi Mahakama mpya ila tunaunda Idara ndani ya Mahakama Kuu, ambayo ina Mamlaka *exclusive* ya kusikiliza kesi ambazo zinatokana na masuala ya *Labour*. Kwa hiyo, ningemwomba Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wafikirie namna ya

kurekebisha hili jambo, *at least* tumefanya makosa tulipoanzisha *Commercial Court* na *Land Court,* tuanze sasa tusirudie hilo kosa baada ya kuliona, tufanye *amendments.*

Nilikuwa nafikiri kwamba, ikiwa itabidi basi, wakati wa Kamati nita-*introduce schedule of amendment* ili neno *"Labour Court"* liweze kuondolewa liwekwe *"Labour Division of the High Court".* Pamoja na hayo, ninafikiria kile kifungu cha 50 kinatakiwa kipunguzwe, ukishasema: *"Labour Division of the High Court",* huna haja ya kusema itakuwa na Jaji wa *High Court* tena maana yake Jaji wa *High Court* tayari atakuwepo. *It is the High Court.* Kwa hiyo, kutakuwa na haja ya ku-r*ecast section 50* ili iweze kuendana na hayo mabadiliko ambayo nimeyapendekeza.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kutoa ombi. Sasa hivi tunayo taabu sana katika Mahakama za Ardhi. Hatujaweza kufungua kesi za ardhi kwenye Mahakama za Wilaya au za Mkoa kwa sababu hazijaundwa tangu ile sheria itungwe. Mahakama Kuu, *Land Division* inafanya kazi. Sasa tunamwomba Waziri kwamba, tukipitisha hii sheria, hizo Mahakama na *Tribunal* na *Commission* ziwe *set up* mara moja kwa sababu tutaachwa kwenye sehemu ambayo wafanyakazi wetu watababaika waende wapi kutatua matatizo yao. Tumekuwa na tabia ya kuanzisha hizi *institutions* bila kuzifanya zianze kazi mara moja. Naomba Wizara ya Kazi, ionyeshe mfano wa kazi bora, zianze mapema iwezekanavyo ili ile *transitional period* kati ya kuondoa ile Mahakama ya Kazi iliyopo sasa na wakati ambapo tutakapokuwa sasa na hii *Labour Division* kusiwe na *suspense* na wafanyakazi na waajiri waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ikiwa mawazo yangu yatazingatiwa nasema naunga mkono hii hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, lakini kwa kukusaidia Mheshimiwa Lamwai, nimekusikia katika mchango wako ukisema ikibidi wakati wa Kamati ya Bunge Zima, utaleta *schedule of amendments.*

Mheshimiwa Naibu Spika, alieleza jana jioni katika Muswada uliotangulia juu ya utaratibu unaofaa kutumika ni kifungu cha 70(4) kinachosema: "Vile vile katika hatua hii yaani ya kujadili Muswada kwa mara ya pili, Mbunge yeyote aweza kuwasilisha kwa Katibu, taarifa ya maandishi kuhusu mabadiliko anayokusudia kuyafanya katika Muswada huo wakati wa Kamati ya Bunge Zima". Kwa hiyo, kama una kusudio hilo ni vizuri ukawasilisha maandishi kwa Katibu ili awe nayo kabla ya Kamati ya Bunge Zima.

**MHE. PHILLIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa vile pia ni mara yangu ya kwanza kusimamia katika mkutano huu, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais au Spika wa Bunge la Afrika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mongella, ningeshauri aendelee na tabia ya kusafiri kwa mtumbwi mara kwa mara ili mazoea hayo baadaye iwe rahisi kuchaguliwa kuwa Mbunge na wenzetu watakaokuwa hapa mwaka ujao wamchague tena kuwa

Mbunge wetu katika Bunge la Afrika na aendelee kuwa Spika wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada huu, mimi nina machache ya kusema. Imeelezwa kwamba, Muswada kwanza unaunda taasisi kadhaa za kumshauri Waziri wa Kazi. Pia inaunda Tume ya Usuluhishi na inaunda Kamati ya Huduma Muhimu, inaunda Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara, inaunda Kitengo cha Ukaguzi na pia inaunda Mahakama ya Kazi. Kwa kweli Muswada huu sasa unasaidia ule Muswada uliopitishwa jana uweze kutekelezwa. Muswada huu utasimamia utekelezaji wake.

Mimi sikupata nafasi ya kujadili huo Muswada wa jana, lakini pia kwa sababu ni wakati wake wa kujiuliza, Waziri alijiuliza na ile Kamati Maalum ambayo wakati wa mchakato wa kuleta Muswada huu haikujiuliza kwamba ni vyema kama alivyosema Mheshimiwa Masumbuko Lamwai kwamba, sasa sheria za kazi inakuwa kama sheria moja. Lakini ni kwa nini leo mwaka 2004 tumeweka sheria hizi pamoja. Sheria zingine ni za zamani kweli kweli. Sheria ambazo zitafutwa sasa ambazo zimefutwa jana ni pamoja na *Employment Ordinance Cap.3, 1966.* Sheria nyingine inayofutwa ni *Regulations of Wages on Terms of Employment Ordinance Cap. 300, Security of Employment Cap. 574, Surveillance Allowance Cap. 487* na zingine za karibuni, *Industrial Courts Act 41 of 1967, Local Government Services Negotiating Machinery Act of 1983* na nyinginezo. Sheria zingine ni za zamani kweli, za wakati wa ukoloni, huu ni mwaka wa 2004. Kwa maoni yangu ni kama yai la kuku likitaka kuanguliwa yaani linaanguliwa baada ya miaka mingi mpaka kifaranga kinakuwa kimedumaa. Ni kwa nini tumefikia hali kama hii? Tutaongea baadaye madhara ambayo tumeyapata na pengine yataendelea hasa wakati huu wa utandawazi.

Kwa maoni yangu ni kwamba, mwelekeo wa uhusiano kati ya mfanyakazi na mwajiri haukuwa unaeleweka vizuri. Kwa sababu katika hali ya kawaida tunafahamu enzi zile za ujima, ubwanyenye, ubepari, sio siri kwamba mfanyakazi hana tofauti na chombo kingine cha kazi kama punda anayevuta plau au kama trekta. Pengine trekta likiharibiwa na mfanyakazi, mwajiri anaweza hata akamuua mfanyakazi kwa sababu trekta lina thamani zaidi kuliko mfanyakazi. Sasa hizo sheria zilivyo ni sheria za ukoloni, za mwaka 1937 au 1957 na kadhalika. Waziri alikiri kwamba, ilibaki vile vile isipokuwa kulikuwa na viraka vichache. Maana yake katika hali halisi ambapo sheria hizi tulizirithi kwa wenzetu ambao walikuwa na tabia za enzi zile za ubepari, ubwanyenye za kumwona mtumishi kama mali zilikuwepo mpaka uhuru na zipo mpaka leo na ndio tunazifuta. Sasa hata tukizifuta itatekeleza malengo ambayo tunayatarajia katika wakati huo wa utandawazi? Hapa ndipo inatufikisha aliyoyasema Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, je, sasa ndio tumetatua tatizo? Hii ni changamoto kubwa sana. Tumechelewa kwa sababu enzi hizi ni za haki za binadamu, usawa wa jinsia, demokrasia na usafi wa mazingira. Miaka mingi imepita karibu miaka 26 tangu tuwe na hizi *agenda* za dunia na lazima ingelikuwa sisi kama nchi, tungebadilisha sheria zetu kulingana na hali halisi ya dunia. Sasa tumechelewa kinachofanyika ni jitihada. Sasa jitihada hizi zinajibu?

Kwa maoni yangu nasema hazijibu katika mantiki ile ile aliyoiongelea Mheshimiwa Dr.Willbrod Slaa. Sasa kwenda kwa undani zaidi kwenye sheria hii ya

jana, tumeshapita tungependa kwenda huko lakini Waziri ajue kwamba ni changamoto katika kuiendesha sheria hii sasa. Kingine kilichonistua sana ni kuona katika mchakato wote wa Miswada halijajitokeza suala la sheria moja ambayo nayo ni ya zamani, ambayo inamwona mfanyakazi kama chombo, inaitwa *Workmen's Compensation Ordinance.* Katika maktaba na sehemu mbalimbali sijaona kama sheria ile imefutwa. Je ile *Task Force* haikuona hili? Kwa sababu hakuna lugha ya Kiswahili ya kuisemea ile sheria isipokuwa kwa kimombo naweza kusema ni *very primitive,* kwa sababu ni sheria muhimu ambapo mfanyakazi wakati wote anakuwa katika hatari ya kuumia kazini. Lakini anavyotendewa ni nafuu kuliko hata gari la kazi au baiskeli ya kazi au trekta. Mwanzo wake ni huko huko kwamba, mfanyakazi ni sawa na chombo cha mwajiri.

Sheria ile ina maeneo mawili. Eneo la kwanza, daktari ambaye atahakikisha kwamba mwajiri ameumia kazini, baadaye daktari ataeleza ni asilimia ngapi. Kwanza hii yenyewe ni dhana potofu sana. Asilimia ya mtu ni nini?. Ni aibu kwa sababu pengine haifiki hata laki. Kwa sababu asilimia ya mguu na malipo ambayo yanatajwa kwenye sheria ni aibu kutaja na ni aibu kwa dunia kuelewa. Kwanza, asilimia ya mguu ni nini kwa sababu asilimia100 ni kwamba, mfanyakazi amekufa. Sasa asilimia mbili ni nini? Miguu miwili ni asilimia ngapi? Katika sheria hii yote mimi sijaona hili. Mfanyakazi wa Tanzania yuko hatarini kila wakati, akiwa njiani kwenda kazini na kurudi nyumbani, akiwa kiwandani, ofisini na kadhalika.

Lakini ukielezwa sasa ukipata janga kazini, ukiathirika kazini, kipimo cha athari ile ni nini na malipo yake ni nini. Haina tofauti na yule mfanyakazi wa kiwanda cha nguo cha Uingereza mwaka wa 1850 au wale wakatamiwa kule Caribbean au wale waliokuwa wanalima karafuu hapa Unguja kwenye miaka 200 iliyopita. Hamna tofauti kwa sababu mguu wako pengine haufiki hata thamani ya Shilingi laki mbili, Shilingi laki mbili leo ina thamani gani?

Mheshimiwa Spika, hebu Waziri aniambie kama ni mimi sijafanya utafiti vizuri kuhusu sheria hii ya *Workman's Compensation Ordinance* au inafanyiwa kazi. Atueleze waziwazi kwa sababu ni eneo nyeti sana la kulifanyia kazi kwa sababu linahusu maisha. Tuache tu riziki ya kila siku, ajali kazini inahusu maisha ya kiumbe ambaye anaitwa mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kulieleza hili kwa kirefu zaidi, nadhani nimelielezea kwa uchungu na habari imefikia kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria nataka niongelee eneo moja tu ambalo Mheshimiwa Dr. Lamwai aliligusia. Mheshimiwa Dr. Lamwai amezungumzia kuhusu Mahakama ya Biashara, Mahakama ya Ardhi na sasa Mahakama ya Kazi. Yeye anapendekeza *Land Division* ya *High Court,* lakini mimi nafikiri ni *tribunal* tu kwa sababu hasa hapa ndiyo tunarudi kule kule nyuma tena, hivi haki itatendeka kwa mfanyakazi yeyote wa Tanzania kwa kutumia utaratibu wa mahakama hii? Kama mahakama yenyewe hii ndiyo ya mwanzo kabisa, ya usuluhishi *okay*. Mahakama hii ndiyo mwanzo halafu ndiyo unakata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa. Ukiangalia ibara ya 57, hakuna mahakama nyingine hapa katikati na ndiyo ya mwanzo na sijui

Majaji wa Mahakama hii wako wangapi. Nafikiri yuko mmoja tu na nchi kubwa hii yenye viwanda na migodi na nini una Jaji mmoja! Nafikiri mahakama ni mbili, ipo Arusha na Mwanza sasa imefunguliwa, sasa haki itapatikana wapi? Hakuna mahakama nyingine inaingilia masuala ya kazi, ibara ya 51 na 52. Sasa zinahusika.

Kwa hiyo, hii dhana ya Mahakama ya Ardhi, Mahakama ya Biashara na Mahakama ya Kazi nafikiri ingeangaliwa upya. Mwenzangu hata angeleta hoja sasa hivi isingesaidia sana kwa sababu suala hili ni zito zaidi kuliko inavyoonekana. Ardhi ni kitu gani kuliko riziki ya kila siku ya mfanyakazi? Kwa mfano, kwa suala la ardhi tunaanza na Baraza la Ardhi la Kijiji, hapa ndiyo haki inatafutwa. Unakata rufaa kwenye Baraza la Kata, unakata rufaa kwenye Baraza la Ardhi na Majengo ya Wilaya, Mkoa ndiyo unakuta huyu Jaji wa Mahakama wa Ardhi. Hapa kuna haki, basi kwa nini hii isiigwe kwa eneo nyeti kama la Wafanyakazi? Unaanza kule juu kabisa Mahakama ya Kazi ambayo ni Jaji na rufaa yake ni Mahakama ya rufaa hamna mahali pengine pa kwenda. Sijui hapa sasa hivi kuna kesi ngapi kwenye Mikoa yote ya Tanzania ambayo inasubiri kusikilizwa na mahakama hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kusema kwamba eneo hili ni eneo gumu na nyeti, ni eneo la mapambano muda wote katika historia ya binadamu. Sisi historia isituhukumu kwamba katika mapambano haya tuko sehemu ya ukandamizaji kwa kutunga sheria kama hizi. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba bado kuna kazi kubwa kama ile *taskforce* haijavunjwa iendelee kuangalia kwa undani zaidi sheria hii katika hali ya sasa ya utandawazi na maana ya kuwa na mahakama hii ambayo ina *level* mbili tu wakati Mahakama ya Ardhi ambayo siyo muhimu sana ina *level* zaidi ya sita. Halafu pia na lile eneo la ajali kazini na fidia. *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache na kwa vile kwa hatua tuliyonayo sasa hivi hatuwezi kufanya lolote nalazimika kuunga mkono Muswada. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa maoni yangu katika huu Muswada. Lakini nami naomba niungane na wazungumzaji waliotangulia kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mongella kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Ntagazwa kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa niende moja kwa moja kwa kuanzia kifungu cha 4(2). Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuhusu ile *composition* ya lile Baraza. Katika kile kifungu (b) ile ya kwanza inasema: *"Sixteen other members comprising the Permanent Secretary and three other members to represent the interest of the Government."* Hapo sina matatizo, lakini kinachonipa matatizo ni kile cha pili. *"Four members to represent the interest of employers."*

Mheshimiwa Spika, hapa ninaomba anisaidie, hawa *employers* ni wepi anaowazungumzia kwa sababu hapa hata Serikali na yenyewe inaajiri. Sasa kama utachukua watu kutoka Serikalini tayari pale ukichanganya wale wa kile kifungu cha

kwanza na cha pili utakuwa tayari na wawakilishi wengi zaidi katika upande wa *employers* kuliko wale wengine. Kama kutakuwa na suala la kupiga kura ina maana wale wote siku zote watakuwa wanaendelea kushinda. Naomba tu ufafanuzi, inawezekana labda mimi naelewa vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine naomba nizungumzie pale kuanzia ibara ya 45 kuhusu madaraka ya Maafisa kazi kukagua sehemu za kazi. Kifungu hiki kina lengo zuri sana la kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanapokuwa katika maeneo yao ya kazi wanakuwa katika maeneo ambayo ni ya salama na watafanya kazi bila matatizo na kuna uwezekano wa kuepusha ajali kwa hao wafanyakazi ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa amani. Lakini kama ambavyo alikuwa amezungumzia Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, hiki kifungu au hii idara ya Maafisa kazi na mimi naomba iimarishwe vizuri kwa sababu katika ziara ambazo tumepata kufanya katika Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara tumekuta katika maeneo mengi Wafanyakazi wanakuwa katika mazingira ambayo si salama, lakini vile vile hawapatiwi vifaa vya kuwakinga kwa ajili ya afya zao ili waweze kufanya kazi katika hali salama. Sasa, hawa wafanyakazi ukiongea nao unakuta wanakuwa na malalamiko yao na hii inaonyesha kwamba hawa Maafisa kazi wamekuwa hawakagui mara kwa mara, wangekuwa wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara haya matatizo yasingekuwa yanajitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki taifa letu limefungua milango katika utaratibu wa mambo ya kiuchumi na biashara kwamba, kutokana na utaratibu wa soko huria na utandawazi watu wamekuja kuwekeza shughuli zao za kiuchumi hapa kutoka maeneo mbalimbali. Unapozungumzia mwekezaji kuweka mazingira mazuri maana yake ni gharama na mara zote wafanyabiashara wanakuwa ni watu ambao wanaangalia faida.

Kwa hiyo, tusipoangalia huyu mfanyabiashara ambaye amekuja kuwekeza kwetu kwa lengo la kupata faida anaweza asikubali kuwekeza fedha zake nyingi katika kuangalia mazingira ya mfanyakazi badala yake anaweza akakwepa na matokeo yake wafanyakazi katika hivi viwanda wakawa katika hali ambayo siyo salama.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nimwunge mkono Mheshimiwa Lamwai kama alivyozungumza kwamba, hiki kitengo kiimarishwe na katika kuimarishwa sina uhakika kama kitengo kina wafanyakazi wa kutosha kwa sababu ninavyofahamu hawa wapo katika ngazi ya Wizara na wapo katika ngazi ya Mkoa, lakini katika ngazi ya Wilaya hawapo. Sasa, sina uhakika kama kwanza wapo wa kutosha.

Lakini pili, katika kuwawezesha kufanya kazi; je, nyenzo zote ambazo wanahitaji kama vyombo vya usafiri ama fedha kwa ajili ya kujikimu wanapokuwa safarini au katika shughuli zao wanapata za kutosha? Hili suala la kuwezesha wafanyakazi mara nyingine katika Wizara ama hata katika Mikoa huwa kuna baadhi ya idara huwa hazitazamwi vizuri. Unaweza ukakuta kuna idara nyingine zinawezeshwa vizuri zaidi na idara nyingine haziwezeshwi vizuri. Sasa, ili tuweze kutimiza lengo la huu Muswada katika kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanakuwa katika mazingira mazuri ya kufanyia kazi, naomba hiki kitengo kiangaliwe kwa maana ya kwamba kinapatiwa wafanyakazi wa kutosha na wanapatiwa nyenzo za kutosha. Lakini vile vile, pale wanapohitaji kuwa

na fedha kwa ajili ya kujikimu wanapokuwa safarini katika maeneo mbalimbali ya kazi waweze kupewa fedha za kutosha. *(Makofi)*

Eneo la mwisho ambalo nataka nizungumzie ni lile la adhabu, ambalo liko katika ukurasa wa 44. Ukisoma pale katika ukurasa wa 44(a) wanasema: "Kwa watu watakaokuwa wamefanya makosa watapata adhabu iliyozidi Shilingi milioni 5." Pale katika kile kifungu kidogo cha 3 pale chini wanasema: "Atapata adhabu isiyozidi Shilingi milioni 10."

Mheshimiwa Spika, katika hiki kifungu kwa maoni yangu naona hii fedha ni nyingi. Katika huu utaratibu wa kuitisha wawekezaji, wawekezaji siyo lazima wawe watu wa kutoka nje. Wawekezaji pia wanaweza wakawa ni Watanzania ambao mara nyingi tumekuwa tukiwahimiza na wao wajitokeze kuwekeza katika miradi mbalimbali, lakini kwa historia ambayo mimi naifahamu ya nchi hii ni kwamba, sisi huko nyuma hatukuwa na utaratibu wa shughuli za kibiashara za watu binafsi tulikuwa na Mashirika ya umma, ni hivi sasa tu ndiyo Watanzania wameanza kujitokeza mmoja mmoja kuweza kuwekeza katika shughuli za biashara na za kiuchumi. Sasa wengi wao utakuta si wazoefu sana, siyo watu wenye uwezo mkubwa sana. Ili hawa watu waweze na wao kushiriki katika hii dunia ya soko huria na utandawazi, nafikiri hapa wangefikiriwa kwa sababu siyo wote ambao wana uwezo wa kuweza kulipa hii adhabu kama ilivyopangwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kuna mahali katika huu Muswada pale tunapozungumzia suala la kuunda hii Kamati ya kuchunguza mambo ya mishahara, katika mambo wanayoangalia pamoja na mambo mengine kuangalia gharama ya maisha na kadhalika. Lakini wamezungumzia pia gharama za uendeshaji wa hizi shughuli za biashara kama ni ndogo, za kati ama kubwa. Vile vile, wameangalia kama hizi shughuli kama ni kiwanda ni kipya ama ni cha zamani. Ina maana kwamba katika kupanga mishahara pia wanajaribu kuangalia, pamoja na kuangalia gharama za kuishi hiyo peke yake haiwezi ikawa ni kigezo. Lakini vile vile, wanaangalia na hivi viwanda kama ni vikubwa ama vidogo, kwamba siyo kila kiwanda kilazimishwe kulipa kiasi fulani cha mshahara, ina maana kwamba hivi viwanda vimetazamwa. Sasa kama vimetazamwa, basi na hawa wafanyabiashara hasa Watanzania ambao nao wataingia katika uwekezaji katika hii dunia ya soko huria na wao wana tofauti, wapo wenye uwezo mdogo, wapo wenye uwezo wa kati na wapo wenye uwezo mkubwa. Kama tutapanga viwango vya adhabu vikubwa kama vinavyoonekana hapa kwa kweli wengine tutakuwa tunawakatisha tamaa na tutakuwa tumewanyima nafasi ya kuweza kushiriki katika suala zima la uwekezaji. Kwa hiyo, naomba kama Wizara inaweza ikaliangalia hilo iliangalie ili kuweza kutoa nafasi kwa hawa Watanzania na wao waweze wakafanya shughuli zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu wa leo. Niruhusu vile vile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana

na Michezo; Mheshimiwa Profesa Kapuya na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyofanya. Unajua siku zote mtu ukifanya kazi basi ndiyo unaweza ukasahihishwa, yule asiyefanya kazi basi huwezi kujua makosa yake na hivyo huwezi kumsahihisha au kumpa maelezo ya kurekebisha au kuboresha. Kwa hiyo, kama wanaona ushauri wetu labda ni mkali sana, ni kwa sababu ya kutaka wafanye vizuri ili kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Waziri alisema pengine mimi nasema sana kwa jazba kwa sababu nilikuwa upande wa wafanyakazi na yeye mwenzangu alikuwa mwakilishi wa TRAWU wa Kanda. Nadhani leo ukweli umejidhihirisha, Dr. Slaa hapa ameeleza kwa uchungu kabisa na yeye hakuwa mwakilishi wa Wafanyakazi. Ndugu yangu Mheshimiwa Philip Marmo ameeleza kwa uchungu kabisa hapo na yeye hakuwa huko, pamoja na wengine akina Mheshimiwa Ismail Iwvatta hapa wameeleza kwa uchungu na hawakuwa huko. Sasa hata ile hoja yake ya jana kwamba mimi nimesema sana wakati, yeye alikuwa mwakilishi wa Kanda, mimi nilikuwa *National Chairman*, kwa hiyo ni vitu viwili tofauti. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo niseme tu kwamba, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuleta *schedules of Amendment* hasa kifungu cha 102 kile ambacho tulikipigia kelele jana katika ile sheria nyingine, kwamba sasa kwenye marekebisho haya (e) pale inaonyesha kwamba: *"Chief Justice may exempt the Labour Court from their requirement of filing fees in any labour matter filed before it."* Ninampongeza sana kwa kusikia kilio chetu. *(Makofi)*

Lakini sasa ombi langu ni kwamba, ukishaiweka *'may'* kwa Wanasheria hawa ume-*dilute* ile kesi, kwa hiyo ile hoja bado iko *diluted*, kwa sababu *'may'* kwa tafsiri yangu mimi ambaye ni Mwanasheria wasiwasi anaweza akafanya *Chief Justice* na anaweza asilazimike kufanya. Lakini kutokana na umuhimu ambao tulikuwa tumeueleza jana, bado nimwombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na marekebisho haya aliyofanya yeye pamoja na mtaalam hapa Mwanasheria Mkuu kwa kweli waseme tu kwamba: *"The Chief Justice shall exempt...*" badala ya kutumia *'may'* kwa sababu *'may'* bado inampa nafasi yule *Chief Justice* atakaposhauriwa na wasaidizi wake au yeye mwenyewe kuona kwamba anaweza kufanya au asifanye.

Mheshimiwa Spika, jana nilisema ninataka nirudie kuwa moja ya tatizo sasa ni kwamba kesi za wafanyakazi zinachelewa sana katika mlolongo uliokuwepo zamani na nia ya sasa ni kurahisisha kiasi kwamba kesi hizi zikamilike mapema na kuzipa uzito unaostahili ndiyo maana kinaundwa kitengo au inaundwa idara kama walivyoshauri wenzangu hapa ya Mahakama Kuu.

Ombi langu katika hili ni kwamba, kwa sababu Mahakama Kuu ina Kanda mbalimbali na kesi hizi za wafanyakazi zimetapakaa Tanzania nzima, naomba nisisitize kwamba katika kupiga kasi ya kushughulikia kesi hizi niiombe sana Mahakama Kuu katika kesi zake za kawaida pia zishughulikie na kesi za wafanyakazi badala ya kutegemea tu Mahakama Kuu iliyoko Dar es Salaam kwa sababu wingi wa kesi hizi ni nyingi na kwa hiyo watakuwa wamefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka nizungumze ni kwamba, kimsingi tunafahamu kwamba masuala ya kazi ni masuala ya utatu kwa maana ya Serikali, Chama cha Waajiri *(ATE)* na Chama cha Wafanyakazi kwa sasa, kwa maana ya *TUCTA*. Hii ndiyo *composition* ya utatu uliopo sasa na maana yake ni kwamba jambo lolote ambalo linastahili kuamuliwa katika masuala ya kazi ni vizuri likazingatia sana utatu badala ya kuwahusisha watu wengine kwa sababu hawa ndiyo wadau wakuu.

Mheshimiwa Spika, sasa *composition* hii ya *Labour Economic and Social Council* ingawa imezingatia hayo, lakini tatizo langu ni kwamba Serikali *by implication* inakuwa na Wajumbe wanane kwa maana ya kwamba kile kifungu cha 4 (1)(b)(i) tayari yupo Katibu Mkuu na watu wake watatu, lakini vile vile kifungu 4 (b)(iv) wako watu wanne watakaochaguliwa na Waziri au na Serikali. Kwa vyovyote vile hawa lazima walinde *interest* ya Serikali na kwa maana hiyo Serikali itakuwa na Wajumbe wanane katika ile *council.* kama hivyo ndivyo, hata maamuzi yale utakuta kwamba Serikali itakuwa na *lion share.*

Mheshimiwa Spika, katika kile kifungu namba 9(4) liko suala la maamuzi yatakayofanywa na *council* hii na kama ilivyoelezwa pale katika wale wadau watatu, basi ingawa wanahitajiwa wanne mmoja akiwepo *quorum* imetimia na kwa ajili hiyo kikao kitafanyika na maamuzi yatafanyika kutokana na *majority* ya wale watu walioko pale. Sasa nimesema hapa kwamba Serikali ina watu wanane na waajiri wanne jumla kumi na mbili na wale wafanyakazi wanne wanakuwa kumi na sita. Nadhani upande mmoja umelemea. Mdau mmoja amekuwa na kauli kubwa zaidi kulikoni wenzake.

Mheshimiwa Spika, nilisema masuala ya kazi ni masuala ya utatu, nadhani hapa uamuzi utokane na wadau hawa watatu kwa sababu ndiyo wenye shughuli yao, siyo suala la *majority* la watu wale kumi na sita, hapana. Uamuzi utokane na wadau watatu, Serikali wale wanne na Wafanyakazi na *ATE* jumla kumi na mbili, kwa maana kila mdau mmoja atakuwa na kura yake moja. Kwa hiyo, pale ikibidi kupiga kura maana yake watu watatu wanapiga kura au wadau watatu wanapiga kura *two is to one.* Maana yake wale ambao watakuwa kwenye upande wa wawili basi watakuwa wameshinda kulikoni kuweka kwamba watu kumi na sita wapige kura, kwa vyovyote vile Serikali hapa itakuwa na *say* kubwa zaidi na kwa sababu *ATE* hapa nao mara nyingi wanaonekana kwamba wanaelemea huko tayari wako kumi na mbili, hawa wavuja jasho wangu mimi watakuwa hawana kitu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, ili kuondoa tatizo ambalo limeonekana lipo ni vizuri maadam suala hili ni suala la utatu na utatu unajulikana ni Serikali, wafanyakazi na waajiri, kura ya uamuzi ipigwe kuzingatia utatu na siyo suala la *majority* kama ambalo limeelezwa katika kifungu kile cha 94, kwa maana ya *constituency vote* ndicho kitu ambacho tunakizungumzia hapa kulikoni *majority* vinginevyo ile *argument* ya kusema kwamba mmoja akiwepo anatosha, nasema itakuwa haina msingi sana kwa sababu tayari upande mmoja umekuwa na matatizo kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza inatosha kulieleza hivyo. Lakini lingine ni katika ile *part four* ambapo inazungumzia ile habari ya *wage brood* au mishahara na kadhalika. Wenzangu wameeleza kiasi fulani, nataka niseme tu kwamba suala la mishahara sasa kwa kweli limefika mahali pagumu, pagumu *in the sense* kwamba karibu maeneo yote au maeneo mbalimbali kila eneo ukiliangalia unaona kwamba kuna umuhimu. Hii *classification* ambayo tumeanza kusema kwamba upande huu ni nyeti kwa hiyo wanahitaji mshahara mkubwa zaidi ili kusudi wafanye kazi nzuri zaidi unakuwa *defeated* kwa sababu unatumia *criteria* gani kusema kwamba hili ni nyeti na hili si nyeti?

Kwa mfano, *TRA* sasa wanapata mishahara mahsusi kwa maana kwamba ni kitengo nyeti ili kisiwe *tempted* au wafanyakazi wale wasiwe *tempted* kukaribisha visenti senti vingine ambavyo ni kinyume cha maadili. Kwa ajili hiyo wafanye kazi nzuri na wajitume katika kutafuta pesa. Napenda niwapongeze *TRA* kwa kweli kwa kazi nzuri ambayo wamefanya, mapato yetu siku zote hapa tumeambiwa kwamba yameongezeka, ni kwa sababu ya kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali na hasa *TRA.* Kwa hilo nawapongeza sana sina ubishi nalo. *(Makofi)*

Lakini napenda kusema kwamba, ukishasema *TRA* ni nyeti makundi mengine yanakuja nayo ni nyeti. Siku zote hapa tunazungumzia habari ya walimu ni nyeti, wako mbali, wanafanya kazi katika mazingira magumu hawa nao unawaondoaje katika fungu nyeti? Tunazungumzia siku zote hapa suala la madaktari kwamba hawa ni wataalam, miaka saba, miaka kumi mtu anasoma udaktari tu, leo unasemaje huyu siyo nyeti ukizingatia kwamba anapasua tumbo la Mheshimiwa Missanga hili kubwa namna hii mpaka likae sawa sawa na halafu aweze kutembea. Siyo kazi nyeti kweli hiyo! Unawaondoaje hawa kuwa nyeti? *(Kicheko/Makofi)*

Lakini vile vile wako wahasibu wanatutengenezea fedha zetu hapa ni nyeti na ndiyo maana leo Serikali yetu, Serikali kama Serikali ina wafanyakazi wenye *CPA* sijui kumi na ngapi *out of* chungu nzima ambao wanahitajiwa pale, wanakimbia kwa sababu mishahara yao ni duni. Hao nao ni nyeti. Pia wapo mainjinia.

Mheshimiwa Spika, nasema hili suala la mishahara kwa kuzingatia unyeti, nyeti ziko nyingi sana. Nadhani sasa wakati umefika Serikali ikae tena upya iangalie unyeti, iangalie namna ya kurekebisha mishahara ilingane na taaluma hizi vinginevyo tutaendelea kufundisha watu, kutumia fedha chungu nzima katika vyuo vikuu sijui Muhimbili, sijui wapi, wataalam hawa wote wanakimbia wanakwenda nchi za nje. Ni jambo zuri kwa sababu wenzetu wanapata maslahi mazuri zaidi, lakini kwa upande mwingine baada ya ku-*incur expenses* kubwa za kuwafundisha watu tunatarajia hawa Watanzania watusaidie. Sasa hawatusaidii wanakwenda kujisaidia wao badala ya kuwasaidia wale watu ambao wamewasomesha. Niombe sana katika hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe mfano mwingine. Sisi Kamati ya miundo mbinu tulikwenda pale kutembelea *agency* ya ndege za Serikali tukakuta kesi pale, wale watumishi marubani na mainjinia walikuwa na madai ya kusikitisha sana. Watumishi wale ambao wanamwendesha Rais na Mawaziri hawa wako *very low paid* ukilinganisha

na watumishi wa *Precision Air Services.* Hivi karibuni wamefanya *interview* waka-*recruit* mainjinia sita, baada ya miezi miwili wameondoka watano amebaki mmoja tu. Wote watano wamekwenda *Precision Air Service*. Kima anachopata yule injinia wa ndege ya Rais ni mara saba au nane chini ya kile ambacho anapata injinia wa *Precision Air Service.* Hivi kumwendesha Rais siyo kazi nyeti?

Mheshimiwa Spika, nyeti nyingine hiyo. Mkuu wa nchi, tumepigiana kelele hapa na wenzetu hawa wa Upinzani juu ya ndege ya Rais kwa sababu na kwa heshima ya Rais wetu tupate ndege na ndege inakuja halafu hawa wanaomwendesha Rais na chombo kile ambacho ni ghali kuliko vyote wanalipwa mshahara ambao ni mara saba au nane chini ya injinia wa *Precision Air Service,* hili nalo ni tatizo. Kwa hiyo, niombe sana kwamba Serikali iangalie mishahara ya watumishi wake wa Serikali hasa hii *classification* ya nyeti. Lakini napenda nitumie nafasi hii pia kuwa *agency* hii ya ndege ya Serikali nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ashirikiane na Mawaziri wote wanaohusika kwamba kweli ndege ya Rais ni ndege nyeti, watumishi wale ni lazima walipwe vizuri ili wawe *comfortable* na waweze kuwasafirisha viongozi wetu katika hali ya kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nilitaka niseme tu kwamba, katika ile *council* sijaona mahali popote kwamba inakutana mara ngapi. Sasa sijui kama itawekwa katika kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri atatunga baadaye, lakini nadhani ni vizuri ikajulikana hii *council* itakutana mara ngapi, itakutana mara ngapi, itakuwa na vikao vingapi. Vikao vikijulikana ni vingapi hata wale wanaokuja kuhudhuria vile vikao watakuwa wanajua, ratiba itakuwa imepangwa kwa hiyo hakutakuwa na sababu ya mtu kukosekana na akapiga kelele kwamba mimi mlininyima taarifana hata zile *acquisition* zingine zitapungua. Kwa hiyo, ningeomba vikao vya *council* vijulikane ni vingapi, ratiba ipangwe vizuri ili wote wanaohusika waweze kuhudhuria katika vikao vile. Kama katika Muswada huu hapa haiwezi kuwekwa, basi nimwombe sana Mheshimiwa Waziri katika kanuni ambazo atazitunga baadaye hilo nalo liweze kueleweka.

Mheshimiwa Spika, nasema leo itoshe, kwa sababu nikizungumza sana Mheshimiwa Waziri anasema nazungumza kwa sababu mimi ni mkereketwa wa Wafanyakazi. Lakini nimefurahi sana kwamba wakereketwa wako wengi, nadhani sasa atafuta ile kauli yake na sasa aone kwamba Wabunge wote hawa ni wakereketwa na kwa kweli tumekuja hapa kuwawakilisha wananchi pamoja na wananchi wengine wakulima wako pia wafanyakazi watakwenda kutuuliza: “Hivi ninyi siku hizi mnakwenda kutuondolea hata yale ambayo tayari tunayo?” Mimi hiyo ndiyo naogopa sana, yale ambayo wanayo tunawaondolea. Hivi tukienda tukiulizwa kule kwenye Majimbo yetu, ikiwa ni pamoja na Jimbo la Urambo, Jimbo la Mchinga na kadhalika, tutakwenda kujibu nini? Kwamba: “Kile ambacho tunacho mmetuondolea, hivi ninyi Wabunge tuliwatuma mkatutetee, mkatuongezee au mkatupunguzie?”

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupatiwa nafasi hii na mimi niweze kusema yale niliyoyaona katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuwa Rais wa Bunge letu la Afrika, pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuwa Rais wa Mazingira, kazi ambayo ni ngumu na ni *challenge* kwake hasa huko kwake anakotoka ambako wakimbizi wamemaliza misitu. Inawezekana ana kazi ngumu sana ya kulinda hadhi hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu mimi haunijii vizuri kwa sababu lengo ni kutetea na kuwawezesha wafanyakazi wapate haki na waweze kuishi vizuri zaidi. Sasa waishi vizuri zaidi kutoka wapi? Lazima wao wenyewe wachangie kazi yao wenyewe ndiyo izalishe. Pamoja na kwamba watu wanasema elimu, mimi nimesoma, umesoma elimu yako ina bei gani? Bei ni kazi unayozalisha kutokana na elimu yako. Kama elimu yako haileti mazao yoyote ya kuleta uchumi nchi hii, basi elimu yako ni bure tu wala haina maana yoyote. Kwa hiyo, hustahili hata kufikiriwa kuwa wewe ni mfanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tuwe tunakumbuka wakati wa ujamaa tulikuwa tunasema mtu asiyefanya kazi ni mnyonyaji, maneno haya yalikuwa ni mazito yalikuwa yanachokoza mioyo ya watu na watu walikuwa wanajituma ili wasionekane wanyonyaji, ndiyo chambo cha kuonekana ni wanyonyaji na wanadhalilisha uchumi wa nchi. Hatukuwa na matatizo ya watu kutokuzalisha, hatukuwa na matatizo ya machinga kujaa Dar es Salaam na kubeba maduka mabegani. Watu walikuwa wanafanya kazi, lakini sheria hii ukichukuekifungu kile pale namba 5 tunaanzisha *council, council* itashauri juu ya uchumi upi na wataupata wapi uchumi huo, watalinganisha na nini? *(Makofi)*

Mimi nadhani hapa sheria ni vizuri ikaeleza vizuri ili tusije tukawa tunaunda tu sheria za kuongeza taasisi za upande wa Serikali, ambao watu wanalipwa mshahara unaotokana na nguvu za wakulima maskini vijijini wananeemeka bila sababu yoyote. Tunaongeza hapa Mkurugenzi, taasisi, watu Kamati zote hizi zinategemea ziwe katika msululu wa kulipwa mishahara na marupurupu ya utaratibu wa Serikali. Lakini si utaratibu wa uzalishaji. Mfanyakazi lazima azalishe ndipo alete tija. Tumekwishafuta sheria ya nguvu kazi sasa tunampima vipi mfanyakazi? Leo nguvu kazi tumeondoa mfanyakazi anazembea, hafanyi kazi inavyotakiwa, mnafikiria kumwongezea marupurupu kima cha chini, kima cha chini kitoke wapi? Lazima mambo haya tuwe tunajiuliza na tunaangalia tunakwenda wapi? Tumeunda taasisi ya tija, hivi taasisi ya tija inafanya nini? Juzi tumewaita kwenye kikao wamesema mbona ilikwishakufa haipo. Sasa vitu vya namna hii tusipoangalia tutajikuta tunaunda sheria zinakwenda mwishowe tunakuja kufanya tena *amendment* ambazo hazitusaidii tunakokwenda kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaona tatizo lingine wawekezaji hawatakubali na utaratibu huu wa kuunda *council* ya kutetea wafanyakazi katika kiwanda chake alichoanzisha. Mwekezaji anaanzisha kiwanda ili apate faida, kama hutaki mwekezaji achana naye atakwenda sehemu nyingine.

Wewe unakwenda kusimamia watu hawazalishi pale kiwandani unataka mshahara kima cha chini kipande, kipande kutoka wapi wakati hajapata faida? Mimi nadhani iko haja hapa ya kuonyesha kwamba hii *council* isimamie wafanyakazi ambao watalipwa haki ya uzalishaji wao. Si hivyo tu hata katika Serikali. Nenda hata leo pamoja na sheria zote hizi unakuta ofisini hakuna watu na wanadai kila mwisho wa mwezi mishahara, siku ya mshahara ndiyo wa kwanza kufika asubuhi kudai mishahara, tunafanyaje? Hivi kweli tutapata tija, hivi kweli Serikali itaongeza uchumi wa kuwalipa vizuri zaidi hawa watu? Tutawalipa vizuri zaidi kutoka wapi? Tunazidi kuumiza tu wananchi na wanakata tamaa hata hakuna maendeleo, viwanda vyote vinakufa kwa sababu utekelezaji na ufanyaji kazi haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hapa *council* hizi ziwasimamie wale wanaotakiwa katika kazi, walioajiriwa wawe kweli ni wenye kujibu hoja ya tija ya kazi yao. Wale ndiyo wasimamiwe na wale ndiyo waungwe mkono na Serikali ndiyo iwape nguvu hawa. Lakini siyo kijumla jumla tu. Tumetumbukiza watu humo na wengine basi ndiyo wanajidai wanapata faida tu bila jasho kutumika na kuna watu hata sasa wanasema mshahara mimi nitapata tu, mimi niko kwenye *pension,* hata nikiacha kazi nitapata *pension*. Sasa hiyo *pension* imezalishwa na nani? Tutaleta misingi hii sasa ni utandawazi na utandawazi ni watu kunyonywa sasa kiuchumi *(neocolonialism)* tutanyonyana kiuchumi kama hatuzalishi. Huwezi ukategemea mtu akuletee kitu wewe ufaidike tu, lazima uzalishe uonyeshe na wewe unajaza pale alipofikia ili faida ile ndiyo tufikirie kuiwekeza katika mgawanyo wa mfanyakazi na yule mwekezaji hapo tutakwenda sawa. Lakini siyo kuegemea unakwenda kusuluhisha halafu unasema ana haki, haki gani? Tumeunda vitu hivi na taasisi nyingi tunaunda mahakama mpaka leo kesi nyingi sana ziko mahakama hazijaamuliwa na watu mnataka walipwe nusu mshahara, watalipwa mpaka lini? Nani anayezalisha huku? *(Makofi)*

Tusipoangalia tutajenga urasimu ambao utatuletea matatizo huko tunakokwenda hatutaweza kufanikisha hata kidogo na kuleta uchumi tunaoutegemea. Sasa tunajenga tabaka la watu kutegemea kula na kuishi bila kufanya kazi, hii ni hatari tunakokwenda huko. Hizi tume tunazozijaza ni hatari sana, zinaweza kutuletea matatizo na misululu ya kufuatia mtu apate haki yake hapa haiko, mtu kama kazi yake ameifanya pale, hivi kwa nini aende kwenye tume hata yule aliyemwajiri ataona aibu atampa tu haki yake.

Huu utaratibu wa kupandisha mishahara Serikali bila kuangalia uzalishaji na kadhalika nayo hii inawafanya hata wazalishaji wanaotoa nguvu zao wakate tamaa kuzalisha. Ni lazima tuangalie hili suala kwamba sisi sote wakulima na wafugaji wote tunafanya kazi ya kuongeza uchumi katika nchi ndipo tunaweza tukajifunza na tukaona maana ya kuongeza uchumi wetu. Tusiegemee kutetea tu kuliko kusimamia kazi. Hizi *council* zote na tume hizi zitetee kazi, uchumi ukipatikana nani atakayenyimwa haki yake, nani atakayeonewa? Lakini kama hakuna uchumi mzuri hata tungetetea, tunatetea umaskini tu na tutakufa maskini katika dunia hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, migogoro inayosuluhishwa isisuluhishwe kwa kuanza kuuliza maswali, isuluhishwe kwa kuona nani aliyeleta sababu, siyo masuala ya kuzungumza tena ahaa! sijui nani alianza, kama mtu hakuwepo kwenye kazi au kafanya uzembe ya

nini kupoteza muda kupeleka tume na posho za watu na kula watu pale? Ndiyo tunaofilisi nchi hii. Yule mtu asiyefanya kazi pale abanwe na kanuni waacheni wafanyakazi nawaambieni watafanya kazi.

Mwalimu Marehemu Baba wa Taifa alisema kiwanda kikifa na ninyi mmekufa. Sasa watu hawa wanabaki si ndiyo maana watu wanadai sasa tupewe mkono wa kheri, mkono wa heri wakati mmefilisi kiwanda, mkono wa heri utoke wapi? Watu mnataka muweke tume za kutetea watu waliofilisi wapate mkono wa heri uko wapi? Mnataka kutudhulumu bure tu nchi hii tufe maskini haiwezekani kufanikiwa. Mambo haya mjaribu kuyaona na kuyaangalia ili tuweze kufanya vitu ambavyo vitatuletea maana na faida na kuendelea hali ya kupambana na utandawazi katika dunia hii. Leo hii hao wafanyakazi wetu kama tutawachukulia hivi hatutafika. *(Makofi/Kicheko)*

Mtu mmoja wa Kenya aliniambia kwa kweli katika umoja wetu wa Afrika Mashariki hatuwezi kuajiri dreva kutoka Tanzania, nikamwuliza kwa nini? Akasema dreva wa Tanzania anamchukua *boss* wake Waziri pale anafika anasimama, Waziri anafungua mlango anachukua begi lake anakwenda kwenye mkutano, akishatoka anateremsha kiti analala usingizi. Waziri akija huko au kiongozi wake ndipo anashtuka akimgongea dirishani anapandisha kiti ndiyo anaanza kushika usukani.

Sasa hawa watu muwatetee kweli na tume na *council* ziende hapo watu wa namna hii? Kwanza hata muungano huo hatutapata kazi Watanzania. Inaonekana sisi tunafanya mambo ya kuishi kwa ulaghai laghai tu kwa ujanja ujanja tu. Hatutakwenda mahali popote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kweli hii sheria kwa kuwa imeletwa hapa sasa hatuwezi kuirudisha tuwatake watu hawa waende waiangalie zaidi, tuiunge mkono kwa kuwa imefika na ndipo walipofikia hapo, pengine ndiyo upeo wetu ulipofikia, sasa waanze kutafuta wapi sasa twende hatua nyingine kujikomboa na kujiokoa. *(/Kicheko/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edson Halinga ndiyo msemaji wa mwisho kwa mujibu ya orodha ya walioomba kuchangia na nilimweka mwisho kwa makusudi. Kwa kawaida yetu huwa tunawapa Mawaziri nafasi ya kutafakari haya yaliyochangiwa humu ndani kabla ya kujibu na wawasiliane na watalaam wao kupata majibu yenye uhakika.

Kwa ajili hiyo, nimeshamwarifu Mheshimiwa Waziri mtoa hoja kwamba atahitimisha hoja yake saa kumi na moja jioni, ili apate muda wa kujiandaa. Kwa ajili hiyo basi nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. *(Makofi/Kicheko)*

*(Saa 06.12 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii moja kwa moja, lakini ninaomba yafuatayo yaangaliwe:-

(i) S.7(1)(g) isomeke, *is convicted of a (criminal) an offence* na kuishia hapo hapo tu. Ikibidi basi iendelee kuwa and *sentenced to imprisonment with or without an option of fine.*

(ii) S.9(2) isomeke, *The Chairperson shall preside over all meetings of the Council* bila kuweka maneno *at which the Chairperson is present.*

(iii) S.9(b) isomeke, *in case of a tied vote, the Chairperson of the meeting shall have a casting vote.*

(iv) S.10(b) neno, *may libadilishwe kuwa shall.* Ahsante.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Muswada husika kama ifuatavyo:-

Muswada unaeleza kuwa kutakuwa na ulipaji wa fedha katika kuandikisha kesi na gharama zinginezo kama kipengele hicho chafaa kirekebishwe kama si kufutwa kabisa. Ukurasa 69 Ibara 15(1)(b) naungana na Waheshimiwa wenzangu kuwa kipengele hicho kiwe *the employee's place of domicile.* Pia ukurasa 108 Ibara 72(2)(d) inayozungumzia suala la kuwa *accounts* tofauti kati ya michango ya wanachama wenye kadi na wale wasio na kadi katika chama cha wafanyakazi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili likitekelezwa kama Muswada unavyopendekeza, linaweza kudhoofisha vyama vya wafanyakazi na hii ni kuingilia mno utendaji ndani ya vyama. Nashauri kwamba haya yaachiwe vyama na taratibu za fedha zinavyowahitaji kufanya, si vema kuleta mabadiliko ambayo yanaweza kuleta matatizo. Baada ya kuandika haya naendelea kuunga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Napenda nianze na Mheshimiwa Haroub Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yote ya Kamati yamezingatiwa katika Muswada huu na kwa ufafanuzi suala la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi litawekwa bayana katika muundo wa Wizara na kwa sababu hiyo hatutauona muundo huo ndani ya Muswada. Naomba nimshukuru vile vile na kumpongeza Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii kwa mchango

mkubwa ambao amekuwa akitupatia ndani ya Kamati lakini hata katika kipindi cha Bunge.

Aidha, kuhusu kifungu cha 31(5) ambapo alikuwa ametoa ushauri juu ya Waziri kumwondoa Mjumbe wa Kamati ya huduma muhimu *essential services.* Sababu za kumwondoa Mjumbe huyo zimeorodheshwa vizuri katika kifungu cha 31 alichokitaja ibara ndogo ya (5)(a) mpaka (f). Kwa sababu hiyo hatuhitaji tena kuziorodhesha nyingine. Kwa sababu tunaamini zilizopo zinatosha.

Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa alitaka utandawazi usifikie mahali kuvuruga hata maslahi ya wafanyakazi wetu na wananchi kwa ujumla. Sisi tunalifahamu tatizo hilo la utandawazi katika sekta binafsi kwamba siku zote hutafuta nafasi ya kumtoa kafara mfanyakazi ili aweze kupata faida yake na ndiyo maana ya Muswada huu umezingatia sana haki, lakini vile vile na wajibu wa wafanyakazi. Katika kifungu cha 35 pia alikuwa amezungumzia kwa uchungu sana juu ya kupishana kwa mishahara kisekta. Nataka nimhakikishie yeye pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba Bodi hii inayoundwa hapa yaani *Wage Board* kazi yake kubwa kama ilivyoainishwa katika kifungu cha *36 sub-section 1 and 2* kazi yake kubwa itakuwa ni hiyo kuhakikisha hali ya mishahara ya kisekta inawekwa vizuri na kifungu cha 4 alitakasifa za akipata Mwenyekiti, ziwe bayana asije akachukuliwa tu mtu ambaye hana uwezo.

Hili Mheshimiwa Naibu Spika, tumelizingatia na katika mabadiliko ambayo yataainisha pale kwenye 4(1)(a) itaongezwa isomeke *a Chairperson with expertise in labour or economics and social policy formulation who shall not be* na kuendelea. Kwa hivyo tumezingatia ushauri wake. Lakini alisema kwamba Waziri anapaswa kushirikisha wadau wakati anafanya uteuzi wa Wajumbe. Hilo tayari limo katika kifungu cha 4(a) na (c) na katika kifungu cha 4(3). Alitaka Baraza liwe na Bajeti yake, lakini hiyo bajeti haijaainishwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza litapata bajeti yake kupitia Serikalini. Lakini alitaka vile vile kuwe na bajeti ya Kamisheni ambayo haitaathiri uhuru wa Kamisheni kutokana na michango ya wafadhili. Nalo hili liko bayana katika kifungu cha 23(1)(b) ambako uhuru wa Kamisheni umewekwa wazi wazi na pia Kamisheni hii kwa mujibu wa kifungu hiki inawajibika moja kwa moja kwenye Bunge hili Tukufu kuhusu mapato na matumizi yake, kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 23(ii).

Alizungumzia vile vile juu ya kifungu cha 16(b) kwamba hawa Makamishna sita wanapoteuliwa basi vyama vya wafanyakazi vihusishwe. Kwa kweli Muswada huu umezingatia hilo na ndiyo maana kifungu hicho cha 16(b) kifungu kidogo (iii)(c) na (d) zinaainisha jinsi wafanyakazi na waajiri watakavyohusishwa katika kupendekeza majina ya makamishna hao.

Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kwanza tunamshukuru sana kwa mchango wake na katika kifungu cha 20(4) na kifungu cha 50. Nataka tumhakikishie kwamba tumezizingatia, isipokuwa katika kifungu cha 50(2) kimebakia kama kilivyo sasa kwa

sababu moja, pale (a) kifungu kinaongelea uteuzi wa Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo. Kukitoa kabisa tunapata tena tatizo la namna ya kumpata huyu Jaji Mfawidhi.

Lakini (b) kinazungumzia uteuzi wa Majaji wengine kulingana na kupanuka kwa shughuli za Mahakama kama tunavyojua nchi yetu ni kubwa kwa hiyo tungependa Kanda za Mahakama Kuu nazo, ifikie wakati ziweze kufanya kazi hizo hizo. Tukiondosha kabisa fungu la pili, maana yake uteuzi huu nao unakwama. Lakini na (c) kimeongelea kuhusu Washauri wa Mahakama. Hiyo ikiondoshwa, Washauri hawa nao ambao wanawakilisha maslahi ya Wadau watakuwa wamekosekana. Hofu yetu kuu ni hiyo kwamba tunaweza tukafanya Mahakama katika ngazi za Kanda kule zikashindwa kusaidia katika hili ambalo tunaamini litasaidia kuharakisha kesi.

Kifungu cha 45 alizungumzia juu ya kuimarisha ukaguzi, ili kupunguza ajali zisizo za lazima katika sehemu za kazi. Serikali ilikwisha kulitambua hili na ndiyo maana hivi sasa tunaendelea kushirikia na *ILO* na *DANIDA* katika kuimarisha uwezo wa wakaguzi na wasimamizi yaani *Capacity Building.* Lakini alitoa ombi vile vile kwamba kipindi hiki cha mpito cha utekelezaji wa Sheria hii mpya kisiwe kirefu mno na kuliweka li-*vacuum* likubwa lisilo na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelizingatia ombi hili na tunapenda kulihakikishia Bunge lako kwamba kwa vile vituo ambavyo sasa vipo vitaanza mara moja utekelezaji wa sheria hii mara itakapopitishwa.

Mheshimiwa Philip Marmo, alizungumza kwa uchungu sana. Hivi kwa nini mabadiliko haya yanafanyika sasa na isiwe pale mwanzo. Kwa kweli mabadiliko haya yalianza wengine hatujaingia Bungeni. Kumbukumbu zinaonyesha kwamba ilipofikia mwezi Mei, mwaka 1986 Wizara ya Sheria iliagiza Tume ya Kurekebisha Sheria *(Law Reform Commission)* ufanywe utafiti na kutoa mapendekezo ya Sheria za kazi. Tume hii ilifanya kazi zake na ilikamilisha kazi zake mwaka 2000. Na Waziri wa Kazi aliteua Tume Maalum chini ya Mheshimiwa Jaji George John Mrosso, mwaka 2001 na Muswada tunaoujadili leo hapa ni matokeo ya Tume hiyo.

Kwa hivyo hili jambo halikuanza juzi au jana kwa sababu labda ya shinikizo la utandawazi na wawekezaji. Ni jambo ambalo limeanza huko nyuma toka mwaka 1986. Vile vile aliuliza swali, hivi Muswada huu, kweli tunajibu matatizo ya wafanyakazi wetu? Bahati mbaya kabla hatujajibu mwenyewe akajibu hapana! Lakini sisi tunaamini kwamba Muswada unajibu matatizo kwa sababu moja, wadau wote kwa maana ya wafanyakazi na waajiri wameshiriki katika kuuandaa Muswada huu.

Lakini pili, Wizara ilitoa nafasi kwa Wataalam na wananchi wote kutoa maoni yao na kuwasilisha kwenye Tume hii. Tatu, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii nayo imeshiriki katika maandalizi haya. Lakini na mtu mmoja mmoja na leo Mheshimiwa Dr. Slaa hapa alituhakikishia kwamba hata yeye alialikwa kwenye Semina iliyofanyika kule Morogoro.

Lakini Mheshimiwa Marmo alitaka vile vile *essential services* zinazotajwa humu ziainishwe wazi na kweli zimeainishwa ukiangalia kwenye kifungu cha 77(2) cha Sheria ya ajira na mahusiano kazini ambayo tuliipitisha jana tu. Mambo haya yote yameainishwa bayana kabisa. Pia ni kazi ya Kamati hii kuainisha huduma zingine muhimu ambazo hapa leo hazipo. Kuongeza au kupunguza kulingana na hali itakavyojitokeza. Maana hii sheria inahusu watu, na watu tunabadilika kutokana na mazingira yetu. Kwa hivyo hatutarajii kwamba itabaki hivyo hivyo tu ilivyo. Alitaka kuwepo na muda maalum wa kukamilisha tatizo la upangaji wa kima cha chini kwa hofu kwamba Kamati inaweza kumshauri Waziri halafu Waziri akaamua kukalia tu ule ushauri kwa kipindi kisichokuwa na mwisho.

Labda tueleze tu kwamba Kamati hii si ya kudumu. Waziri anaiteua Kamati hii anapoona ipo haja ya kupandisha kima cha mishahara. Kwa hivyo hofu ya Waziri kukalia ushauri huo haipo maana ameiunda hiyo Kamati ili imshauri. Lakini pili, Kamati iliyoteuliwa na Waziri inatakiwa ifanye uchunguzi wa kina kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa katika kifungu cha 37 hivyo si busara kuweka muda maalum namna nyingine vigezo hivi vitakuwa haviwezi kufanya kazi iliyokusudiwa.

La tatu, si kweli kwamba kima cha chini kilitangazwa zamani sana. Maana tunakumbuka kwamba kima cha chini kwa mara ya mwisho kilitangazwa mwaka 2002 mwaka juzi tu na leo ni mwaka 2004. Lakini akauliza tena kwa uchungu kwa nini hakuna *Work Man's Compensation.* Nafikiri tatizo hili limejitokeza tu kwa sababu Mheshimiwa jana hakuwepo hapa. Tulipokuwa tunatoa majibu tulieleza kwamba suala hili litashughulikiwa katika awamu ya pili ya marekebisho ya Sheria za Kazi. Lakini suala hili litaangaliwa pamoja na masuala ya hifadhi ya jamii na *employment contingencies.*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo siyo kwamba hili halipo humu. Halipo humu kwa sababu lipo kwenye eneo lake la *Phase Two.* Na kama tunavyofahamu sote mambo haya yanahusiana tena na mifuko yetu ya jamii mbalimbali. Juu ya suala la Mahakama ya Kazi kuwa chini ya Mahakama Kuu ikiwa na ngazi mbili tu tofauti na ilivyokuwa katika Mahakama ya Ardhi. Na hili nalo si sahihi kwa sababu Mahakama hii ina a ngazi mbili. Katika migogoro ngazi ya kwanza itakuwa ni usuluhishi. Ngazi ya pili itakuwa ni uamuzi. Ngazi ya tatu, ni Mahakama ya Kazi na baada ya hapo itakwenda Mahakama ya Rufaa. Hivyo tunazo ngazi za kutosha. Lakini la msingi hapa Muswada huu unalenga kuhakikisha kwamba migogoro kazini inamalizwa kwa njia ya usuluhishi ili kuokoa muda wa uzalishaji na kuleta mahusiano mazuri sehemu za kazi. Ndiyo maana hizi ngazi za chini tunaziona ni za msingi zaidi kuliko huko Mahakamani ili mambo yaishe hapa kwa haraka zaidi watu warejee kazini kwenda kufanya kazi ya kukuza uchumi wetu.

Ndugu yangu Ismail Iwvata, Ibara ya 45, Idara ya Kazi iimarishwe. Wafanyakazi hawatoshi na suala la vitendea kazi vile vile ni matatizo. Nafikiri wakati namjibu Mheshimiwa Dr. Slaa nilisema kwamba Wizara sasa hivi inajitahidi kujenga uwezo wa Kitengo hiki cha Ukaguzi kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani pamoja na *DANIDA.* Juu ya kifungu cha 64 kwamba faini kwa waajiri ni kubwa mno. Mamilioni yale makubwa kwa wawekezaji wadogo wa hapa nchini wanaweza kukata tamaa kwamba mimi nitaweza kulipa kiwango hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango hiki ni cha juu, n*ot exceeding.* Kwa hivyo, tunaamini kwamba kwa *prudence* ya Mahakama au ya Hakimu atatoza faini kulingana na hali ya shauri lenyewe lilivyo. Ndiyo maana *not exceeding* anaweza hata asitozwe faini. Hii inategemea busara za Mheshimiwa Hakimu. Dhana ya urekebishaji wa Sheria za Kazi siku zote ni kupunguza makosa ya jinai katika Sheria za Kazi. Na makosa yaliyopo tunayaona yanachangiwa sana na ukorofi na baadhi ya Waajiri na wafanyakazi pia. Kwa hivyo, zimewekwa sheria hizi ili kujaribu kuzuia ukorofi huu usirudishe nyuma dhamira yetu ya kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, ametaka marekebisho katika kifungu cha 50(8) ambayo ilitawanywa leo asubuhi. Neno *may* liondolewe liwekwe *shall.* Yule Jaji yule asiambiwe *may,* yule aambiwe *shall.* Kwa desturi si utaratibu wala si utamaduni wa uandishi wa sheria kutoa amri kwa mamlaka na hivyo kuinyima mamlaka hiyo wigo wa kutumia busara. Unapoweka may unampa nafasi huyu Jaji kutumia *discretion l*akini ukiweka *shall* unambana anakuwa anaangalia hapo tu. Sasa kisheria wanasema si utamaduni huu mzuri na uliozoeleka. Kuhusu Kanda za Mahakama Kuu zipewe mamlaka ya kusikiliza kesi za masuala ya kazi. Kifungu cha 50(2)(b) kinaruhusu kuteuliwa Majaji wa Mahakama ya Kazi. Kadri shughuli za Mahakama zitakavyokuwa zinapanuka. Na ndiyo maana tulivyomba Mheshimiwa Lamwai atukubalie kile kifungu namba 2 kibakie kwa sababu ya kutoa uwezo huo wa huko Mikoani kuendelea kufanya kazi hizi ambazo zimeainishwa katika Muswada huu.

Kifungu cha 4(1)(b)(i)-(iv) muundo wa *LESCO,* Mheshimiwa alikuwa na matatizo kwamba huu uteuzi wa Wajumbe wanne nje ya utatu unaonekana utakuwa unaegemea zaidi Serikalini ambapo ndiyo wameteuliwa kuliko upande wa Waajiri na wafanyakazi na hivyo kuifanya Serikali kuwakilishwa na watu wanane.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasi wasi huu sio wa lazima kuwepo kwa sababu uteuzi wa Wajumbe unakusudia kuleta utaalam katika Baraza hili. Hawa Wajumbe wanaoteuliwa na sifa zao kama zilivyoorodheshwa. Wanawekwa mle kuja kusaidia utaalaam Lakini vile vile mantiki haikubali kwamba eti mtaalam akiteuliwa na Serikali basi siku zote hulazimika kutekeleza majukumu kwa kufuata miongozo ya watu waliowateua. Tunao Majaji wanateuliwa na Rais. Lakini kesi ngapi Serikali tumeanguka, kama ingekuwa hofu hii ni ya kweli basi naamini kesi zote ambazo Serikali inapelekwa Mahakamani zingekuwa Serikali inashinda. Kwa hivyo hii ni hofu tu kama nilivyoizungumzia jana ile ya upya wa mambo yenyewe. Ninaamini yakianza kufanya kazi yakazoeleka hofu hii itakuwa inajiondosha yenyewe taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9(5) kupiga kura kwa utatu, kwamba hawa wanne walioteuliwa na Waziri wasipige kura. Waachiwe wenyewe wa utatu wapige kura. Sisi tunaona kwamba lengo na mwelekeo wa *ILO* ni kuboresha *social dialog* ambayo utatu ni sehemu ya *social dialog* ni kupanua wigo wa ushiriki ili watu waache kukaa mle ndani kila mtu akivutia ngozi kwake tukasahau na maslahi ya watu wengine pamoja na uchumi wetu kwa ujumla. Kwa hiyo, kwa kuwepo watu ambao ni *neutral* mle ndani kunasaidia sana kutupa changamoto ya kuacha kujiangalia sisi

wenyewe muda wote na kuyaacha mazingira yaliyotuzunguka kwa maslahi yetu wenyewe.

Kuhusu *Wage Boards* mimi nilizungumzia vizuri wakati natoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Dr. Slaa na Mheshimiwa Dr. Lamwai. Lakini Mheshimiwa alizungumzia habari ya nyeti vile vile kwamba huu unyeti wa *TRA, pilot* wa Rais naye hana unyeti? Walimu je? Madaktari wanaoweza kupasua matumbo yetu makubwa yakakaa sawasawa, huo nao sio unyeti? Kwa kweli na mimi nakubaliana na wewe kwamba nyeti ziko nyingi sana. Lakini kila nyeti nayo ina uzito wake , hivyo mimi nakubaliana na yeye juu ya viwango tofauti vilivyo kisekta na mimi nafikiri ni kazi ya *Wage Board.* Wataangalia nyeti gani inahitaji hifadhi zaidi ya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikao vya *LESCO* ni vingapi kwa mwaka. Kama nafikiri atakuwa ameuangalia Muswada sasa hivi kifungu cha 9(1)(a) kimeainisha kwamba vikao kwa mwaka basi visiwe chini ya vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo waliochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Margreth Mkanga, alitaka hizi shughuli za *LESCO* kiongezwe kifungu chenye kushughulikia watu wenye ulemavu. Sisi tunadhani kwamba na tunaamini kwamba shughuli zi zilizoainishwa chini ya kifungu cha 5(1)(a) zinawahusu pia watu wenye ulemavu kwa sababu hakiwabagui. Lakini vile vile ametaka uwakilishi wa watu wenye ulemavu katika *LESCO* kupitia kifungu cha 4(1)(d) kiongezwe kifungu chenye kuwahusu walemavu na wao wawe na nafasi yao ya kuwakilishwa mle ndani.

Serikali inadhani kwamba kifungu cha 4(1)(b)(i)-(iv) watu wenye ulemavu hawabaguliwi. Lakini Sheria iliyopitishwa jana ya ajira na mahusiano kazini katika kazi inazuia mtu kubaguliwa kwa sababu tu ya ulemavu wake kama inavyoonyesha kifungu cha 7(4)(i) na tukiendekeza hii tutafikia mahali kundi nyingine maalum zitajitokeza zinataka nafasi. Suala la *LESCO* ni suala la utaalam lakini ni suala la udau. Kuna la wafanyakazi, kuna kundi la Waajiri, kuna kundi la Serikali na kuna lile kundi la Wataalam. Sasa tukianza kuweka na makundi ya wenye ulemavu tena tutajikuta hatuna ukomo wa kuweka makundi ni makundi na makundi. Mimi nafikiri vyama vya wafayakazi, vya Waajiri, Serikali inatambua kwamba kama mtu ana sifa, anastahili kuingia kwenye Kamati hizi bila kujali kama yeye ni mlemavu au mtu aliyekamilika kwa viungo vyake. Mheshimiwa Frank Michael Mussati, yeye alitaka kufanyike mabadiliko kwa mfano kile kifungu cha 7(1)(g). Huyu mtu anayetaka kuondoshwa kwenye Kamati, ile sentensi iishie tu *is convicted on criminal offence* isiendelee yale mambo mengine.
"

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumeona kibakie, kwa sababu hata kama ile fine ndiyo hakulipa tuseme aliwekwa ndani kama inavyoonyesha, amefungwa. Huyu mtu akiwekwa ndani atahudhuriaje kwenye vikao hivi. Maana yake moja kwa moja huyu ameshaondoka ndiyo maana ya kifungu hiki. Kwa hiyo tunafikiria kibakie tu. Lakini vile vile kifungu cha 9(2) anataka isomeke *The Chairperson shall preside over* bila kuweka yale maneno at which the Chairperson is present sisi tunaogopa kwamba tukitoa maneno haya kutaingia ukiritimba kwamba kama Mwenyekiti hayupo basi kikao hakifanyiki.

Sasa tukifanya hivyo, ni hatari. Sasa tukaona kwamba kifungu hiki cha 9(3) kinawaruhusu Wajumbe kumchagua Mwenyekiti wa muda miongoni mwao kuongoza kikao hicho. Kwa hiyo tumeona kifungu hiki kibakie hivi hivi kilivyo, kikao kiendelee kufanyika na akataka vile vile kifungu cha 9(4) yaongezwe maneno yafuatayo: *in case of a tied vote the Chairperson of the meeting shall have a casting vote.*

Lakini hiki kifungu ndiyo kinavyosomeka hivyo. Kwa hivyo kama kinasomeka hivi kama alivyokiandika mwenyewe, maana *the man who is presiding and Chairperson au Chairman* tunaona maana ni ile ile. Kwa hivyo tumeamua kibakie kama kilivyo. Na cha 10(b) alitaka neno may libadilishwe kuwa shall.

Yule *Permanent Secretary,* anaweza kuchagua mtu kutoka ndani ya Wizara yake kuingia kwenye sekretarieti. Mheshimiwa nataka tubakize *shall.* Hofu yetu ni kwamba kama wakati wa kikao mtu competent hatakuwepo ndani ya Ofisi. Tuliweka neno *shall, Permanent Secretary* atalazimika kupeleka mtu *bogus* kabisa ambaye ni hatari kwa kikao kumbe angeweza kwenda hata mwenyewe. Kwa hiyo, tunafikiria neno may libakie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi kutoa maoni yangu juu ya hoja hii na naunga mkono asilimia mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kunipa nafasi ili niweze kujibu au kuendeleza majibu ya hoja ya Waheshimiwa Wabunge kama yalivyotolewa leo asubuhi kuhusu Muswada wetu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Haroub Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa mchango aliowasilisha na Kamati yake. Ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Mudhihir, kwa jinsi ambavyo ameweza kufafanua karibu sehemu kubwa ya hoja hizo ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge.

Vile vile naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa heshima zake ambazo wamezitoa toa leo bahati mbaya ameunga mkono hoja hii kwa sababu kwa kweli ni hoja ambayo inazingatia maslahi ya Taifa na yeye kama Mheshimiwa Mbunge anaweka mbele utaifa.

Baada ya kusema hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi. Kwanza Mheshimiwa Margreth Mkanga, pili, Mheshimiwa Frank Michael Mussati. Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kwa mdomo au kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Dr. Masumbuko R.M. Lamwai, Mheshimiwa Ismail J.R. Iwvatta, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Edson M. Halinga na Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir.

Kutokana na majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa hapa leo, ni dhahiri tumejitahidi kufafanua karibu hoja zote walizotoa Waheshimiwa Wabunge na naomba nirudie nikumbushe yale ambayo niliyasema jana. Miswada hii miwili inategemeana na imeletwa hapa ili kutuletea Sheria ambazo zitajibu hoja na matarajio ya mfumo mpya wa uchumi ambao kama Taifa tumeamua kuufuata. Kwa hiyo, Miswada inategemeana imeletwa kwa makusudi kabisa ili kujaribu kuendana na hali ya sasa na mfumo wa uchumi ambao tunaufuata kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ameonyesha kuwa suala la kuzirejea Sera na Sheria za Kazi vuguvugu lake lilianza zamani na mpaka ilipofika mwaka 1986 ndipo Serikali ilipoamua kuielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria ili wapendekeze mfumo muafaka. Kwa hiyo, ni historia hapa. Tume ilikamilisha kazi yake mwaka 2001 na mwaka huo huo mwezi wa 10 ndiyo tukaunda Kamati Maalum. Kuundwa kwa Kamati kulitokana na hali halisi ya mageuzi ya kiuchumi na kisiasa yanayoendelea nchini mwetu yakiwemo na masuala ya utandawazi. Ni kweli Tume iliundwa miaka kama kumi na kitu iliyopita kunako 1986. Kutokana na vuguvugu ambao ulikuwepo zamani.

Lakini walipowasilisha matokeo yao ilikuwa tayari kuna kasi nyingine ambayo tayari imeshaingia ya uchumi kubadilika, utandawazi umeshatukumba. Kwa hiyo ilibidi dhahiri basi tukae chini na tuunde Kamati Maalum ambayo inaitwa *Task Force* ili kuangalia jinsi ambavyo tunaweza tukaja na Sera na Sheria mpya ambazo zitalinda maslahi ya wafanyakazi na wakati huo huo ni kwamba nguvu za uzalishaji haziathiri.

Nayasema haya kuonyesha kuwa tumefika hapa tulipofika, siyo kwa sababu ya shinikizo la mtu au Taasisi yoyote. Huu mchakato wa mabadiliko na kama Taifa linaloishi lazima tuwe sehemu ya mchakato huu. Kutokana na mchakato huu, wawekezaji wa ndani na nje nchi sasa wamekuwa ndiyo injini kubwa ya uchumi wetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mageuzi haya ya uchumi yafanikiwe, ni muhimu kwa Bunge na Serikali yake kuyasimamia na kuyaratibu vizuri. Ni dhahiri katika dhana ya uchumi lazima kutakuwa na makundi ya wafanyakazi na waajiri. Ni muhimu kwa Bunge na Serikali kuonekana kwa vitendo kuwa kila kundi linaamini kuwa litapata haki yake iwe Bungeni, iwe Serikalini. Lugha ya kuendelea kudhani kuwa waajiri wote ni mashetani kwa sasa hivi imepitwa na wakati. Ni kazi ya Bunge hili kuona kuwa makundi yote mawili yanapata haki kuliko kujenga mazingira ya kuwakatisha tamaa waajiri na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilisema na narudia tena changamoto inayoweza hata kutishia amani ya nchi yetu ni ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Ni muhimu Waheshimiwa Wabunge tujenge mazingira ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi yetu ili ajira ziongezeke. Kuendelea kudhani kuwa Wazungu wanaokuja kuwekeza kutoka Afrika ya Kusini ni Makaburu sio sahihi hata kule kwao Afrika ya Kusini dhana

hii imekwishapitwa na wakati hawaitwi Makaburu tena. Tusisahau baadhi ya waajiri hawa na kwa kweli wengi wa waajiri hawa ni Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kama wawakilishi wa wananchi lazima turidhike kuwa sheria hizi zinawahakikishia wafanyakazi maslahi na haki zao. Tukirejea kwenye mchango wa Mheshimiwa Mwanri jana kuwa mfumo huu wa uchumi lengo lake kuu ni kuzalisha faida kibao yeye alisema *super profit* lakini tufanye hivyo tukikumbuka kuwa sisi hao hao ni wawakilishi wa waajiri. Nilipozungumza jana nilimkumbusha Mheshimiwa Missanga kuwa tusisukumwe sana na hisia za historia yetu au historia zetu katika Vyama vya Wafanyakazi. Nilisema hivyo kwa kufahamu kuwa wakati wa mimi na Mheshimiwa Missanga tulipokuwa viongozi ndani ya Vyama tuliamini katika kumtetea mfanyakazi hata kama ana kosa la dhahiri ilikuwa ni kazi yetu hiyo na hata leo vipo baadhi ya Vyama vya Michezo hasa vina Katiba kabisa kwamba wewe ubishe mpaka ufe. *(Makofi)*

Sasa hii ilikuwa ni katika Vyama vya Michezo lakini wakati huo tulipokuwa viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi hata kama mfanyakazi ana kosa dhahiri ilikuwa lazima wewe kiongozi usimame kidete kumtetea. Mtu alipata uongozi kutokana na uwezo wake wa kuwatetea wenye makosa na wasiokuwa na makosa. Ukiwa na uwezo zaidi uliweza kufikia nafasi ya juu ya uongozi kama Uwakilishi wa Kanda hivi na waliokuwa hodari zaidi waliweza kupata nafasi ya uongozi hata katika ngazi ya Taifa. Kwa sasa sisi ni Wabunge, tuongozwe na kilicho na maslahi kwa Taifa letu, ili kujenga uchumi na kulinda haki za wafanyakazi wanaowajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halinga amenisaidia sana asubuhi alipokuwa akichangia kukumbusha kwamba karne tuliyonayo hivi au zama tulizonazo hivi sasa mshauri anayewapenda wafanyakazi atawapa ushauri wa kubadili tabia ya kufanya kazi ili tuweze kuhimili ushindani ambao utatoka ndani na nje ya nchi yetu lakini vile vile utatoka katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, utatoka katika Jumuiya yetu ya *SADC,* huyo ndio mshauri mzuri. Kuendelea kuwapaka mafuta kudhani kuwa tutaendelea kuwalinda katika mazingira ya kutokuzalisha tutakuwa hatuwatakii mema wafanyakazi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, mimi narudia kusema kwamba ni muhimu tukajaribu kuwashawishi Waheshimiwa wafanyakazi wajue kwamba *times have changed,* mida imebadilika, wajizatiti katika kubadili tabia ya kufanya kazi, wajizatiti katika kujiongezea ujuzi ili waweze kukidhi matarajio ya ajira mpya ambazo zitaendelea kuzaliwa. Bila kufanya hivyo, wao wenyewe kazi walizonazo zitakuwa hatarini lakini vile vile tutakuwa tunajenga mazingira ambayo hatutaweza kuzalisha ajira kwa vijana wetu na hii nasema ni tishio kwa amani ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo lilikuwa limeulizwa hapa ni la *‘may’* kwenye *Court fee,* nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri hakuligusia. Hili la *‘may’*kwenye *Court fee* ni kwamba sisi tunafahamu kwamba Mahakama hii ya Kazi tumeihamisha kuipeleka kwenye Mahakama Kuu itakuwa *Division of the High the Court.* Huku ilipokuwa Mahakama ya Kazi chini ya Wizara ya Kazi ilifahamika kama

Mahakama ya wanyonge kwa sababu waliokuwa wakienda kwa kweli walikuwa ni watu ambao hali zao ni dhalili hawawezi kulipa ada au *Court fee.* Kwa kutambua hilo, ndio maana tumeweka kile kipengele cha *'may'* kumwezesha Mheshimiwa *Chief Justice* aweze kulifikiria hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nataka niseme hivi, Mahakama hii imehamia kwenda Mahakama Kuu, Mahakama Kuu wana utamaduni wao wa lugha na namna ambavyo unaweza kumu-*address Chief Justice*. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kabla sheria hii haijaanza kutumika itakuwa ni kazi ya Waziri anayesimamia masuala ya kazi kujenga hoja na kumpelekea *Chief Justice* ili kuweka wazi uwezo wa *constituency* tunayoitetea ya wafanyakazi ili *Chief Justice* kwa hekima zake aweze kuzingatia hoja hii ambayo itakuwa imejengwa na Waziri anayesimamia masuala ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Taasisi za Kazi wa Mwaka 2003**
***(The Labour Institutions Bill, 2003)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyofanya jana, huu pia ni mrefu kidogo tutapitisha sehemu kwa sehemu. Kwa hiyo, kila mmoja awe makini kuangalia hilo kwa kuzingatia vifungu vilivyoko kwenye kila sehemu ya muswada wenyewe.

Kif. 1
Kif. 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 3
Kif. 4
Kif. 5
Kif. 6
Kif. 7
Kif. 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 9

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 10
Kif. 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 12
Kif. 13
Kif. 14
Kif. 15
Kif. 16
Kif. 17
Kif. 18
Kif. 19

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 20

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 21
Kif. 22
Kif. 23
Kif. 24
Kif. 25
Kif. 26
Kif. 27
Kif. 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 29
Kif. 30

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 31

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 32
Kif. 33

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 34

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yake)*

Kif. 35

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 36
Kif. 37
Kif. 38
Kif. 39
Kif. 40
Kif. 41
Kif. 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 43
Kif. 44
Kif. 45
Kif. 46
Kif. 47
Kif. 48
Kif. 49

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 50
Kif. 51
Kif. 52
Kif. 53

Kif. 54
Kif. 55
Kif. 56
Kif. 57
Kif. 58

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa kukubali pendekezo la kubadilisha jina la ile Mahakama na naridhika na mapendekezo ya marekebisho yaliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna tatizo moja, lile neno ambalo limeondolewa la *Labour Court* linajirudia kwanza katika kichwa cha hicho kifungu sijaona kwenye *schedule* kama kimeondolewa kwa hiyo kichwa kinabaki *Labour Court.* Mimi nafikiri mabadiliko yangeanzia hapo kutoka kwenye hicho kichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pia neno *Labour Court* linaendelea kutumika katika vifungu vingine kwa mfano Kifungu cha 50(7)(b)(ii), Kifungu cha 51, Kifungu cha 52(1) na (2), Kifungu cha 53(2)(a), vifungu vyote hilo neno linaendelea kutumika mpaka kifungu cha 58. Sasa mimi nilikuwa nimependekeza kwa sababu amekubali kutumia hilo neno *Labour Division of the High Court* katika kile Kifungu cha 50 basi hayo mabadiliko yangekwenda kwenye vifungu vyote ili tuwe na neno moja *uniform* ambalo lingetumika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai alishaleta mapema kufuatana na utaratibu mengine yamechukuliwa na Waziri amekubaliana katika *amendment* yake lakini hili mnasemaje, kuna tatizo? Mheshimiwa *Attorney General!*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dr. Lamwai tulikuwa na mawasiliano ya maandishi asubuhi nusu ya ushauri wake, Serikali umeuzingatia. Lakini kwa hilo analolisema kuna tatizo moja, nianze na moja la msingi, tumekubali kufanya hayo marekebisho kwenye Kifungu cha 50(1) kinatoa ile dhana ya kuanzishwa kwa *A Labour Court* ndio maana tukasema tusifanye hivyo. Hiyo ni kwa sababu kwenye Kifungu cha 2 cha Muswada ambapo tunatoa tasfiri ya maneno ambayo yametumika katika Muswada huu katika ukurasa wa sita tulianza na neno *Labour Court means the Labour Division of the High Court established in accordance with the provisions of section 50.*

Sasa kwa vile ni kifupi tu cha maneno *Division of the High Court* ndio maana tukasema ili tusipate haya matatizo ya *cross reference* za kutafuta kila kifungu na kwa ile sheria ya jana ambayo Bunge lilipitisha tukasema ni afadhali tukabakiza hili neno *Labour Court* kwa sababu limepewa tasfiri ambayo ina maana ile ile ambayo tunaitaka kwamba Mahakama hii itakuwa ni sehemu ya Mahakama Kuu. Tukishaelewana hilo, sidhani kwamba hayo ambayo Mheshimiwa Dr. Lamwai anayetaka yatakuwa yanamsumbua mtumiaji wa sheria hii. Kwa hiyo, ili tusipate tatizo la kufanya marekebisho katika Muswada huu baadaye kurudi katika sheria ambayo jana Bunge lilipitisha, ninamwomba sana Mheshimiwa Dr. Lamwai akubali tuendelee kuyatumia maneno haya *Labour Court.*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri naridhika na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nilikuwa na hoja nyingine kuhusu lile pendekezo langu juu ya Kifungu cha 50(1). Kwa jinsi mabadiliko yalivyoletwa bado yanatumika yale maneno *there shall be established the Labour Division of the High Court.* Sasa ukisema *there shall be established* ina maana *actually* Bunge linasema hiyo Mahakama iundwe, na nani, hii sheria haisemi. Mimi nilikuwa nimependekeza katika mapendekezo yangu kwamba watumie *a positive statement* kwamba *it is hereby established* yaani ionekane ni Bunge limeiunda hiyo Mahakama iwepo *by operation* ya uamuzi wetu hapa maana yake jinsi ilivyowekwa inaonyesha kwamba ni mtu mwingine ataiunda sisi tunasema tu iundwe lakini *actually* tunaiunda sisi hiyo Mahakama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Dr. Lamwai ni ya uandishi wa sheria tu. Katika uandishi wa sheria unaposema *there shall be established,* ndio unaendelea kusema a *Labour Court* au *a Labour Division of the High Court* maana yake ni kwamba kwa sababu Muswada utakuwa umeweka ni nini *entry point* ya chombo hicho na hapa unaiona ni uteuzi wa Majaji. Sasa Majaji hawa tunajua wapo lakini kuna mwingine ambaye atawateua kwamba wewe nakupeleka kwenye *Division* hii ya *High Court.*

Pindi pale uteuzi utakapofanyika na chombo hicho ambacho kimetajwa kwa mujibu wa sheria ndio sasa kinachukuliwa kama ndio kimeanzishwa. Ndio maana nilikuwa nasema tumebakiza hii kwa sababu ndio uandishi wa sheria zote ambazo Bunge hili tumekuwa tunaleta Muswada hii kwa sura hiyo. Maana yake ndio hiyo kwamba pale ambapo sasa Mamlaka husika inapotekeleza majukumu yake chombo hicho ndio kinazaliwa. Lakini haimaanishi kwamba Bunge, maana Bunge ndio linatoa idhini hiyo kwamba kitakuwepo chombo hicho sasa utekelezaji wake ndio unaachiwa kwa maelekezo ambayo sheria hii inataka iwe.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 59
Kif. 60
Kif. 61
Kif. 62
Kif. 63

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kif. 64
Kif. 65
Kif. 66

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Taasisi za Kazi wa Mwaka 2003**
***(The Labour Institution Bill, 2003)***

*(Kusomwa mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na imeukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa kwamba Muswada wa Sheria ya Taasisi za Kazi wa Mwaka 2003 *(The Labour Institutions Bill, 2003)* kama ulivyobadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**Muswada wa Sheria ya Bidhaa za Maziwa wa Mwaka 2004**
***(The Dairy Industry Bill, 2004)***

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Dairy Industry Act, 2004* pamoja na marekebisho yake, sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unaleta mapendekezo ya sheria mpya itakayosimamia shughuli za sekta ndogo ya maziwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya maziwa hapa nchini imekuwa ikisimamiwa na sheria ya Maziwa *The Dairy Industry Act No.32, Cap.590* iliyotungwa mwaka 1965. Sheria hii ilianzisha Bodi ya Taifa ya Maziwa *(National Dairy Board)*. Sheria hiyo ilimpa Waziri mamlaka ya kuteua wajumbe wa Bodi ambao wengi walikuwa ni watumishi wa Serikali. Wajumbe hawa, wamekuwa wakiteuliwa kuanzia mwaka 1965 mpaka 1973. Kuanzia wakati huo hadi leo wajumbe wa Bodi hawajawahi kuteuliwa tena. Katika muda wote huo, shughuli za Bodi zilitekelezwa na mashirika tanzu ya Mamlaka ya Mifugo *(LIDA)* iliyoanzishwa mwaka 1974. Mashirika hayo ni pamoja na Kampuni ya Ng'ombe wa Maziwa *(DAFCO)* iliyopewa jukumu la kuendesha mashamba makubwa na

ya kati ya ng'ombe wa maziwa na *Tanzania Dairy Limited (TDL)* ambayo ilipewa jukumu la kuendesha viwanda vya kusindika maziwa. Mashirika haya mawili yalikwishavunjwa kwa hiyo kuna pengo ambalo linatakiwa kuzibwa kwa kuweka utaratibu mwingine wa kupata chombo cha kusimamia sekta hii ndogo ya maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya maziwa nchini inahusisha ng'ombe wa maziwa wanaokadiriwa kufikia 500,000 wanaofugwa ndani na ng'ombe wa asili wapatao milioni 17.2 wanaofugwa kwa mfumo huria. Katika kipindi cha mwaka 2003 ng'ombe hao walizalisha jumla ya lita bilioni 1.2 za maziwa. Kati ya maziwa hayo, lita milioni 400 zilizalishwa na ng'ombe wa kisasa na maziwa yaliyobaki yalitokana na ng'ombe wa asili. Karibu asilimia 80 ya maziwa yote yanayozalishwa hapa nchini hunywewa vijijini na kiasi cha maziwa kilichobaki hunywewa mijini. Kati ya maziwa yaliyozalishwa mwaka 2003 ni lita milioni 54 tu ndizo zilizosindikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya maziwa inakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo magonjwa wa mifugo, ukosafu mdogo wa mifugo iliyopo, uhaba wa vifaa vya kukusanyia, kuhifadhia na kusafirishia maziwa, uhaba na uchakavu wa miundo mbinu na soko dogo la ndani kutokana na unywaji mdogo wa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa uchumi wa soko, Serikali imeiachia sekta binafsi kutekeleza shughuli za uzalishaji kama kuendesha mashamba ya ng'ombe wa maziwa na viwanda vya kusindika maziwa. Aidha, sekta binafsi ndio inayoshughulika na shughuli za uingizaji na usambazaji wa maziwa na mazao yatokanayo na maziwa. Serikali imebaki na jukumu la kuandaa sera; kusimamia sheria na kuratibu maendeleo ya sekta ya maziwa. Sheria ya Maziwa iliyopo imepitwa na wakati na hivyo kusababisha ugumu katika kusimamia ipasavyo shughuli za sekta binafsi ambayo imekuwa ikipanuka kwa kasi siku hadi siku. Aidha, hali hii imesababisha uzalishaji, usindikaji biashara ya maziwa na mazao yake na usambazaji pembejeo za kuzalisha maziwa kukosa usimamizi madhubuti kisheria na hivyo kuathiri vibaya maendeleo ya sekta ndogo ya maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sekta ndogo ya maziwa kukosa usimamizi, wadau wamekuwa wakifanya juhudi za kuanzisha vikundi ili kuratibu shughuli zao kwa lengo la kuziboresha. Hivi sasa vipo vikundi vya wafugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa vipatavyo 1,637 na mitandao ipatayo 54 katika ngazi za Tarafa na Wilaya. Aidha, vipo vikundi mbalimbali vya Kitaifa vya wadau wa maziwa kama vile *Tanzania Milk Process Association, Tanzania Milk Producers Association, Tanzania Animal Feeds Manufacturer Association* na *Tanzania Goats Network.* Vikundi hivi vyote ni wadau muhimu katika uundaji wa uimarishaji wa Bodi ya Maziwa ambayo inategemewa kuundwa iwapo sheria hii itapitishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuandaa Muswada huu wadau mbalimbali walishirikishwa ikiwa ni pamoja na wafugaji wa asili, wafugaji wa kibiashara, wasindikaji, watoa huduma za mifugo na wasambazaji wa pembejeo za mifugo. Wadau hao wameshirikishwa kuanzia ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya hadi Taifa kwa njia ya mikutano, semina, warsha, makongamano na mbinu nyinginezo shirikishi. Aidha,

wadau wengine kama Wizara za Afya, Fedha, Viwanda na Biashara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kilimo na Chakula, Sheria na Katiba na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine walishirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya sekta ya mifugo inaelekeza ifuatavyo ninanukuu: "Ifikapo mwaka 2025 kuwe na sekta shirikishi ya mifugo na inayozingatia ufugaji wa kisasa, endelevu, inayoendeshwa kibiashara, yenye mifugo bora na yenye tija kubwa, itakayoinua maisha ya Mtanzania na kutoa ajira, kuzalisha malighafi kwa ajili ya usindikaji, kuongeza pato la Taifa na kuhifadhi mazingira". Dira hii inatilia maanani Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000. Ni mategemeo ya Wizara yangu kwamba sheria hii mpya itarahisisha kufikiwa kwa malengo na matarajio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, sheria mpya itaondoa mapungufu yaliyokuwepo kwenye sheria ya zamani na kufanya iwe ni kichocheo halisi cha ukuaji wa sekta ndogo ya maziwa na sekta ya mifugo kwa ujumla katika misingi ya uchumi wa soko. Mambo muhimu katika Muswada ni kama ifuatavyo. Kwanza ni kuanzishwa kwa Baraza Kuu la Wadau katika sekta ndogo ya maziwa. Pili, kuundwa kwa Bodi ya Maziwa. Tatu, usajili wa shughuli mbalimbali za maziwa chini ya sheria hii. Nne, kuanzishwa kwa mfuko chini ya sheria hii. Tano, Waziri kuweka kanuni na taratibu mbalimbali za kusimamia sekta ndogo ya maziwa na sita ni kuainisha makosa na adhabu mbalimbali chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mpangilio na mtiririko wa Muswada huu, naomba nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Ardhi na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa na Makamu wake Mheshimiwa Alhaj Shaweji kwa kuchambua Muswada huu na kukubali kuwa uletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nashukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hasa Idara yake ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa mchango wao mkubwa katika kuelezea dhana na vipengele mbalimbali kwa wajumbe wa Kamati. Mwisho, nawashukuru wataalam na watumishi wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa maandalizi ya awali ya Muswada huu na Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa msaada mkubwa alionipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa shukrani hizi, naomba nitoe kwa muhtasari mpangilio na maeneo muhimu ya Muswada huu. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu saba kama ifuatavyo. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wwakati vifungu vya 1-3 vinaelezea jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii na tasfiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika kwenye Muswada huu. Sehemu ya pili, vifungu 4 - 7, vinaelezea kuanzishwa kwa Baraza Kuu la mwaka la wadau wa sekta ndogo ya maziwa, wajumbe wake na mambo mengine mbalimbali yanayohusu mkutano mkuu wa wadau.

Sehemu ya tatu, vifungu 8 - 15 vinaelezea kuanzishwa kwa Bodi ya Maziwa, wajumbe wa Bodi, majukumu na mamlaka ya Bodi, muda wa wajumbe wa Bodi na taratibu za vikao vya Bodi. Aidha sehemu hii inafafanua mambo ya utawala wa Bodi,

ikiwa ni pamoja na uteuzi wa watumishi mbalimbali wa Bodi na kinga kwa wajumbe na watumishi wa Bodi wanapotekeleza majukumu yao chini ya sheria hii. Sehemu ya nne, vifungu 16 - 23 vinahusu usajili wa wazalishaji, watengenezaji na wauzaji wa maziwa na bidhaa za maziwa pamoja na wasambazaji wa zana au pembejeo Kif. 27zinazotumika kwenye fani hizo. Sehemu hii pia ina masharti yanayohusu uteuzi wa Msajili na majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano, vifungu vya 24 mpaka 25, sehemu hii inaainisha makosa na adhabu mbalimbali chini ya sheria inayopendekezwa. Sehemu ya sita ina vifungu vya 26 mpaka 31, inahusu uanzishwaji wa Mfuko wa uendeshaji wa sekta ndogo ya maziwa, majukumu ya mfuko huo, usimamizi wa mfuko na ukaguzi wa mahesabu ya mfuko. Sehemu ya saba, ina vifungu vya 32 mpaka 35 na inatoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya sekta kutengeneza kanuni na taratibu mbalimbali chini ya sheria hii pamoja na kufutwa kwa sheria ya sasa ya maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Muswada huu unapendekeza majedwali kwa ajili ya taratibu za wajumbe wa Baraza Kuu la Wadau na Wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi naomba kuleta maoni na mapendekezo na nafanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Na. 70(2) ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo naomba na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Kuchaguliwa kwake ni heshima kubwa kwa Taifa letu na Bunge letu.

Pia napenda niwapongeze Wabunge wa Bunge la Afrika kutoka Bunge la Tanzania na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki ambao kwa pamoja walishirikiana sana kuhakikisha kwamba Mheshimiwa Balozi Mongella anapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wajumbe waliupitia kwa makini sana Muswada huu tangu hatua za awali na tarehe 7 Aprili, 2004 Kamati ilikutana na wadau wa sekta hii ya maziwa ambao ni wazalishaji, wasindikaji, washauri na wataalam kwa pamoja na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ili kupata maoni kuhusu Muswada huu. Kamati ilifurahishwa kusikia kuwa Wizara iliwashirikisha wadau katika hatua zote katika Muswada huu na kwamba wao wenyewe wadau waliuona ni mzuri na kuukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu baada ya kuwasilikiza wadau pamoja na Mheshimiwa Waziri, iliketi tarehe 8 Aprili, 2004 na wajumbe wafuatao ndio waliohusika katika kuuchambua Muswada huu:-

Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Abdillah Namkulala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Edward Lowassa na Mheshimiwa Anthony Diallo kama wajumbe wa Kamati pamoja na ndugu Aggrey Nzowa ambaye ni Katibu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau ambao walifika mbele ya Kamati ni Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, wataalam toka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, *Tanzania Food and Drugs Authority,* Mratibu *ASCO Project Association,* Taasisi ya Chakula na Lishe, *Tanzania Milk Processors Association, Southern Highland Livestock Development Association,* Bodi ya Maziwa, Dr. A. G. Rwehumbiza, Dr. G. Mwakatundu na Profesa M. Kyoma, ambaye ni mshauri na wengineo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ingawa ulitakiwa uwe umeshaletwa miaka mingi iliyopita. Ni kweli kumekuwa na Sheria ya Maziwa ya Mwaka 1965 *(The Dairy Industry Act, 1965)* ambayo Mheshimiwa ameizungumza sasa hivi, lakini kutokana na kupitwa na wakati haikuweza kutimiza majukumu yake barabara.

Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa Bodi iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Maziwa ya mwaka 1965, ilifanya kazi zake hadi mwaka 1973. Baada ya hapo mashirika mawili yaani *Dairy Farming Company (DAFCO)* na *Tanzania Dairies Limited* yaliundwa ili kutekeleza majukumu ya Bodi hiyo na yalipovunjwa kukawa sasa kuna pengo haikujulikana sekta hii itashughulikiwa na nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi sana wanajihusisha na uzalishaji wa maziwa tofauti na miaka ya 1965 ambapo maziwa yaliyotumika hapa nchini yalitoka nje ya nchi na kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na viwanda vya kusindika maziwa vikubwa na vidogo. Hivyo Sheria hii ni muhimu kwa ustawi wa sekta ya maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umetoa majibu kwa mambo muhimu ya kuendeleza sekta ya maziwa ingawa wadau kwa upande wao nao walitoa mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, katika kifungu cha 9(b), wajumbe wa Bodi ya Maziwa Tanzania walipendekeza wawepo watatu badala ya wajumbe wawili hasa kwa sababu hao ndio wazalishaji, kwa hiyo, wangepaswa kuwa wengi kuliko wale wengine.

Pili, wadau waonyeshwe wazi kuwa wao ndio wachangiaji muhimu wa kuendesha Bodi hii kuliko inavyoelezwa kwenye kifungu cha 28(c).

Tatu, kwa vile sheria inalenga katika kuendeleza sekta ya maziwa walipendekeza jina la Bodi liwe *Tanzania Dairy Development Board* badala ya jina la sasa la *Tanzania Dairy Board* kama ilivyo katika kifungu cha nane.

Nne, kuwepo na mwakilishi toka Wizara ya Ushirika na Masoko kwenye Bodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wake Kamati inasisitiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kupata maziwa bora ni vema shughuli za ugani ziboreshwe. Hali ya ughani au *extension services* katika nchi hii ni duni sana. Tunapoingia katika uzalishaji wa maziwa wa soko huria ni vema huduma hii iboreshwe na iimarishwe. Sheria tuliyoipitisha hapa Bungeni mwaka 2003 ya *Veterinary* inaruhusu huduma ya ughani kutekelezwa na Serikali pamoja na sekta binafsi. Lakini inaonekana kuwa utekelezaji wake bado haujaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa katika baadhi ya maeneo hakuna majosho au hakuna dawa za kukogeshea mifugo. Pia bei ya dawa ni kubwa kiasi ambacho baadhi ya wakulima wanashindwa na hivyo mifugo ambayo haikuwekwa dawa inaweza ikazalisha maziwa yasiyofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, huduma za uzalishaji ziimarishwe na kudhibitiwa ili pawepo na mifugo yenye ubora unaotakiwa katika kuzalisha maziwa. Mheshimiwa Waziri alitueleza kuwa anaandaa sera ya uzalishaji *(National Breeding Policy)* na hatimaye kuwe na Sheria ya Uzalishaji. Tunadhani hiyo itakuwa ni hatua nzuri ili kuzuia uwezekano wa wafanyabiashara kuleta wanyama au mbegu ambazo hazifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba tu niwashukuru sana wewe mwenyewe, pamoja na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na wataalam wote na zaidi ya yote niwashukuru sana sana Wajumbe wa Kamati hii kwa jinsi walivyoshirikiana katika kuuchambua Muswada huu. Kwa vile haukuwa Muswada wenye matatizo makubwa kwa sababu wadau wenyewe waliukubali na Serikali ikakubali baadhi ya marekebisho na masahihisho Kamati iliamua kuupitisha na kuuleta hapa Bungeni kwa majadiliano kama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria *The Dairy Industry Bill* wa mwaka 2004. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(c) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Anthony Diallo, pamoja na watendaji wa Wizara hiyo kwa kuweza kuandaa na kuwasilisha Muswada huu ambao una lengo la kuiboresha sekta hii muhimu kwa manufaa ya wananchi na wafugaji kwa ujumla.

Aidha napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kwa maoni na nasaha zake zenye madhumuni ya kuweka mambo sawa ili kufikia lengo lililokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiitupia jicho Tanzania tutaona kwamba ni nchi iliyojaliwa kwa mifugo mingi kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika. Lakini pamoja na wingi wa mifugo yetu ukosefu wa huduma bora na miundombinu umeifanya sekta ya ufugaji nchini kushindwa kutoa mchango mkubwa katika kuinua hali ya maisha ya wafugaji walio wengi pamoja na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali kukuza mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa, bado unaendelea kuwa ni mdogo. Sekta ya maziwa ni miongoni mwa sekta mbalimbali zilizoathiriwa na mageuzi ya uchumi na utandawazi jambo ambalo linapelekea Serikali nayo kutunga sera mpya zinazoendana na mageuzi hayo mathalani *Free Market Economy.*

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Muswada huu ni hatua muhimu sana katika kuweka utaratibu wa kudhibiti, kuboresha na kuhamasisha uzalishaji, utengenezaji, utafutaji wa masoko na matumizi ya maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulielezwa hapo awali kwamba chimbuko la Muswada huu ni wadau wenyewe, wao ndio walioubuni na baadaye kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na kuukamilisha na kuweza kuwasilishwa hapa hii leo. Huo ni ujasiri mkubwa unaofaa kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wadau hawa kwa dhati kabisa kwa juhudi yao hiyo. Sisi tunaona huo ni mwanzo mzuri na tunatarajia baada ya Muswada huu kuwa sheria kamili basi utekelezaji wake utakuwa wa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yanaweza pia kupatikana kutokana na sababu kwamba katika utekelezaji wa sheria hii unatoa fursa ya kuwashirikisha wadau

wa sekta husika katika kuleta maendeleo ili kukidhi haja ya mabadiliko ya kiuchumi yanayotokea ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegusa mambo yote muhimu na kwamba tulipata muda wa kutosha wa kuupitia na kuujadili na kutoa mapendekezo yetu. Wizara kwa upande wake ilijitahidi kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na kwa hilo tunaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha hoja yangu naomba kutoa ushauri mdogo kwa Serikali. Ili sheria hii iwe ya manufaa zaidi na kuwavutia wawekezaji hapana budi Wizara iandae kanuni maridhawa zitakazoweza kuleta mvuto ili kuongeza idadi lakini pia na ufanisi katika uzalishaji wa maziwa.

Aidha, utaratibu uliobuniwa katika kifungu cha 17 wa kusajili wazalishaji, wasindikaji na wadau wengine uwe wazi, unaoeleweka na ambao hautaleta usumbufu kwa wadau wakati wa utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9(1) (j) kwenye uundwaji wa Bodi ya Maziwa kinasema na ninanukuu: *"One member from a Public University for Agriculture."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapendekeza baada ya neno *agriculture* yaongezwe maneno haya yafuatayo: *"or a Livestock Training Institute,"* na kwamba sasa isomeke: *"One member from a Public University for Agriculture or a Livestock Training Institute."*

Ushauri huu unatokana na sababu kwamba vyuo hivyo vya mifugo vipo karibu sana na wadau kwa njia ya kuwapatia Maafisa Ugani hasa Vijijini, lakini pia mara nyingi huandaa mafunzo mbalimbali kwa wadau wanaozalisha na kusindika maziwa, mahusiano yao ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naunga mkono hoja na tunawaomba Waheshimiwa Wabunge baada ya kuujadili Muswada huu waupitishe kwa kauli moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wasemaji wakuu kwa Muswada huu wamemalizika. Hapa ninao wachangiaji nane kwa ujumla wote nao nitawataja wote Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. Kwa hiyo, sidhani kama leo hii tunaweza kumaliza lakini tutakapofikia basi kesho tutaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, atafuatiwa na Mheshimiwa Talala Mbise.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya awali ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Moja kwa moja niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ninawaomba Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina sehemu ndogo tu ya kusisitiza au kuboresha zaidi nayo ni kazi za Bodi *(the function of the Board).* Nilikuwa napendekeza neno ku-*expand* shughuli hizi za sekta ya maziwa zisikose tafadhali ili na sisi kule ambako hatuna maziwa Mtwara na Lindi, basi Bodi iwe na kazi ya kuhamasisha zaidi na ikiwezekana tupatiwe ng'ombe wa maziwa. Mlishatupa ng'ombe lakini hatukuwaambieni mtupe ndiyo maana tulichinja wote, ila leo tunawaambieni tupeni. Mtwara na Lindi kila Kijiji ng'ombe si chini ya watatu, watatu au wanne, wanne, kopa ng'ombe lipa ng'ombe wa maziwa tusaidiwe ili na sisi tufaidike na hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu haina dini, kwa hiyo, mambo yake hayafuati ustaarabu wa Kiislam wala wa Kikristo. Lakini Waislam kila wanapofanya shughuli zozote zile kama ni kuchinja ama ni kusali huelekea *Kibla* yaani Kaskazini na Kusini hukupa mgongo. Sasa Serikali naona inakuwa kama waislam hivi, kila jambo likianza ni Kaskazini tu. Barabara nzuri Kaskazini, mambo ya utalii Kaskazini, maji safi Kaskazini, Makao Makuu ya *East Africa* Kaskazini, ng'ombe hao Kaskazini, huku Kusini kutuonyesha mgongo.

Sasa leo naomba katika hili kama kweli Serikali haina dini geukeni mwonyeshe macho Kusini. Ku-*expand* shughuli hizi kwa kumwaga ng'ombe kila Kijiji kwenye Vijiji vya Mtwara na Lindi ili Bodi hii ionekane ni ya Tanzania nzima siyo kwa Wamasai na Wasukuma tu maana yake Mheshimiwa Waziri Mmasai, Naibu Waziri Msukuma, wote wa ng'ombe ng'ombe nimeshawastukia katika hili tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kama Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kumwaga ng'ombe wa maziwa Mtwara na Lindi kila Kijiji. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ikiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara na hasa kwa ubunifu wa hali ya juu unaofanywa na hii Wizara na kielelezo kimojawapo ni huu Muswada ambao wameuleta mbele yetu na ambao unastahili kupongezwa na kuungwa mkono, nami naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye masuala yafuatayo:-

Kwanza, ni kuhusu kazi ambazo zimeorodheshwa kwa ajili ya Bodi ambayo imependekezwa katika Muswada wa hii sheria Ibara ya kumi ule ukurasa wa 58 hadi 59, nimejaribu kuzitazama zile kazi ambazo zimeorodheshwa zipo 22 na baada ya kufanyiwa kazi kwenye hizi *amendment* zilizokuja sasa hivi zimebakia 20. Mimi kwa jinsi ambavyo

naziona kidogo ni nyingi, hizi kazi ni nyingi na kwa chombo cha aina ya Bodi mimi naona ni *overwhelming.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masuala ambayo ningependa nipate ufafanuzi kidogo kuhusu kazi za aina tatu pale. Kwanza ni kuhusu ile *function (c)* ambayo inasema: *"to search and to develop markets."*

Mimi sijui kama kwa kweli Bodi itakuwa na *competence* pamoja na *capabilities* ya kuweza ku-*develop market per se* labda ambacho ningeona kwamba ina uwezo na ambayo ingekuwa ni kazi yake ni ku-*facilitate the process* ya ku-*develop market* pamoja na kufanya *search* ya hizo *markets* badala ya Bodi yenyewe ku-*develop* hizo *markets* maana yake sidhani kwamba watakuwa na *competence* kwa sababu wao wenyewe hawako kwenye ile sekta kama *producers* au *processors.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ni ile ya (f) kwenye *amendment* au kabla ya *amendment (g)* ile ambayo inazungumza ku-*ensure availability of appropriate technology for the industry.* Mimi kidogo pia hapo ninahitaji ufafanuzi kidogo kwa sababu sidhani kwamba Bodi yenyewe itakuwa *appropriate* halafu pili kama itakuwa na *competence* na *capability* ya *issues* za *technology* katika *industry.* Mimi nadhani wao kufanya kazi za ku-*coordinate* ni sawa lakini katika ku-*ensure* sijui kama wao watakuwa na *competence* lakini nitapenda kupata *clarity* kuhusu hiyo *function.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu kazi nyingine ambazo mimi zimenifurahisha. Moja ni ile ya (h) kwenye hii *amendment* ambayo ni ku-*monitor execution of contracts and marketing arrangements.* Imenigusa kwa sababu ya hali ilivyo kwenye Jimbo langu la Arumeru Mashariki. Kuna mifano mingi ambayo kwa ukosefu wa kuwa na chombo kama hiki cha Bodi tumeona madhara yake.

Nitoe mifano miwili, tuna taasisi moja ambayo wakati fulani ilikuwa na mitambo mizuri sana na ilikuwa ina-*process* maziwa na kutoa *products* nyingi tu na taasisi yenyewe ilikuwa ya Serikali, ilikuwa inafanya kazi nzuri sana na ilikuwa inatoa soko kwa wazalishaji wa maziwa. *Producers* wa maziwa wenyewe walikuwa wanauza kwao na walikuwa wamekuwa na soko zuri na watu walikuwa wamewaamini lakini baada ya muda wakawa hawawalipi wakulima kwa muda unaostahili, mwishowe wananchi wakakata tamaa. Mpaka sasa hivi nadhani wananchi wanadai taasisi.Wizara ingetusaidia kufuatilia hiyo *machinery* imefikia wapi na nadhani kwa kweli wananchi wameshakata tamaa na mitambo iliyokuwepo nadhani imeshakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu Kampuni moja ya maziwa iliyopo Kaskazini. Nadhani hiyo ni ya watu binafsi Mheshimiwa aliyetangulia, haikuletwa na Serikali, imekuja yenyewe. Ningeomba pia hiyo kampuni ifuatiliwe. Ilienda kwa wananchi ikawa-*organize* wananchi katika vikundi wakusanye maziwa yao. Wakaandaa watu wawe mawakala wa kukusanya maziwa kutoka kwa wananchi. Lakini wakala hawakuwa wanawalipa wananchi fedha zao kwa wakati uliokuwa unastahili. Wananchi wamelalamika, tumepeleka taarifa kwamba wanalalamika lakini kwa sasa hivi ni karibu

miaka mitatu na wananchi hawajalipwa hela yao na walikwishakata tamaa kwamba hilo soko halitawafaa tena na huyo mnunuzi wa maziwa yao nadhani ameshaacha uhusiano.

Kwa hiyo, ile *arrangement* iliyokuwepo kati ya mzalisha maziwa na mnunuzi huyo ambaye alikuwa yeye anakwenda ku-*process* ilishakufa na wananchi wamebakia na hasara ambayo hawajui jinsi ya kufidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni *function (k)* ule ukurasa wa 59 ile ku-*promote* na ku-*coordinate development of small, medium* na *large scale dairy keepers* na *processors.* Hiyo pia nayo naifurahia kwa kiasi kikubwa mfano ambao tunao tayari kwenye Jimbo langu wananchi walijiunga kwenye vikundi vidogo vidogo wakapata mfadhili ambaye aliwapa mashine za kufanyia hiyo kazi. Bahati mbaya sana tu hawakupata *technical assistance,* hawakupata ni jinsi gani wapate msaada kutoka Serikali au kutoka kwa mtu yeyote kuwasaidia ili uhusiano kati ya wale wazalishaji wa maziwa na hawa wanao-*process* na matumizi ya ile teknolojia waliyopata waweze kuitumia vizuri na kwa manufaa ya zao lao la maziwa. *As a result* ni kwamba sasa hivi kwa kweli haifanyi tena kazi kama jinsi ambavyo ingetazamiwa. Wizara kupitia Bodi, ifufue na kuhamasisha juhudi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu ieleweke kwamba kwa sisi kwenye Jimbo langu kwamba maziwa ni zao la kutuondolea umaskini na sisi ng'ombe wa maziwa ndiyo ambao unafahamu kwenye Jimbo langu hatuna ardhi, sisi kwetu tunafanya *zero grazing,* zao letu ni maziwa na huduma tunayopata kupitia kituo cha *NAIC* kilichoko *Usa River* ni huduma kubwa tunayopata kutoka Wizarani tunawashukuru sana kwa hiyo huduma. Isipokuwa tatizo tunalolipata mara kwa mara kwenye kituo cha *NAIC,* tunapofuatilia mbegu pale ni kwamba Kituo cha *National Artificial Insemination Centre (NAIC)* wanakuwa na tatizo la kuweza kutufikia kuja kutupa ile huduma kwa sababu hawana usafiri unaotosheleza kulingana na mahitaji ambayo tunawapelekea.

Tungeomba Wizara wasaidie ile *center* waweze kuwafikia wale ambao tunakwenda kutafuta hiyo huduma ili kuhakikisha kwamba uzalishaji wetu unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Shirika Lisilo la Kiserikali la *Heifer Project. Heifer Project International (HPI)* ni Shirika ambalo linashirikiana na watu ambao wanafanya *zero grazing* ya ng'ombe wa maziwa na nadhani linashughulikia siyo tu kwenye Jimbo langu nadhani lipo pia Kasulu na sehemu zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya mradi ambao nimeuona kwa kweli unatuondolea umaskini kwenye Jimbo langu ni huo Mradi wa *Heifer Project International.* Tungependelea tuone kwamba huo mradi unapanuka kwa zaidi ya ulivyo sasa hivi. Juhudi za kupanua Mradi wa *Heifer Project International* zionekane kama ni juhudi za kuondoa umaskini kwenye Jimbo letu na kwenye maeneo mengine ambapo wao wameupokea huo Mradi wa *Heifer Project International.* Kwa hiyo, kama ambavyo inazungumzwa kwamba *Heifer Project International* ni *partner* wa Serikali uonekane

pia kwamba ni *partners* wa Serikali katika kuondoa umaskini na sisi tutaunga mkono kikweli kweli kwenye hilo suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, langu la mwisho ni kuhusu suala la *market* na jinsi ya kuwasaidia wananchi ambao wanafuga ng'ombe wa maziwa na zao lao kuu hasa baada ya zao la kahawa kuwa na tatizo ni hili la maziwa. Tunayo masoko mawili.

Kwanza, ni soko la Mererani, Wilaya ya Simanjiro liko kilomita karibu 58 kutoka kwenye *center* kuu za uzalishaji na soko la Arusha Mjini ambalo liko wastani wa kilometa 12 mpaka 26 kutegemea na mtu anatoka wapi. Sasa soko linalopendelewa zaidi ni la *Mererani naturally.* Lakini watu wanavyosafiri kwa kweli ni kwa matatizo makubwa mno. Wanasafiri kwa baiskeli si chini ya kilometa 50 mpaka 59 kutoka Songoro kupitia *Usa River* mpaka Mererani wakibeba si chini ya lita 20 mpaka 50, 60 wakibeba na baiskeli. Kwa kweli ni kazi nzito. Sijui ni vipi Serikali mnaweza kutusaidia kwenye hili. Lakini labda hili ambalo limejitokeza kwenye Muswada huu ni kwamba Bodi ita-*promote marketing.* Njia mojawapo ni ku-*promote* Wakala kwa mfano, sehemu za *Usa River,* iwe ina-*link* kati ya Mererani au Simanjiro na Arumeru Mashariki na sehemu zingine za Ngarenanyuki na ukanda wa mbali kidogo.

La mwisho, ni kuhusu huduma kwa mifugo. Huduma kubwa ambayo tunaikosa ni huduma kwa ajili ya mifugo tuliyonayo ambayo ndiyo *source* ya maziwa nayo ni maji ya kunyweshea mifugo. Maji ni tatizo letu kubwa katika ukanda wa Arumeru Mashariki kuanzia hata Ngarenanyuki *all the way* mpaka Majengo, Makiba na Mbuguni kwa kweli ni tatizo kubwa mno.

Tungeomba Serikali ione uwezekano wa kuanza kutufikiria, tumeomba kupatiwa maji kwa njia nyingi sana na kwa muda mrefu sasa, lakini mpaka sasa hivi hatujafanikiwa. Tumejaribu kuomba kwa njia ya kupata Malambo bado hatujafanikiwa. Nina imani ili waweze kutuondolea umaskini kwa kukuza hili zao la maziwa wakati huu watatufikiria kupata njia ya kutusaidia nayo ni kuhakikisha kwamba mifugo yetu ina afya, inapata uendelevu kwa njia ya kupata maji ya kunyweshea, kwa kweli bila kunyweshea mifugo yetu hatuna njia ya kujiondoa na umaskini kama hatutapata maji ya kunyweshea mifugo yetu. Malambo tunayaomba, tunaomba maji tafadhali kuanzia Ngabobo *all the way through* Ngarenanyuki, King'oli mpaka Majengo. Hilo ndilo ambalo tunapendekeza na tunaomba kwa unyenyekevu kabisa Serikali itufikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya *Dairy Industry Act.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wa Wizara kwa kutuletea Muswada huu wa Sheria ambapo pamoja na mambo mengine unafuta sheria ya zamani ya Maziwa ya 1965.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pia kwa sababu ya malengo ya Muswada huu ambayo pamoja na mambo mengine unaanzisha Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta ndogo ya Maziwa na pia Muswada huu unaounda Bodi ya Maziwa ya Tanzania na mimi kama Mbunge ambaye nawakilisha wafugaji wadogo wadogo wa Kongwa ni vizuri nikapata fursa kama hii nikazungumza kwa niaba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua shughuli za ufugaji na uzalishaji mali kwa maana ya kutokana na ufugaji ni sehemu kubwa ya mamilioni ya Watanzania wengi hasa wanaoishi vijijini na ufugaji unachukua sehemu kubwa sana ya matumizi ya ardhi yetu kama malisho ya mifugo. Lakini tunafahamu pia kwamba toka miaka 70 hadi juzi Wizara hii ilipoanzishwa chini ya Mheshimiwa Waziri ndiyo hasa mmeanza kufufua shughuli nyingi za mifugo ambazo zilikuwa zimeharibika sana. *(Makofi)*

Sasa ili muweze kufikia mahali pazuri na malengo ya Muswada huu yaweze kutimizwa ni lazima mambo mawili, matatu, manne niyapendekeze ya kufanyiwa kazi.

Moja, umesema kwamba kuna ng'ombe wetu wa asili zaidi ya milioni 17. Nilikuwa nasema basi katika suala hilo la maziwa hebu tu-*develop* ng'ombe wetu hao, waboreshwe ng'ombe hawa badala ya kutegemea ng'ombe kutoka nje ili wawe ndiyo *central* katika suala zima la kutoa maziwa katika nchi yetu tusitegemee ng'ombe wa kigeni.

Tunalo tatizo kubwa sana la maeneo ya mifugo kuvamiwa kwa ajili ya kilimo. Ningeomba eneo hili liangaliwe na Sera tufike mahali maeneo ya mifugo yaeleweke na maeneo ya matumizi mengine yaeleweke. Bila huduma za kifedha kwa wafugaji wetu wadogo wadogo hawawezi kufika mbali, lazima jambo hili pia litazamwe ni namna gani tunaweza kuwawezesha wafugaji wetu ikiwa ni pamoja na wafugaji wenye lengo la kuzalisha maziwa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu nchi jirani ya Kenya wameendelea sana katika eneo hili la *Industry* ya Maziwa sana sana, tujifunze kutoka kwao katika upande wa uzalishaji, usindikaji na masoko, wamewezaje wenzetu wale kufika mbali kiasi hicho na mimi naamini inawezekana tukafika mbali kuliko wao.

Lakini la mwisho katika mapendekezo yangu na la umuhimu zaidi ni kupambana na magonjwa ya mifugo katika Wilaya yangu hasa yanayotokana na kupe. Sera inasema masuala ya majosho yaachiwe wafugaji wenyewe, Serikali iko pembeni kidogo. Ningeomba sana Serikali irudi isaidiane na wananchi kuona kwamba majosho yanakuwa kila mahali katika nchi nzima. Tusipofanya hivyo Sekta ya Mifugo haiwezi kufika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema sisi wa Wilaya ya Kongwa ni wafugaji na bahati nzuri tunayo *Ranch* pale japo nia na malengo yake ni *Ranch* kwa maana ya kutoa ng'ombe wa nyama, lakini pia kuna maziwa yanazalishwa. *Ranch* nyingine nchini zimebinafsishwa kwa namna moja au nyingine kwa Watanzania. *Ranch* yetu sisi bado inabaki mikononi mwa Serikali. Tunakubaliana na uamuzi huo ingawaje

tulipenda sana *Ranch* yetu nayo iende sawasawa na *Ranch* nyingine nchini zilivyofanyiwa ili na sisi sekta binafsi katika Wilaya yetu ingeweza kukuzwa zaidi. Lakini malengo ambayo Serikali imetuahidi ni mazuri kwamba *Ranch* hizi ambazo zimebaki zitakuwa kama ndiyo kitovu cha kueneza ufugaji bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini toka ahadi hii imetolewa Mheshimiwa Waziri, kwa kweli si mengi yamefanyika kuelekea upande huo tungeomba sana kukumbusha mambo haya kwamba *Ranch* sasa isaidie sana wafugaji wanaozunguka maeneo yale, ili waweze kuwa wazalishaji wazuri wa ng'ombe wa nyama na wazalishaji wazuri wa maziwa na *Ranch* yenyewe ndiyo *center* ya shughuli hizi za maziwa, itakuwa ni jambo zuri sana, mengine mengi tutaongea wakati wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye sheria moja kwa moja nikianza ukurasa wa kwanza wa 55 kwenye *definition* pale. *Definition* ya mwisho pale chini ya neno: *"dairy"* inasema: *"means any premises,"* nilikuwa na taabu kidogo kama ndiyo ilikuwa lengo. Nilidhani *"dairy"* itakuwa ni masuala *"milk products," skins* na kadhalika.

Nikienda ukurasa unaofuata wa 56 lile neno la kwanza kabisa pale juu *"designated milk,"* amesema pale mbele *means milk of which* kuna neno fulani la ajabu kidogo pale *"milch animals"* nafikiri kuna haja ya kurekebisha au pengine inaweza ikawa kwenye *amendment* imefanyiwa kwa sababu nimeipata sasa hivi sijaweza kuisoma. Linalofuata pale *milk means milk of cows.* Nilikuwa na taabu kidogo kama tunataka kuboresha masuala ya maziwa kwa nini maziwa mengine ya mbuzi na kadhalika tunayakataa yana matatizo? Nilikuwa nadhani tupanue zaidi shughuli hizi iwe ni maziwa yoyote yale ambayo tunaona kuna umuhimu wa kuyaboresha kuwepo kwake.

Ukurasa wa 58 fungu la 9 kwenye Bodi. Kwenye Bodi ile kuna *composition* kadhaa ya watu wanaoingia mle kuanzia Mwenyekiti na wengine. Kuna wajumbe muhimu sana watatu, wajumbe kwenye kundi B ambao ni wawili wanaowakilisha wazalishaji wa maziwa na kundi (f)Mjumbe mmoja anayewakilisha *consumers* hawa ndiyo watu muhimu kweli kwenye suala hili maana wazalishaji na walaji. Lakini ni watatu tu wajumbe hawa kati ya 12, mimi nadhani kwa sababu kundi hili ndiyo kubwa sana lingekuwa na wajumbe zaidi. Nilikuwa najiuliza huyu wa (f) kwa sababu bahati mbaya *registrar* ambaye ameanzishwa humu ndani hatakuwa na *register* ya *consumers* na haiwezekani kuwa nayo, sijui atapatikanaje huyu anayewakilisha *consumers?*

Nikienda ukurasa wa 59 kuna *functions* za Bodi, hii sitarudi ameeleza Mheshimiwa Talala Mbise, aliyeongea kabla yangu kwamba *functions* za Bodi ni nyingi mno, zilikuwa 22 zimepungua hadi 20, lakini bado kwa kweli ni nyingi mno.

Kwenye ukurasa wa 61 lile fungu la 16(5)(a) huyu *Registrar* atakuwa ana *register* ya *milk producers,* sasa tumesema kuna ng'ombe milioni 17, wazalishaji wako wengi kweli kule Kongwa, hivyo *register* hiyo itafananaje? Au ni *producers* wa kiwango fulani tu ndiyo watakuwa *registered* au iko? Kwa sababu hiyo inanipa wasiwasi pale fungu 17 ukurasa ule ule wa 61, 17(1) anasema: *"any person who deals*

*with milk or milk products"* lile neno deal linanipa taabu pale. Kwa sababu kwenye *definition* haliko mahali, ku-*deal* na maziwa ni kitu gani?

Nina ndugu zangu wengi sana hapa Dodoma wanatembeza maziwa kwenye ndoo wanauza kidogo kidogo tutawaita *dealers* wale kwamba wasitembeze tena kwa sababu hawajawa *registered* na vitu kama hivyo, tusije tukajikuta tumepitisha sheria ambayo inaweka ukiritimba mkubwa katika wauzaji wadogo wadogo wa maziwa ambao ndiyo wapiga kura wangu wengi kule na ndiyo Watanzania wengi. Ku-*register processes* ni sawa sawa na mambo mengine ni sawasawa lakini ku-*register* wazalishaji na hasa wazalishaji wadogo wadogo ilikuwa inanipa taabu itakuwa kuwaje hii? Maana shughuli ya uzalishaji maziwa sasa inakuwa kama ina wenyewe vile inakuwa siyo ya kila mtu kama ilivyo sasa.

Kwenye ukurasa wa 63 kwenye *offences and penalties* utaona pale kwenye fungu la 25(1) inasema: *"any person who contravenes any provision of this Act"* ndiyo yale yale kama aki-*contravene* kwa maana ya kuwa ame-*deal* na maziwa atapata matatizo makubwa, ndiyo maana nataka hili neno ku-*deal,* hili suala la kushughulika na maziwa tunamaanisha nini humu lieleweke vizuri.

Mwisho, kwenye ukurasa ule ule wa 63 fungu 25(2) anasema: *"Where a person is convicted of an offence under this Act, the court may order that any milk or milk product in respect of which the offence has been committed be forfeited."*

Ni vizuri lakini hapakusemwa hapa: *"under what circumstances the court may order so..."* ni vizuri zaidi tungejaribu kueleza kidogo kwa kufafanua vizuri zaidi ili kuweka usalama zaidi katika shughuli nzima ya kushughulika na maziwa.

Mwisho, kama nilivyosema mwanzo ningeomba kupongeza sana juhudi zote zilizofanyika katika kuleta Muswada huu wa kufuta ile sheria ya zamani ya mwaka 1965 na kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba wananchi wa Tanzania watafaidika na wananchi wa Kongwa watafaidika, kwa hiyo, sina sababu ya kutounga mkono hoja hii. Naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamepata nafasi mbalimbali katika dunia hii.

Kwanza, Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika na pili, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa. Kama walivyoeleza wenzangu wametuongezea sifa kwa nchi yetu kuonekana imeweza ku-*produce* Marais wawili, naamini na wengine hatujui kama wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Muswada huu. Suala la maziwa kwa mara ya kwanza sasa limepata heshima ya kuweza kuzungumziwa na Taifa nzima. Maziwa ilionekana kama ni shughuli ya mtu ambaye basi tu kama hawa wenzetu ambao asili yao ni wafugaji kama ni jadi yao tu. Lakini suala la maziwa ni suala linalohusu afya ya binadamu na hasa watoto wetu.

Suala la maziwa kama walivyoeleza wengine ni kazi muhimu kabisa ya kumuondolea mtu umaskini wake kama ikifanywa vizuri. Kwa hiyo, siyo tu kuondoa umaskini lakini kazi ya kufuga ng'ombe na kuuza maziwa inasababisha watu kupata ajira na katika kiwango kikubwa shughuli ya kufuga ng'ombe wa maziwa pia inasaidia katika hifadhi nzima ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimesema kwamba tunashukuru kwamba leo Serikali imeleta Muswada huu na kuzitambua kabisa shughuli za wafugaji wa ng'ombe wa maziwa zikitambulika Kitaifa. Wananchi wengi wamekuwa wanajishughulisha na shughuli za ufugaji, lakini wanafanya kwa namna ambayo hakuna anayewatambua ama anayewaona wanafanya nini?

Kwa hiyo, ukichukua kama sehemu za vijijini hususan kama sehemu za kwetu kule Njombe, mtu anaweza akawa na ng'ombe wa maziwa akapata maziwa akauza hata kwa bei ndogo kabisa ambayo haina hata faida kwake yeye mwenyewe anayefuga. Kwa utambuzi huu na shughuli ambazo Bodi hii inaweza kuzifanya, na mimi nakubaliana na wale wadau waliosema pengine tungesema Muswada wa Kuendeleza ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Kwa sababu wale waliokuwa wanafuga sasa walishazoea kuwa na wanyama wale nyumbani, lakini kwamba wana faida sana kwao ilikuwa si kubwa. Kwa sababu namna ya kuuza yale maziwa ilikuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata huduma zile za ugani kwa asilimia kubwa zilikuwa hazipatikani kwa urahisi. Mtu anakuwa na ng'ombe wake kijijini, akiugua hasa ng'ombe wa maziwa wa kisasa, akiugua hajui apate wapi huduma za kumtibu yule ng'ombe. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwa maana ya Muswada huu tutakuwa tunaangalia ng'ombe kama ni njia mojawapo ya uchumi katika nchi yetu. Kule kwetu kuna Chama kabisa cha wafugaji wamejitahidi kuanzisha Chama ili waweze kupata hizo huduma kama inawezekana. Lakini mara nyingi wamekuwa wanahangaika wao wenyewe hawapati kutambuliwa kwa urahisi kama ilivyo.

Sasa mimi naamini kabisa humu nimekuta msajili yule atakuwa anasajili wale wafugaji. Lakini nafikiri pia tungeongeza kwamba wasajili hata Vyama vilivyoundwa visajiliwe kama Vyama. Najua Bodi nyingine Vyama vinasajiliwa kama Ushirika, unasajiliwa kama Ushirika wa Wafugaji, maana mwingine ana ng'ombe mmoja, wawili lakini wana Ushirika wao ambao katika Ushirika wao wana ng'ombe wengi wangeweza kusajiliwa.

Naomba katika utaratibu huu wa kutambua wafugaji naamini hii Bodi itakapokuwa imeundwa pia itatambua pia wataalam wa mifugo kila mahali wanafanya kazi zinazostahili na wao pia watambuliwe. Najua Wizara ina kazi hiyo, lakini Bodi hiyo pia ingetambua hawa wataalamu wapi wanaweza kuhudumia mifugo mbalimbali. *(Makofi)*

Halafu naamini kabisa Bodi hii pia itafanya sensa ya kujua mifugo hii ya ng'ombe wa maziwa iko mahali gani na kwa kiwango gani. Kwa sababu kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara, kuna maeneo kweli ng'ombe wapo wachache au hawapo kabisa. Lakini kuna maeneo watu wanafuga ng'ombe hivi hivi kienyeji kienyeji tu. Kwa hiyo, mimi naamini Bodi hii kazi yake moja ni kutambua mifugo *concentration* yake iko wapi?

Halafu pia watambue na viwanda ambavyo vingine vimeanzishwa kama alivyozungumza Mheshimiwa Talala Mbise. Kuna viwanda vya maziwa vilikuwepo hata kule Njombe tunacho kiwanda, lakini kwa muda mrefu hakijaanza kufanya kazi, kuna maelezo mbalimbali ambayo yanashangaza kwa nini kiwanda kinachelewa kilitakiwa kuanza mwaka juzi mpaka leo hakijaanzishwa. Lakini naamini hii bodi ikitambua kwamba kuna viwanda vipi katika nchi na kwa nini viwanda hivi vinakwama ama kwa nini havifanyi kazi?

Kwa hiyo, hii Bodi itakuwa imeanzia na vitu ambavyo vipo. Sasa watakuta sehemu nyingine wafugaji wako wengi, lakini viwanda vya namna hiyo havipo. Kwa hiyo, nadhani ni wajibu wa hiyo Bodi kuona kwamba kule ambako kuna wafugaji wengi viwanda havipo vianzishwe, vile vilivyopo vifanye kazi tena vizuri. Kwa hiyo, mimi naamini kwamba hiyo itakuwa ni kazi nzuri kwa upande wa Bodi. Lakini wakati huo huo nchi yetu ni kubwa hata Jimbo langu tu ni kubwa kwa maana ya ufugaji. Kutoka Makao Makuu ama kwenye Kiwanda hicho mpaka kwa mfugaji wa mwisho kuna kilometa saa nyingine 60, kuna kilometa 70 mpaka 100. Sasa hiki kiwanda kiko mjini kwa umbali huo atakusanyaje maziwa kutoka kule na kuweza kuyapeleka karibu na kiwanda yasiweze kuharibika?

Nakumbuka zamani kulikuwa na vituo vya kukusanyia maziwa katika Shirika moja lilikuwa la maziwa wakati ule nimesahau jina lake. Lakini nafikiri sasa ni wakati muafaka Bodi ibuni mbinu ambazo zinaweza kuwawezesha wafugaji wadogo wadogo kuweza kukusanya maziwa na kuyapeleka kunakohusika kwa urahisi zaidi kuliko kusafiri maili nyingi kama ambavyo wenzangu wamezungumza. Kwa sababu hiyo watajua kabisa nafuga ng'ombe wangu, nakusanya maziwa yatakwenda kwenye kiwanda kinachohusika mapema kabla hayajaharibika na mwenyewe mwenye ng'ombe kulipwa fedha anazostahili.

Sisi kule kwetu Wilaya ya Njombe tunatumia sana mbolea ya chumvi chumvi katika ardhi kukuza mazao yetu mengine. Mpaka hivi sasa ardhi yetu inahitaji mbolea nyingi sana na acid yake imekuwa juu sana. Kwa hiyo, unakuta sasa hivi hakuna namna mtu anaweza akalima mazao yake asitumie mbolea ya chumvi chumvi akapata kitu. Lakini sisi tunaamini kabisa kama tungekuwa na ng'ombe wengi, watu wangeanza

kutumia mbolea hiyo ya ng'ombe katika kubadilisha udongo usiwe na chumvi chumvi nyingi kama ulivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Shirika la dini la *CARITAS* limeanzisha kilimo cha kujinusuru. Wanachokifanya wanatengeneza shimo moja kubwa na kujaza mbolea nyingi hii ya samadi ambayo katika shimo lile unaweza kupanda mahindi au unaweza kupanda kahawa au unaweza kupanda mazao mengine, lakini katika miaka mitatu unabadilisha ili kusudi ubadilishe ile chumvi chumvi iliyoko ndani ya ardhi angalau iweze kubadilika kwa kutumia mbolea ya samadi. Sasa kama sheria hii ikipitishwa na Bodi yetu ikafanya kazi vizuri naamini kabisa kazi yake moja kubwa itakuwa ni kueneza mifugo mingi zaidi katika maeneo ambayo mifugo yake ni michache. Kwa sababu hatutazungumzia *export* ya maziwa kama mifugo ni kidogo kama ilivyo katika maeneo fulani fulani. Kuna maeneo yenye baridi kama kwetu mimi naamini ni mazingira mazuri zaidi ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa pengine kuliko maeneo mengine yote. Kwa sababu magonjwa yanakuwa kidogo yamepungua na utunzaji wa maziwa na mazao mengine ya maziwa yanaweza kutengenezwa kwa urahisi sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni ombi kwamba Bodi hii moja ya kazi yake kubwa ni kuangalia usambaaji wa mifugo katika nchi na pale ambapo mifugo inaweza kuwa mingi na ardhi ni kubwa kama kwetu watu wakaongezewa ng'ombe hata kwa utaratibu huu wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Ingawa mimi huwa siupendi sana, kwa sababu ng'ombe mpaka atakapokuwa amepandwa mpaka akazae mpaka upate wewe inaweza ikapita miaka miwili, mitatu. Kwa hiyo, nadhani kabisa Bodi nayo itatafuta utaratibu ambao ni rahisi zaidi wa kupata ng'ombe na kuwakopesha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa naomba tu kwamba Bodi yetu hii isimamie kweli masoko ya maziwa hayo yatakayokuwa yanapatikana ndani ya nchi, kwa sababu tunahitaji sana maziwa kwa watoto wetu wengi wanapata matatizo ya utapiamlo kwa sababu wengine hawajawahi kunywa maziwa. Kwa hiyo, kwa maana ya Bodi hii kufanikiwa ni kujaribu pia kuongeza wingi wa ng'ombe katika maeneo mbalimbali ambako ng'ombe wanaweza kuendelezwa. Halafu uwepo na utaratibu wa soko la ndani la maziwa ku-*export* maziwa ni sawa, lakini soko la ndani la maziwa pia liweze kutambuliwa kama wanavyofanya sehemu nyingine kunakuwa na *packet* za maziwa mtu anaweza akayanunua maziwa wakati wowote na mahali popote kwa urahisi. Hivi sasa watu wanauza maziwa kwenye ndoo mpaka uyapeleke mwisho yanakuwa yamekwishaharibika, hujui usafi wake.

Kwa hiyo, nadhani Bodi hii pia katika soko la ndani itakuwa na *package* ndogo ndogo zinazoweza kununuliwa kwa bei ndogo yaani *package* ndogo anayoweza kununua mtu yeyote kwa urahisi. Lakini wakati huo huo kama nilivyosema sisi kwetu tunacho kiwanda, lakini kimechukua muda mrefu sana kuanza na matatizo yake mimi sielewi. Lakini nadhani Bodi hii itatambua viwanda vilivyopo katika sehemu mbalimbali ndani ya nchi na vile vinavyoweza kufanya kazi vifanye kazi.

Mwisho, ni kwamba mifugo yetu inahitaji madawa. Bei za dawa za mifugo ni aghali sana, kwa hiyo, huyu mfugaji ambaye ana ng'ombe wachache na bei ya maziwa ni

ndogo na bei ya dawa ni kubwa inakuwa vigumu sana kwa mtu huyu kuweza kuendeleza ng'ombe wake na akawa anaweza akafanya kazi ya kufuga ikawa ni sehemu mojawapo ya kujiondoa katika umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda wako naomba niseme kwamba Bodi hii itusaidie kuongeza huduma za ng'ombe kama alivyosema ndugu yangu kuhusu suala la maji. Tunafurahi kuona katika sehemu mbalimbali Mheshimiwa Waziri tangu ameanza kuongoza Wizara hii malambo mengi yameanzishwa. Mimi nadhani juhudi ya kuanzisha malambo kwenye maeneo yanayotakiwa malambo iongozwe na juhudi ya kupata maji mengine katika maeneo hayo ya mifugo pia iongezwe, kusudi ng'ombe wanaokuwa wanatoa maziwa pia watoe maziwa yaliyo safi na mazuri kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili nami nichangie katika Muswada huu. Muswada wa Sheria ya Maziwa wa mwaka 2004.

Nianze na mimi kumpongeza Mheshimiwa Getrude Mongella ambaye amechagauliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa ambaye naye amepata wadhifa huo wa Rais katika Baraza la Mazingira la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii sasa niwapongeze Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Naibu wake pamoja na wataalamu wa Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kuleta Muswada huu ambao kwa kweli umeshirikisha wadau wa maziwa. Muswada huu ni muhimu nadhani ni vizuri wote tukajua chimbuko lake. Tunajua kabisa kwamba ipo Sheria ya Maziwa ya mwaka 1965 na kwamba kutoka mwaka 1965 mpaka mwaka huu wa 2004 yametokea mabadiliko makubwa ya kijamii na kiuchumi. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba sheria hii ambayo imekuwa ikitumika sasa haiwezi ikakidhi mahitaji ya mabadiliko ya hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukaona kama mabadiliko ya aina tatu yametokea. Mheshimiwa Waziri ameyataja kwa kina, lakini kwa kijumla yametokea mabadiliko matatu makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 1965 wakati wa sheria hii mpaka mwaka 1967 tumeshuhudia kwamba uchumi wetu umekuwa ukisimamiwa zaidi na vyombo binafsi. Baada ya mwaka 1967, baada ya Azimio la Arusha yametokea mabadiliko makubwa ya kusimamia na kuendesha uchumi wetu, ambayo baada ya Azimio la Arusha tumeona kwamba uchumi wetu ulisimamiwa zaidi na Serikali au na umma. Lakini baada ya mwaka 1990 njia kuu za uchumi zimerejeshwa tena na kusimamiwa na watu binafsi na tumeanza sera ya ubinafsishaji. Sasa mabadiliko haya makubwa matatu ni dhahiri kwamba hayawezi yakasimamiwa na sheria iliyotungwa

mwaka 1965. Kwa hiyo, ndiyo maana sheria hii ni muhimu sana ili kuweza kuleta mabadiliko ya kusimamia sekta hii ndogo ya maziwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya sheria hii mpya kama ilivyoelezwa inakusudia kudhibiti, kuboresha, kuhamasisha uzalishaji, utengenezaji, utafutaji wa masoko na matumizi ya maziwa na bidhaa zake. Sasa sheria hii katika kukidhi maeneo haya yaliyotajwa itaweza kuleta maendeleo katika sekta ya maziwa. Sheria hii kwa kweli itaweza kutatua matatizo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wameyataja kwamba katika kusimamia maziwa, maziwa ni *delicate product* na huwezi ukayahifadhi kwa muda mrefu.

Kwa hiyo, yanahitaji masoko ya haraka ama yanahitaji utashi mkubwa katika *processing* ili yaweze kudumu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, sheria hii ambayo wadau wenyewe wameisimamia au wameshiriki katika kuitunga itasaidia sana kufanya *promotion* ya kuweza kuuza maziwa, kwa sababu maziwa yatakuwa na ubora unaofaa zaidi na katika usindikaji sheria hii itasaidia kuhakikisha kwamba maziwa yetu yanasindikwa kwa ubora unaotakiwa na kwa kuweza kuhifadhika kwa muda mrefu ili yaweze kuhimili ushindani wa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema waliotangulia kwamba katika biashara hii ya maziwa sisi Watanzania tumepitwa na wenzetu wengi. Tumeona hapa maziwa mengi yanauzwa kwa mfano maziwa ya *cowbell* hayatoki hapa yanatoka nje yanaleta ushindani mkubwa sana kwenye maziwa yetu. Kwa hiyo, kwa kuwa na sheria hii ni dhahiri kwamba uundaji wa vyombo hivi viwili, uundaji wa Baraza la Mwaka na uundaji wa Bodi utawawezesha wadau kubadilishana mawazo na kuweka taratibu ambazo zitaweza kuongeza ushindani katika maziwa tunayoyazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ni nzuri na mimi napenda niseme naiunga sana mkono. Yako maeneo tu machache ambayo kama tunataka kuimarisha uzalishaji kama dhamira ya sheria yenyewe ilivyotaja yako mambo muhimu ambayo yanatakiwa yatazamwe. Kwa mfano, suala la uzalishaji maziwa kwa kutumia ng'ombe bora. Hivi sasa ng'ombe wetu wengi waliopo vijijini ni wa kienyeji. Kama takwimu zinavyoonyesha kwamba wako ng'ombe wa maziwa wa kisasa kama laki tano. Lakini wako zaidi ya milioni 16 ng'ombe wa asili ambao pia ni ng'ombe wanaotumika kwa kutoa nyama na kutoa maziwa. Kwa hiyo, kama tunataka kuongeza uzalishaji wa maziwa ili tuweze kupunguza gharama maana unapoongeza uzalishaji kwa ng'ombe mmoja vile vile unapunguza gharama ya lita ya maziwa unayozalisha.

Kwa hiyo, ili tuweze kufikia lengo hilo la kuongeza uzalishaji wa maziwa na hivyo kuweza kupunguza gharama ya uzalishaji na kuweza kuuza kwenye bei ambayo ni ya ushindani ni vizuri kabisa taratibu zile za uzalishaji ambazo zitaelezwa kwenye kanuni zitilie mkazo sana uzalishaji na uendelezaji wa ng'ombe wa kisasa. Kwa maana ya kuzalisha kwa kutumia ng'ombe wetu hawa hawa lakini kwa kuingiza mbegu bora ili tuweze kupata uwanja mkubwa wa ng'ombe wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ambayo ni muhimu katika uzalishaji huo ni huduma za ugani pamoja na huduma za tiba na huduma za *artificial insemination.* Sasa huduma hizi tatu kama tunavyofahamu kwa kiwango kikubwa huduma ya tiba na ya uhamilishaji imeachiwa sana sekta binafsi. Sasa ipo hatari kama Muswada huu hautatazama ni kiasi gani utasimamia hii *artificial insemination* ukiachilia mbali kwamba upo Muswada unaozungumzia tiba lakini Muswada huo wa uzalishaji ama *breeding* haupo bado. Kwa hiyo, ni vizuri sheria hii kupitia kanuni basi Waziri akatamke wazi kwenye kanuni ni jinsi gani hawa wanaofanya *artificial insemination* watahakikisha kwamba wanatumia mbegu bora na mbegu ambazo hazijapita wakati wake. Kwa sababu liko tatizo la hawa wafanyabiashara kwamba kama wasiposimamiwa vya kutosha wanaweza wakazitumia hata mbegu ambazo hazina ubora unaoridhisha. Kwa hiyo, ni vizuri jambo hili likatiliwa mkazo.

Yapo maeneo machache katika Muswada wenyewe ambao nadhani Waheshimiwa Wabunge wengine wameyataja lakini naomba niyataje tena kwa sababu ya umuhimu wake. Kwanza ni *definitions.* Katika Muswada huu tunazungumzia juu ya *diary industry.* Zimetolewa *schedule of amendments* sikuona kama kuna *definition* ya *diary industry.* Nafikiri bado tunafikiri kwa *assumption* kwamba wote tunajua *diary industry* ni kitu gani. Kwa hiyo, ningeomba katika Muswada huu tui-*define* hiyo *diary industry* ila kila mtu aweze kuelewa kwamba tunazungumzia kitu gani.

Katika ukurasa wa 35 kulikuwa na *concern* ya Mheshimiwa Job Ndugai ambayo na mimi nimekuwa nayo juu ya *definition* ya *diary.* Sasa ukiangalia ukurasa ule wa 55 ile *definition* ya *diary* pale mwisho *means any premises used for production.* Halafu ukienda ukurasa wa 59, kipengele (h) kinachozungumzia *to register producers and processors of diary and diary products.* Hapo ndiyo unaona kabisa kwamba nadhani *definition* ya *diary* pale haikukaa sahihi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri waitazame ile *definition* ili isilete utata katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema na walivyosema wengine Muswada huu kwa kweli umekuja kwa wakati. Nadhani ni Muswada ambao kwa kuwa wadau wengi wameshiriki na wenyewe wameukubali hakuna tena mantiki ya kusema tena Muswada huu si mzuri kwa vyote vyote utaboresha uzalishaji wa maziwa na kuongeza ubora wa maziwa na hatimaye kufanya maziwa yetu yaweze kununulika na kupata soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Muswada wa Sheria ya Maziwa ya mwaka 2004. Kabla sijachangia kwanza nimpongeze Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Naibu wake na wataalamu wake katika Wizara kwa kuweza kutuandalia Muswada huu. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Pili, nataka niseme machache tu. La kwanza najaribu kufikiri huu Muswada utatufanyia nini. Najaribu kutafakari sana. Kwa sababu sio mara ya kwanza katika nchi

yetu tunatengeneza Miswada. Tulikuwa na *DAFCO* mwaka 1965 kitu kama hicho alizungumzia Waziri . Tulikuwa na *LIDA,* Shirika kubwa sana ambalo lilikuwa linabeba Mashirika mengi sana ya mifugo, kuku, samaki na kila kitu, lilikuwa linabeba mifugo yote katika nchi hii. Hata hii *diary* tulikuwa nayo ikaishia mwaka 1975.

Sasa ninachotaka kusema hivi tunasogea wapi maana nikikumbuka wale waliokuwa kwenye *DAFCO* na *LIDA* walivyokula walinenepa vizuri sana mpaka yakafa yote. Ng'ombe wa maziwa zilikuwa zimeenea katika nchi hii. Sio Musoma wala wapi mpaka na kadhalika. Sio *diary* tukapata na kadhalika wacha hii *cowbell* ambayo inakuja sasa hivi. Tulishakula siagi nzuri nchi hii. Hebu tufikiri ni kitu gani kabisa kilikuwa kimeua Mashirika na hili tunaloanzisha sasa ni kitu gani ambacho tuta-*improve* ili kisife.

Mimi nimeona hapa *source of income* katika hii Bodi wameweka sana. Lakini wameingilia sasa zile *products* kwamba ukiwa na kiwanda nao wanapata asilimia. Sasa watu 12 ambao hawana mahali pa kula wanataka sasa kula kupitia migongoni mwa watu wengine, kweli hii kitu kinaweza kuishi. Maana yake tunaunda kitu wao hawazalishi kila kitu au labda Serikali itoe kitu fulani iwape *support* lakini *income* yao kubwa sasa *customer* wake someni ziko pale mtakuta mlaji hana nafasi ya kupumua hapa, hana. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kilichoua zile Mashirika ndiyo haya na tunazidi kurudia tena. Kwa hiyo, naomba sana kama ndivyo hivyo tutoe kabisa mahali ambapo unapata *income* kutokana na muuza maziwa asije akaterereka tena. Sio kwamba unapeleka kiwandani halafu anatoa asilimia 5 ya Bodi, asilimia 3 sijui ya kitu gani. Nao wafuge ng'ombe nao wafanye nini wauze kama Bodi. Wafuge ng'ombe wauze wapate faida. Si kutegea watu wengine waende nao shambani. Kama Bodi tujue kabisa ile *farm* ni ya Bodi na inapata mshahara wake kweli kwenye Bodi kuliko kutegea wakulima. Ndiyo tunajua kabisa kwamba hawa watu kweli wanasimamia kabisa hii *diary.* Bodi yenyewe maana mabodi ya sasa hayazalishi wanaegemea egemea hapa na pale. Kama wewe ni wa *diary* kusema kwamba Kitungule au *farm* fulani ni ya Bodi posho yako utapata kwenye hiyo *farm.* Labda niseme hilo tu. *(Makofi/Kicheko)*

Halafu lingine nimalizie tu kwamba kwa kweli maziwa ya *industry* ni muhimu sana, lakini soko. Wenzangu wamezungumzia soko. Wengi wangeweza kufuga kweli ng'ombe wa maziwa na inaondoa umaskini kwa haraka sana. Ukiangalia mahali ulipo *Heifer Project International* wananchi kwa kusema kweli wamejikwamua wanapata maziwa na wanauza vizuri tu. Lakini dawa ya mifugo sasa hivi ni ghali sana.

Mimi juzi nimechukua dawa ya mifugo yaani nimetumia karibu shilingi laki tatu hivi hivi tu. Sasa hakuna mtu anayeangalia na mfugaji hakuna mtu anayeangalia lakini wote mnakula nyama, mnakunywa maziwa lakini kusema huyu mfugaji anaumia kiasi gani, hamna. *Subsidy* hamna wote kwa mkulima ndio wote tunagutuka eeh, jamani kule punguza *subsidy.* Sasa mfugaji nani atakupunguzia *subsidy.* Lugha tu ni mkulima na wafugaji lakini wakati wa kwenda kula kukaa vizuri anaachiwa mfugaji pembeni mkulima anahudumiwa vizuri. Mkulima ukila nyama sasa hivi 17.2 milioni ng'ombe ndugu yangu huyu anayefuga ukimwona unasikitika. Anapolala, anapovaa, elimu yake

lakini tuna-*enjoy benefit* yake. Tunakula tu kama binadamu huachi leo kwa nini hukwenda kuchukua kilo moja wewe namna gani imelika kitu gani bila nyama hapa. Unamwangalia na yule alivyo na hali na mifugo yake.

Kwa hiyo, naomba sana hebu tuangalie ili waweze kunufaika hawa wafugaji. Tuangalie madawa ya ng'ombe ambayo yanatumika.

Halafu sio hiyo tu tuangalie wanafugia wapi. Mmeshaweka mahali pa kufungia hawa wafugaji. Wana maeneo yao, mnayajua wote au wanatembea hivi tu ukikutana nao ukienda Morogoro unaona ng'ombe wana *cross* hivi unajua wanakwenda wapi? Wewe unapishana tu ni lazima ieleweke kwamba hawa wako wapi na wanakwenda wapi na wataishi wapi. Wewe unasema tu 17.2 milioni wako wapi wanaishi namna gani.

Kwa hiyo, hiki inahitaji *planning* kubwa sana kama tunataka kwenda mbele wenzetu walifanya hivyo. Halafu ukitaka hii sio watu wote wanakunywa maziwa. Lakini lazima tufanye utaratibu wa watu wote kujifunza kunywa maziwa kama sisi tunafanyiwa *experiment* ya namna ya kula samaki. Kuna watu nao lazima wafanyiwe *experiment* ya kunywa maziwa. Sasa siku hizi kuna maboti na utaratibu wa kula samaki tunafanyiwa *experiment* miiba isije ikaingia tumboni, ndiyo hivyo na ninyi lazima mkafanye *experiment* ya kunywa maziwa. Ukitaka hiyo *experiment* anza na watoto wadogo.

Katika Shule za Msingi mtoto anayekunywa maziwa mwili wake unatereza hauna mabaka. Anakua haraka na ukimwona mtoto wa miaka 15 yaani unamwona kabisa kwamba ana afya nzuri sio sababu ya kupaka ma-*lotion* hapana. Tuanze na watoto wa Shule za Msingi kwa nini wenzetu wa Kenya wameanza pale.

Kuna siku ya kunywa maziwa, watoto wanakwenda shuleni na vikombe ni siku ya Taifa. Watoto wana afya nzuri. Sasa kama tunaangalia watoto hivi saa nne utakuta utapata *producers* wazuri wa maziwa karibu na mashule, watoto hawa wakishakuwa miaka 15 au 16 watoto hawa watakunywa maziwa. Lakini kuna watu hapa mkiambiwa maziwa chai ya rangi, unataka nini? Chai ya rangi. Kwa sababu tumbo lake halithamini mikiki mikiki ya maziwa. Haithamini ina mafuta na jasho lete chai ya rangi. Kwa hiyo, lazima tubadili nia na tabia yetu.

Kwa hiyo, naomba hilo tuangalie kabisa na tuwe *agressive* na sehemu zote ambazo watu wanakunywa maziwa kweli uchumi wao uko juu kidogo kwa kufuga ng'ombe wawili. Ipelekwe Kusini kama alivyozungumza. Yapelekwe na tena tumekwenda kule Masasi ni sehemu nzuri kabisa ya kufugia ng'ombe. Kusini haina matatizo kabisa. Hakuna na ndugu yangu Namkulala yeye anafahamu, Kiteto badala ya kuja kuchukua mahindi achukue na ng'ombe.

Sasa wewe unaacha ng'ombe huku unapeleka mahindi, sasa basi. Lazima na watu wa Kusini na wao wawe *aggressive* kuinua uchumi wao. Ng'ombe mmoja nyumbani umetoa umaskini. Utapata maziwa ya kutosha, utauza, utaelimisha watoto wako bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwisho leo usiku na mimi nichangie kidogo kuhusu hoja ya maziwa.

Mimi ni mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ambaye inashughulikia upande wa mifugo vile vile. Kwa hiyo, nilikuwepo katika kupitisha Muswada huu ndani ya Kamati. Kwa hiyo, mimi hapa nasimama kwa kusema kabisa kwanza naunga mkono hoja hii. Ninachokifanya hapa ni machache ya kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli dhana nzima ya kuleta Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka ila umechelewa, kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuunga mkono ili tuwe tunapata mahali pa kuanzia. Ukiangalia Tanzania kama ilivyo utakuta kwamba ni nchi ya tatu kwa mifugo katika Bara la Afrika. Lakini bado hatuvuni raslimali hii kiuchumi kama zinavyofanya nchi zingine kama vile Botswana na kwingineko. Kwa sababu ya kukosa fedha za kuhudumia wataalamu au namna ya kutunza au labda kukosa hizi *Regulatory Boardies* ambazo zinashughulikia hoja nzima ya mifugo hii.

Hapa tumeambiwa kwamba kuna vikundi tayari 1,136 vya maziwa ambayo wadau wake tuliwaalika kwenye Kamati yetu. Lakini pamoja na uzuri wa sheria hii kama hatufanyi mpango madhubuti wa kuwasaidi hawa wenye vikundi na wafugaji kwa ujumla tutakuwa sawa na kwamba unatwanga maji kwenye kinu. Hakuna namna yoyote ile Muswada huu utakuwa msaada kwa wananchi na kwa Watanzania na kwa uchumi wa nchi hii kama hatuwezi kusaidia kutoa ruzuku kwa wafugaji ili wajiwezeshe.

Ninachokiomba hapa na bahati nzuri wakubwa wote wako hapa wakulima pamoja na Waziri mwenye dhamana hii ya mifugo ambaye ni Mheshimiwa Edward Lowassa wanapokwenda kuomba fedha wanaambiwa kwamba fedha mwisho ziishie hapa na wanapewa labda za mishahara michache ya watumishi tu. Fedha haitoshi katika Wizara hii.

Mimi naomba Serikali hii ya Tanzania iangalie uwezekano kabisa na kufumba macho mahali pengine namna ya kutoa fedha ya ziada kwa Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Majosho yaliyokuwepo hayapo sasa hivi na haiwezekani tuseme kwamba itakuwa na miujiza huu Muswada unaopita sasa hivi yatafufuka sasa hivi bila fedha. Haiwezekani, inatakiwa fedha kuiangalia Wizara nzima na sisi tunategemea kwamba ili kumaliza njaa Tanzania ni lazima tuingie kwenye vitu ambavyo ni vya uzalishaji kama mifugo, kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ni mojawapo kufanya *incentive* humu ndani ili tuweze kumpa fedha Mheshimiwa Edward Lowassa. Hii mambo ya kusema tunamwekea *ceiling* Bajeti yake haiwezekani akipeleka kule Wizarani ipite yote, ni maisha yetu sisi

Watanzania. Tusicheze na maisha yetu sisi Watanzania. Vingine kwanza vikae pembeni lakini kilimo, ufugaji Serikali iseme hapa inapeleka fedha yote itasaidia Serikali na wananchi wake na uchumi pia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba hilo ombi lichukuliwe kwa ujumla kabisa wala lisifanyiwe mzaha. Hilo ombi likishapita tunafanyaje. Kuna hivi vikundi sasa. Kuna hii Bodi ambayo tunaipitishia leo Muswada huu. Tunaweza tukanunua mashine ndogo ndogo ambazo zinatengeneza samli, siagi tukawapa wanavijiji vikundi hivyo vidogo vidogo vikafanya kazi nzuri sana. Samli haiozi haraka kama maziwa yenyewe.

Kwa hiyo, ile samli inaweza ikakaa na ikauzwa kwa kipindi kirefu. Tukiwapa hizo mashine zitaweza kufanya kazi nzuri ambayo tutaona *product* hii namna sasa itakavyo *take place* na kila mtu ataona kuna faida ya mifugo ndani ya nchi yenyewe na tupewe fedha kwa mfano tunaongeza Bajeti ya Wizara tunasema kwa kipindi cha miaka mitatu tupeleke ng'ombe Kusini, tufanye hiki, tusaidie vikundi hivi kwa kipindi hicho cha miaka mitatu kwa sababu tumechelewa sana bila kudai kodi. Baada ya miaka mitatu ndiyo unawafuata wale ambao wameshakuwa wafanyabiashara wakubwa. Unaleta sasa kodi kwa sababu tuliwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtoto anapokwenda shule anakopeshwa lakini baadaye anapomaliza anaambiwa sasa unarudisha. Lakini huwezi kuanza leo leo unamwambia kwanza lipa zote. Tuna watoto wanasoma Chuo Kikuu tunawakopesha na hili tufanye hivyo. Serikali itoe fedha kwa makusudi tuwape hao wanapoanza kuzalisha tutawadai baada ya miaka mitatu, tuwape *grace period.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuna kitu ambacho hatuna hapa Tanzania. Ukiangalia maziwa yanayotoka Kenya *packing* zake na utunzaji wake ni tofauti na maziwa yaliyoko Tanzania. Kwa hiyo, sambamba na kununua hizo mashine ndogo ndogo za huko vijijini vile vile tuwe na mashine nzuri kubwa ambazo zitafanya kazi sawa sawa na hizo za wenzetu nchi zingine. Tusiogope kununua hizo mashine. Mheshimiwa ataogopaje kununua hizo mashine wakati tayari tutakuwa tumeshamuidhinishia fedha hapa Bungeni?

Mimi mwenyewe nitasema zipite zote zilizoombwa na nitasema kwa Baraza la Mawaziri lipitishe zote. Kwa hiyo, tukinunua hizo mashine tutaweza kupata mafanikio na afya zetu zitakuwa nzuri huku nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kuboresha ni kwamba kuna hawa *Extension Officers.* Sasa hivi *Extension Officers* wengi wanahudumia kibiashara, lakini ni watumishi wetu wa Serikali na hoja kubwa ya msingi ni kwamba dawa wananunua kwa hiyo, hawezi akakupa bure. Kwa sababu vitu kama hivi ni vya hatari kwa sekta hii, ningeshauri kwamba kuwe na duka la Serikali ambalo wale *Extension Officers* pekee ndiyo wawe wanaruhusiwa kununua hapo kwa nusu ya bei, hiyo hela nyingine Serikali iweke hapo, *what's the problem? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Extension Officer* ndiyo awe mwenye ruhusa tu ya kununua pale dukani, anakwenda kufanya kazi yake katika kijiji husika au mtaa husika anam-*charge* nusu bei na yule mtu anajua kabisa kwamba ni mtu wa Serikali amekuja kunihudumia. Kuwe na tofauti ya *Extension Officer* wa Serikali na mfanyabiashara wa kawaida ambaye labda ni mtaalam tu. Ni lazima tu-*differentiate* kati ya *Extension Officer* ambaye Serikali imemuweka pale kwa ajili ya kuhudumia na huyu ambaye ni mfanyabiashara tu ili tujue kwamba huyu ni mtu wa Serikali na kilio cha wanyonge ni Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwamba pamoja na kuwa kuna vitu vingi, lakini kuna hizi mbegu za wanyama, mbegu za chupa ambazo wanatumia sasa hivi kibiashara hao *Extension Officers* ni bei kubwa, lakini kama utawapa nusu bei ya vitu vyao kwenye duka la Serikali na ukaboresha na ruzuku ikaenda vizuri hakuna mtu atakayepeleka *fake* kwa mwananchi wakati anajua Serikali itambana. Kwa hiyo, watakuwa na adabu nzuri ya kufanya kazi na shughuli itakwenda vizuri huko nje yaani vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia kuhusu mambo ya majosho. Mambo ya majosho ni muhimu sana kwa sababu toka nimekuja Bungeni hapa kuna kilio hicho, majosho hayana dawa, majosho hayana dawa, majosho hayana dawa. Kikubwa zaidi utakuta kwamba katika Wilaya zetu asilimia 50 ya Tanzania nzima hakuna hata hao *Extension Officers,* wako sehemu chache tu, nayo ni matatizo ya fedha. Lakini tukikubaliana sasa kwamba Muswada huu tumeanza na kwa sababu tumeanza nao basi tuongezee fedha Wizara hivyo majosho yatapata dawa au *Extension Officers* watapata huduma nzuri na hao ng'ombe watahudumiwa tutazalisha ng'ombe wazuri na maziwa yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako bei ya ng'ombe Botswana ni shilingi 400,000/= ni mkubwa, ni mzuri, anapendeza. Lakini ng'ombe wetu shilingi 70,000/= au shilingi 100,000/= ndiyo mkubwa au shilingi 120,000/= ukienda hapo Pugu unapata. Sasa kama hatuwezi kuamka huku ambapo tupo tunafumbuliwa macho, tunatoa matongotongo kwa ajili ya kujua kwamba kumbe kuna kitu ambacho tulikuwa tunaacha nyuma yaani ruzuku kwa wafugaji, tuweze kusaidiwa ili tuweze kupiga hatua. Kwa hiyo, naomba hilo litiliwe maanani sana. Hizi *packing* nilizosema kama tuta-*pack* vizuri, tukiangalia maziwa yetu tunavyo-*pack* utakuta robo tatu yanamwagika kwenye gari. Kwa hiyo, tuwe na vitu vizuri vya ku-*pack* hayo maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niipongeze Serikali kwa kushirikisha wadau kwa sababu wadau walikuja na wakaelezea yote. Lakini pamoja na maelezo ya wadau bado dalili ya kuomba fedha za kusaidia huduma kutoka Serikalini ilikuwepo na mimi nilisema kwamba nitakuja Bungeni nipige kelele kwamba Sekta hizi za uzalishaji zipate fedha za kutosha tusiwawekee *break.* Hiyo hela haiendi nyumbani kwa Mheshimiwa Edward Lowassa wala kwa mtu gani, inakwenda kwenye huduma ambayo itatusaidia sisi wote Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono kwamba ng'ombe Kusini wawepo. Nilikuwa katika kupitia mambo kidogo hapa *section* ya 17

kuhusu ku-*register*. Nilielezwa, lakini sasa wale wenye maziwa madogo yaani wale wanaozalisha kidogo kidogo wanawauzia hawa tuliowaandikisha, nimegundua kwamba wanawauzia hawa ambao tutawa-*register*. Sasa wakiwauzia hawa ambao tutawa-*register* hatuna uhakika wa ubora wa yale maziwa ambayo tunatoa kule. Nimegundua kwamba kuna Kampuni moja huko Musoma ambayo ni *Musoma Diary Milk* inanunua kwa watu wadogo wadogo kabisa. Sasa kama tunatoa masharti kwa yule mtu tunayemuandikisha, lakini yeye anachukua maziwa kule ya watu ambao tulisema ni *owners risk,* ile *owners risk* itarukia kule kule kwa yule mtu ambaye tulifikiri kwamba ametimiza masharti yetu.

Kwa hiyo, tuangalie kuanzia chini tusiseme kuna mtu ambaye tunafanya ni *owners risk*. Tuangalie kuanzia huyo wa kwanza na zamani ilikuwa hivyo, huwezi kukamua ovyo ovyo tu maziwa yako yaani maziwa ya ng'ombe halafu ukauza bila kukaguliwa na hawa *Extension Officers*. Sasa hivi kazi hiyo imepungua kwa sababu Mheshimiwa Lowassa hana pesa, tumpe fedha ili arudishe ule utaratibu wa zamani wa kuhudumia mifugo yetu na tuweze kuendelea vizuri na afya zetu ziwe nzuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale wote ambao walikusudia kuchangia Muswada huu ama wamepata nafasi au wamebaki watatu tu ambao tutaendelea nao kesho nao ni Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Hawa ndiyo wamebaki kwenye Muswada huu.

Baada ya hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu asubuhi.

*(Saa 01.35 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 16 Aprili, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*